**25 APRILI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 25 Aprili, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, karibu.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

**MHE. BAHATI K. NDINGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu tuendelee.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Sulemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, aulize swali lake.

Na. 160

**Hitaji la *X-Ray* na *Ultrasound* Kituo cha Afya Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya Bukene kitapatiwa mashine ya *x-ray* na *ultrasound?*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seleman Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Bukene kinatoa huduma za kiuchunguzi ambapo kwa sasa kina mashine ya *Ultrasound*. Aidha, kituo hiki hakina miundombinu ya jengo la kuwezesha utolewaji wa huduma za *X-Ray*. Serikali itaendela kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya pamoja na ununuzi wa mashine za uchunguzi ikiwemo *X-Ray* na *Ultrasound* kwa ajili ya vituo vya huduma nchini ikiwemo Kituo cha Afya cha Bukene, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suleman Jumanne Zedi.

**MHE. SELEMAN J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Tangu mashine hii ya *Ultrasound* ifungwe pale Bukene, hakujawahi kuwa na

mtaalam wa hii mashine, na kwa hiyo, wagonjwa wanapofika pale hawapati huduma hii, na badala yake wanapelekwa Kituo cha Afya cha Itobo kilichopo zaidi ya kilometa 20: Je, Serikali inaweza kutoa maelekezo maalum kwa Mganga Mkuu wa Halmashauri au Wizarani ili mtaalam wa *Ultrasound* apelekwe, awe *station* pale kwa sababu hakuna tija yoyote kuwa na mashine ya *Ultrasound* wakati mtaalam wa kuiendesha hayupo na, kwa hiyo haifanyi kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa jengo mahususi kwa ajili ya kuweka mashine ya *X-Ray* katika Kituo cha Afya cha Itobo linakamilika; je, ni nini *commitment* ya Serikali sasa ya kuweka mashine hiyo mara tu jengo hilo litakapokamilika pale Kituo cha Afya cha Itobo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suleman Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imepeleka mashine ya *Ultrasound* katika Kituo cha Afya hiki cha Bukene, lakini safari ni hatua. Tulianza kwanza kuandaa mazingira kwa maana ya kandaa majengo na kupeleka mashine. Sasa hatua inayofuata ni kupeleka mtaalam wa mashine ya *Ultrasound* ili aanze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshatoa maelekezo. Nitumie fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzenga kuangalia ndani ya wilaya kufanya *internal redistribution* ya *staff* kwa ajili ya kwenda kutoa huduma ya *Ultrasound,* na Ofisi ya

Rais, TAMISEMI tutaangalia uwezekano wa kupata mtaalam mwingine kwa ajili ya kwenda kuongeza nguvu kule Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na Jengo la *X-Ray* katika Kituo cha Afya cha Itobo, ni kweli Serikali inaendelea na ujenzi na mara baada ya kukamilika jengo lile, mashine ya *X-Ray* itapelekwa ili tuendelee kutoa huduma kwa wananchi wa Itobo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, nimekuona.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kituo cha Afya Mlalo ni miongoni mwa vituo vikongwe kabisa ambavyo havina huduma ya *X-Ray*: Je, ni lini Serikali itahakikisha sasa kituo hiki kinapata huduma hiyo ya *X-Ray* kwa sababu kinahudumia zaidi ya kata tisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyetu vyote vya afya kote nchini vimewekwa kwenye mpango mkakati wa kujenga majengo kwa ajili ya huduma za upimaji na huduma za *X-Ray* na *Ultrasound* zikiwemo. Kwa hiyo, naomba nilichukue hili ili tuweze kufanya tathmini kwenye Kituo hiki cha Afya cha Mlalo tuone uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kujenga Jengo la *X-Ray* na baadaye kuweka mashine kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 161

**Jimbo la Busanda kuwa Wilaya**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, lini Wananchi wa Busanda watapatiwa Wilaya ya Busanda kama ilivyopendekezwa na Baraza la Madiwani, *DCC* na *RCC* Geita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 24/02/2021 Mkoa wa Geita uliwasilisha mapendekezo ya kuanzisha Wilaya mpya ya Busanda kwa kugawa maeneo ya Wilaya za Geita na Chato. Kwa kuwa mamlaka nyingi zilizoanzishwa bado zina upungufu wa miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya utawala na huduma za kijamii, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakapokamilisha maboresho ya miundombinu na huduma kwenye mamlaka zilizoanzishwa, itaendelea na taratibu za uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala ambayo yatakakidhi vigezo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa uboreshaji huu ni kazi ambayo imepangwa *(planned activity):* Je, Serikali imepanga kukamilisha lini hii kazi ya uboreshaji wa maeneo ambayo iliyaanzisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Jimbo la Busanda lina wananchi takribani zaidi ya 700,000; ina kata 22, lakini ina tarafa mbili tu: Ni lini Serikali itaongeza idadi ya tarafa ili wananchi waweze kufikiwa kwa urahisi zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa miundombinu katika Halmashauri zetu ni zoezi ambalo sasa linaendelea na Serikali imeshajenga majengo mapya ya Halmashauri zaidi ya 115 na inaendelea na ujenzi wa majengo ya Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, na pia tutakwenda kwenye ngazi za kata. Kwa hiyo, zoezi hili ambalo linaendelea kutekelezwa ni la muda, na mara litakapokamilika kutokana na upatikanaji wa fedha, basi tutakwenda kwenye hatua nyingine ya kuona uwezekano wa kuanzisha mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na kuanzisha tarafa katika Jimbo hili la Busanda, namwomba Mheshimiwa Mbunge na pia nielekeze Halmashauri kufuata taratibu za uanzishwaji wa tarafa, kwa maana ya kufanya vikao kwenye ngazi ya *DCC*, *RCC* na kuwasilisha kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tathmini ifanyike na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi, nimekuona.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Vikao vya *DCC* na *RCC* wakati mwingine majibu yake yanachelewa kutoka Serikalini: Je, ni lini Serikali itatupatia majibu ya mabadiliko ya jina la Mji wa Mugumu kuwa Mji wa Serengeti kama lilivyopitishwa na vikao vya *DCC* na *RCC*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amsabi Mrimi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa maelekezo na utaratibu wa taarifa na maamuzi na mapendekezo ya *DCC* na *RCC* kuletwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI yako wazi. Nisisitize kwamba baada ya vikao hivyo, Makatibu Tawala wa Mikoa wahakikishe kwamba taarifa zinafika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jina la Mugumu kwenda kuwa Serengeti, naomba tulichukue hili tukatazame limefikia hatua gani, tuone maoni ya wadau na baadaye Serikali itatoa maamuzi lipi linakwenda kufanyika? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea sasa na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 162

**Ujenzi wa nyumba za madaktari Iringa**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za madaktari wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imejenga nyumba 50 za watumishi zenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 katika Hospitali za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwemo nyumba moja katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauriano yanaendelea ndani ya Serikali ili kukamilisha mchakato wa kuhamisha gereza la mkoa ili kutoa nafasi ambayo itawezesha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kuendelea na upanuzi wa huduma

mbalimbali ikiwemo ni pamoja na ujenzi wa nyumba za Madaktari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Vile vile nitoe masikitiko yangu makubwa sana kwa haya majibu aliyotoa, kwa sababu mchakato huu wa kuhamisha gereza ili hospitali iweze kufanya kazi vizuri siyo wa leo wala wa jana, ni wa muda mrefu sana; je, huu mchakato ni lini utakamilika? Kwa sababu haya majibu nimekuwa nikipatiwa muda mrefu, naomba leo anipe jibu, lakini siyo la mchakato tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa niaba ya akina mama wa Mkoa wa Iringa naomba kumpongeza Daktari Bingwa wa Magonjwa ya akina mama, Dkt. Mwakalebela. Kwa kweli anawatendea haki akina mama, na vifo vya watoto vimepungua; lakini tunayo changamoto ya muda mrefu sana kwa Daktari Bigwa wa Upasuaji wa Mifupa. Wananchi wa Iringa wanapata ajali nyingi sana, hata jana kuna ajali pale Kitonga imetokea; hili tatizo tumeshalileta muda mrefu Serikali, lakini hatupatiwi Daktari, wananchi wanapata shida kuja Dodoma au kwenda Dar es Salaam: Je, ni lini sasa huyu Daktari Bingwa wa Upasuaji atakuja katika Mkoa wetu wa Iringa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia huduma za afya, siyo tu kwa Hospitali ya Mkoa wa Iringa, lakini kwa Wilaya zake za Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni mchakato utaisha lini? Namwomba Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye twende pamoja Wizarani na tutamwonyesha mchakato ulipofikia na tutaendelea kwa pamoja tuumalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia Hospitali ya Mkoa, siyo suala la majengo tu, ni suala la *skills* zilizopo pale na teknolojia iliyosimikwa kwenye hospitali. Kwa hiyo, ni kazi. Ukisema uchomoe hiyo teknolojia haraka ukahamisha, utavuruga huduma za afya kwenye mkoa. Kwa hiyo, ndiyo maana mambo mengi yanachelewa pamoja na mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu Daktari Bingwa wa Mifupa, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya, Bunge liliopita, kwa hospitali yetu ya Iringa kwa mchakato unaoendelea sasa hivi ndani ya Wizara kuhamisha madaktari, Iringa wanahitaji kupelekewa Daktari wa Mifupa, Daktari wa *ENT* na Daktari wa *Neurologist*. Kwa hiyo, tumelipokea na litafanyiwa kazi mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, nimekuona.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Manyamanyama inatoa huduma kwa wananchi wa zaidi ya Mkoa wa Mara pale Bunda Mjini, lakini wana changamoto ya nyumba ya watumishi wa afya. Ni lini sasa mtatupatia nyumba mbili ya watumishi wa afya katika Hospitali ya Manyamanyama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie Mbunge hongera kwa swali lake zuri, nawakumbuka watu wake huko Bunda. Nimwambie tu kwamba kwa nafasi zilizotolewa zaidi ya 21,000 tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tuone ni namna gani tunaweza tukatatua hilo tatizo mapema zaidi kwenye nafasi zilizotoka sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake.

Na. 163

**Kuongeza tija katika kilimo Mikoa ya Kanda ya Kati**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwa na Sera ya kuongeza tija katika sekta ya kilimo kwenye Mikoa ya Kanda ya Kati?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Kilimo ya Taifa ya mwaka 2013, inatambua umuhimu wa kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo. Kupitia sera hiyo, maeneo ya

kipaumbele ya kuongeza tija ni pamoja na kuimarisha utafiti, kuongeza upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo (mbegu, mbolea na viuatilifu), kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji, kupima udongo, kuimarisha matumizi ya zana bora za kilimo na kuimarisha huduma za ugani katika kanda zote za Ikolojia nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza miradi ya umwagiliaji katika Mikoa ya Kanda ya Kati – Dodoma, Singida na Tabora kwa kujenga mabwawa saba na skimu za umwagiliaji kumi; uimarishwaji wa Vituo vya Utafiti vya Tumbi, Makutupora na Hombolo; usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima; na uimarishwaji wa huduma za ugani ikiwa ni mkakati katika utekelezaji wa Sera ya Kilimo ya Taifa ya Mwaka 2013.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa mwaka jana Mkoa wa Dodoma hatukupata mbegu za mtama mfupi lakini vile vile mbegu ya alizeti hatukupata na nataka kupata majibu ya Serikali. Serikali ina mkakati gani kwa msimu unaokuja ili kwanza tupate uhakika wa mbegu ambao tumekuwa hatupati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la jingine la pili ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba yapo mabwawa saba ambayo miongoni yatajengwa Dodoma. Je, mabwawa hayo ni yapi na yataanza kujengwa lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza la kuhusu mbegu za alizeti na mtama mfupi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika msimu ujao wa kilimo wakulima wa Mkoa wa Dodoma pia watanufaika na utoaji wa mbegu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu mabwawa. Katika jibu langu la msingi nimetamka mikoa mitatu kwa maana ya Tabora, Dodoma pamoja na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa ambayo tunayo mpaka yanaendelea hivi sasa ni mabwawa ya Msagali pale eneo la Mpwapwa, Bwawa la Membe ambalo litakuwa lina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo milioni 12 lakini vile vile Lyamalwaga ambayo iko Nzega, vile vile Kongogo ambayo iko Bahi na mengine akiyataka kwa orodha nitamtajia yote katika Mkoa wa Dodoma, kwa sababu ya muda naomba niyataje haya machache. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swalli nalotaka kuuliza ni swali namba 163.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza tija kwenye zao la korosho ambao kwa msimu uliopita imeuzwa kwa bei ya chini na ya kutupa na kuwaletea hasara wananchi wa Mtwara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sera yetu ya Kilimo ya mwaka 2013 kipengele cha pili (2)(3) likiwa ni lengo la pili la malengo 10 ya sera ya kilimo imeeleza kuhusu tija katika mazao yote ya kilimo hapa nchini. Yako mambo lazima tuyafanye kama Serikali ili wakulima wetu waweze kulima kwa tija. Jambo la kwanza ni kuhakikisha tunapima afya ya udongo kutambua virutubisho ndani ya udongo ili tuwashauri vizuri wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni kuimarisha utafiti na cha tatu ni huduma za ugani na ugawaji wa pembejeo. Nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwenye korosho tunajua kuna changamoto nyingi na jana tulikuwa na kikao cha tathmini tumeyaona na tutayafanyia kazi ili wakulima wa korosho na wenyewe waweze kulima kwa tija tuweze kufikia malengo na matarajio ambayo tumejiwekea kama nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge aulize swali lake.

Na. 164

**Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji wa Kyakakera**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji wa Kyakakera uliopo katika Kata ya Kyaka?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya umwagiliaji ya Kyakakera ni miongoni mwa skimu zinazounda Bonde la Mto Ngono lenye ukubwa wa hekta 11,700 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na kufanya usanifu wa kina. Mpaka sasa, Serikali ipo katika hatua za kukamilisha manunuzi ya kumpata mshauri mwelekezi atakayefanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Mpango na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Bonde la Mto Ngono limetengewa bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ambapo jumla ya hekta 3,000 zimepangwa kuendelezwa katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji na Skimu ya Kyakakera itakuwa miongoni mwa skimu za awamu ya kwanza zitakazoendelezwa wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya bonde la Mto Ngono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa majibu ya Serikali japo niseme nina imani sana na Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Antony Mavunde kwa sababu skimu hii imekuwa ni muda mrefu imetelekezwa bila mafanikio. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, skimu hii imeshatumia zaidi ya shilingi milioni 944 ambazo hazikuleta tija yoyote. Je, ni nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba sasa inaumalizia mradi huo na unakuwa na tija kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wakulima wa eneo hilo walisimamishwa kuendelea na ulimaji katika skimu hiyo mwaka 2013, leo ni miaka 10 tunapoongea hakuna chochote kinachoendelea. Naomba Serikali itoe matumaini kwa wananchi hao kuweka *commitment* kwamba sasa skimu hii inaenda kukamilishwa na wananchi wanarudi pale kwa ajili ya kulima kilimo cha umwagiliaji na kuleta tija katika maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni *commitment.* Nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ni dhamira ya Serikali ya kuhakikisha ya kwamba tunaendeleza kilimo cha umwagiliaji kupitia miradi mbalimbali. Mradi wa Kyakakera ambao umekaa muda mrefu ni mkombozi mkubwa wa wakulima. Tumekwisha mwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuhakikisha wanalipitia eneo hili na tulikamilishe kwa haraka ili wakulima wetu waanze kutumia mradi huu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sisi wenyewe hatupendi kumwona Mkulima amekaa bila kufanya kilimo lakini mradi huo ulikuwa chini ya *DADP* na ziko changamoto ambazo zilijitokeza katika utekelezaji wa hii miradi na hivi sasa tumejikita kuhakikisha kwamba tumejenga miradi ambayo itakuwa ni bora na ya kudumu muda mrefu ili wakulima wetu wasipate shida. Miaka

10 ya wakulima ni mingi nataka nikafute kilio hicho kwamba Mkurugenzi Mkuu akienda huko aifanye kazi hiyo vyema wakulima hao waweze kuanza kulima mapema kabisa katika msimu unaokuja hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutenga zaidi shilingi milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Endagaw. Kwa sasa mkandarasi ameweza kusimamishwa. Je, ni lini Serikali itatuletea mkandarasi ili aweze kukamilisha ujenzi wa skimu hiyo na uweze kuleta tija kwa fedha za Serikali lakini kwa wananchi pia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mbunge amekuwa mfuatiliaji mzuri katika eneo hili. Ni kweli mkandarasi aliyekuwepo Endagaw tulimsimamisha na kumwondoa lakini tuko katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi mwingine ambaye atakwenda kukamilisha kazi hiyo kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wape tu matumaini wakulima wako kwamba kazi itakamilika na watafanya kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa bajeti inayoendelea sasa Bunge hili lilipitisha uanzishwaji wa Skimu ya Ibanda Geita na Igaka Sengerema. Ni lini utekelezaji wa skimu hii utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Ibanda ni moja kati ya miradi muhimu sana katika Mkoa wa Geita na hususan Jimboni kwa Mheshimiwa Kanyasu. Habari njema ni kwamba tumekwisha kutangaza juu ya Bwawa la Ibanda na muda siyo mrefu pia tutatangaza kumpata mkandarasi kwa ajili ya skimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo, sasa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba aulize swali lake.

Na. 165

**Tija ya misamaha ya *VAT***

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Misamaha ya *VAT* inayotolewa inaleta tija kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha misamaha ya kodi inakuwa na tija katika uchumi na jamii kwa ujumla, orodha ya bidhaa na vifaa vinavyostahili msamaha wa kodi inaandaliwa, kuhakiki orodha ya bidhaa na vifaa, kuhakikisha mwombaji anajaza fomu maalum inayothibitisha ununuzi wa bidhaa au vifaa husika pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara dhidi ya misamaha iliyotolewa ili kuthibitisha iwapo matumizi ya bidhaa au vifaa vilivyosamehewa kodi vimetumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kutekeleza matakwa ya kisheria husika katika ufuatiliaji na tathmini ya misamaha ya kodi ikiwemo Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ili kuhakikisha kuwa misamaha ya kodi inatolewa kwa kuzingatia sheria na inatumika kama ilivyokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningeomba kuuliza maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitoa misamaha ya kodi ya *VAT* kwa taulo za kike na vishikwambi lakini tija haikuwepo kabisa. Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na changamoto hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa misamaha hii ya *VAT* kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi imekuwa ikichelewa sana na inasababisha hata miradi ya maendeleo mingi kutokamilika kwa wakati. Je, Serikali inachukua hatua zipi kutatua kadhia hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Issa Mtemvu kwa ufuatiliaji wa misamaha hii ama harakati za ulipaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba misamaha ilitolewa kwa vishikwambi na taulo za kike lakini wako ambao walienda kinyume na taratibu lakini Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwemo kufuta misamaha hiyo na kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hao wamelipa kodi inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili mikakati ambayo imechukuliwa na Serikali. Moja ni kubadilisha sheria, sheria iliyokuwepo zamani lazima Baraza la Mawaziri ndiyo litoe msamaha lakini kwa sasa iko juu ya Waziri wa Fedha na Mipango. Jingine Serikali imetengeneza mfumo ambao kwa sasa inaratibu misamaha yote hiyo na inatolewa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Hassan Chande kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa aulize swali lake.

Na. 166

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Wilayani Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu hadi Kamuli Wilayani Kyerwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Jimbo la Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakamilisha usanifu wa miradi ya maji Wilayani Kyerwa mwezi Mei, 2023 na baadae kufuata taratibu za manunuzi ya Wakandarasi. Ujenzi wa miradi utaanza mwezi Septemba, 2023 na utanufaisha jumla ya vijiji 20 vikiwemo Vijiji vya Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu na Kamuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mradi wa Kilela, Lutunguru na Isingiro, mradi huu unajengwa kwa awamu mbili, mkandarasi anakaribia kukamilisha awamu ya kwanza. Ni lini Serikali itatangaza awamu ya pili ili mradi huu uweze kukamililka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wataalamu walifika kwenye Kata ya Businde, Bugala, Kibale pamoja na Kikukuru wakapima vijiji vichache ili wananchi waweze kupatiwa maji lakini adha ni kubwa wananchi wanayoipata. Je, Serikali iko tayari kupima vijiji vyote vya kata hizo ili wananchi hawa waweze kupatiwa maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Bilakwate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi ule wa kwanza alioutaja unaopita kwenye vijiji vya Kilela, Lutunguru ni kweli

awamu ya kwanza umeshakamilika na sasa tunaelekea kwenye usambazaji na tunatarajia mwezi Mei kuweza kuutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la pili, maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge ni kweli vijiji vilishapimwa na tayari tunaendelea na utaratibu wa kuona kwamba maeneo haya yote ambayo miundombinu ya maji kuyapitia iko mbali basi tuweze kuchimba visima na tayari tumshukuru Mheshimiwa Rais ile mashine ambayo ilipaswa kufika Mkoa wa Kagera sasa inatarajiwa kutoka Karagwe na kuelekea Kyerwa lakini vile vile vijiji ambavyo havikupimwa tunavitarajia navyo vipimwe viingie kwenye mpango wa kupata maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, nimemuona Mheshimiwa Leonard Chamuriho.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo langu la Kalenga limekuwa halina chanzo cha uhakika cha maji ambacho kinaweza kikapeleka maji kwenye kata zaidi ya moja. Mfano Kata ya Masaka haina maji kabisa. Je, ni lini sasa Serikali itatafuta chanzo kimoja kikubwa ili tuweze kupeleka maji zaidi ya kata moja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo haya anayotaja Mheshimiwa Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Ni kweli

vyanzo vyake vinapata changamoto kama chanzo kile cha Nyamlenge kwa sasa tunashuhudia wote kwamba kinaendelea kujaa mchanga lakini watu wetu wa bonde wanaendelea kufanya kazi nzuri kuhakikisha vyanzo vinabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo yote ya Kalenga tunaendelea kufanya utafiti, tunatarajia kutumia labda Mto Lyandemberwa ambao unaweza ukasaidia eneo la Kalenga kupata maji safi na salama yakiwa bombani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leonard Chamuriho.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali. Kijiji cha Kyabakari kimekosa huduma ya maji kwa muda wa miezi mitatu sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kijiji hicho kinapata maji japo kuwa kuna mradi mkubwa wa maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leonard Chamuriho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji ambacho kinaweza kikakosa maji miezi mitatu na tayari kina miundombinu ya maji ni suala la kufuatilia changamoto ilipo. Naomba nilichukue tutahakikisha maji yanarejea kwa wananchi ili kuondokana na kero ambayo wanaipata kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi kwa majibu hayo ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba aulize swali lake.

Na. 167

**Kuvirejesha vituo vidogo vya treni vya Njage na Itongowa - katika reli ya *TAZARA***

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini vituo vidogo vya treni vya Njage na Itongowa katika reli ya *TAZARA* vitarejeshwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA* ilipokea barua za maombi ya kufunguliwa kwa vituo vidogo vya Njage na Itongowa katika vipindi tofauti tangu mwaka 2022. Tathmini iliyofanywa ilibainisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kidogo cha Itongowa. Kituo hiki kinachoombwa kuanzishwa kipo kati ya Stesheni kubwa za Chita na Mngeta. Katikati ya Stesheni mbili hizo za Chita na Mngeta kipo kituo kidogo cha siku nyingi cha Ikule. Kituo hiki cha Ikule kipo kilometa sita kutoka aidha Chita ama Mngeta. Kituo cha Itongowa kinachoombwa kuanzishwa kitakuwa

kilometa sita kutoka Mngeta stesheni au kilometa saba kutoka Ikule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kidogo cha Njage. Kituo hiki kinachoombwa cha Njage kipo kati ya Stesheni kubwa za Mngeta na Mbingu ambazo treni za abiria zinasimama. Umbali kati ya stesheni hizo ni kilometa 18 yaani Mngeta na Mbingu. Kitongoji cha Njage kipo katikati Mngeta na Mbingu yaani kilometa tisa kutoka kila upande, Mngeta au Mbingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Wizara imeelekeza sasa *TAZARA* ifanye tathmini ya haraka kwa kina kuona uwezekano wa kuanzisha vituo hivi vilivyoombwa na Mheshimiwa Mbunge ili wananchi wasitembee umbali mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo (a) na (b)

(a) Ningependa kujua kwa kupata *commitment* ya Serikali, ni lini sasa vituo hivi vitarejeshwa?

(b) Wananchi wa maeneo haya Njage na Itongowa wamekuwa wakipata adha kubwa sana ya usafiri hasa ukizingatia wakati huu wa masika sisi Wananchi wa Mlimba usafiri wetu mkubwa ni treni ya *TAZARA*. Sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri lini atakuwa tayari kuambatana nami tupande treni hiyo ya *TAZARA* anaposema hapo Ifakara mpaka Mbingu tushuke kwenda Njabi umbali wa kilometa tisa halafu apate hiyo adha na yeye ataona najua atachukua hatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wanaotumia vituo hivi vya Stesheni ya Reli ya *TAZARA* kwamba tarehe 28 Ijumaa ya wiki hii tunatuma timu ya wataalam kwenda kufanya tathmini ya kina. Itafanya kazi hii kwa wiki moja, mpaka tarehe 06 ya mwezi wa tano, na watatoa taarifa ama ripoti ambayo hiyo itakuwa msingi wake katika kufanya maamuzi. Hata hivyo swali lake la pili ni lini kwenda huko, Mheshimiwa Mbunge mimi na wewe nitakwenda pamoja na wewe siku ya *weekend* wakati vikao vya Bunge vinaendelea, tutaomba ruhusa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Spika ili twende kuona adha hii kwa wananchi na hatimaye kufanya maamuzi sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, swali langu ni dogo; kwa kuwa huduma ya treni ya mwendokasi nchini inasubiriwa kwa hamu kubwa sana.

Je, ni lini shirika hili litaanza kutoa huduma kati ya Dar es Salaam na Dodoma?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Reli yetu ya *TRC* hususan katika mradi wetu wa *SGR* kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma awamu ya kwanza tutaanza kutoa huduma kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro. Hivi ninavyosema tumeshafanya *testing* katika vituo vyote *signal* na treni la Mkandarasi na kwa maana hiyo tunachosubiria sasa ni kuja vichwa na hivi vichwa tunategemea vitakuja ndani ya mwezi ujao ili ianze kufanya hii *station* ya *SGR,* ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naomba nitoe pole nyingi kwa wananchi wa Jimbo la Hai kutokana na mafuriko yanayoendelea sasa hivi kwenye maeneo mbalimbali. Swali langu, ni lini Serikali itajenga kituo kidogo cha treni eneo la Rundugai sokoni?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mbunge wa Hai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambau kwamba kituo hiki cha reli, treni ya abiria inayotoka Dar es Salaam kwenda Arusha ni miongoni mwa maeneo ambayo pia tunashusha. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaweka fedha kwenye bajeti ijayo, nitaomba wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tuunge mkono ili tujenge kituo hiki kiweze kutumika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Makete.

Na. 168

**Kuanza ujenzi wa barabara ya Chimala – Matamba hadi Kitulo**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, ni hatua gani ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Chimala – Matamba hadi Kitulo imefikiwa na lini ujenzi utaanza?

**MWENYEKITI;** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Chimala – Matamba yenye urefu wa kilometa 20.1 ni barabara ya Wilaya ambayo imekasimiwa kwa *TANROADS* kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024. Baada ya kukasimiwa *TANROADS*, barabara yote kuanzia Chimala – Matamba hadi Kitulo ambayo itakuwa na urefu wa kilometa 41.1 itaingizwa kwenye mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Makete nipende kuishukuru Serikali kwa kuichukua barabara hii ya kutoka Chimala kuelekea Matamba kilomita 20 ambayo ina kona 53 kwenye milima. Barabara hii ni ya kiuchumi na barabara ya kimkakati, kwenda *TANROADS* ni msaada mkubwa ambao Serikali imeweza kutusaidia.

Je, kwa kipindi hiki ambacho mvua nyingi zinaendelea Matamba na Makete ni upi mpango wa Serikali kutusaidia barabara hii iweze kupitika kwa sababu wananchi wanaitumia sana kwa muda mwingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna barabara kutoka Kitulo kuelekea Busokelo kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, upi mkakati wa Serikali kuimalizia barabara hii ili iweze kujengwa irahisishe mawasiliano kati ya wananchi wa Makete na wananchi wa Jimbo la Busokelo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Matamba hadi Kitulo ni eneo ambalo kwa kweli Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi lina mvua nyingi sana, na *TANROADS* wako barabarani kuhakikisha kwamba inapitika lakini yako maeneo ambayo tunashindwa kufanya kazi kwa sababu ya mvua nyingi sana ambayo inaendelea kunyesha. Hivi tumewaagiza *TANROADS* kuhakikisha kwamba muda mwingi wawepo maeneo hayo ili pale ambapo jua linatoka basi waweze kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mawasilano na kurekebisha zile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa swali lake la pili, kuhusu kutengeneza barabara ya Kitulo kwenda Busokelo; hii barabara haikuwepo, ni mpya. Atakubaliana nami kwamba tumeshaanza kuifungua na tumeifungua yote, kinachosubiriwa sasa ni kuikamilisha, kwa maana ya kujenga makalavati na kuweka changarawe ili kuhakikisha kwamba wananchi wa pande hizi mbili wanaweza kuwasiliana, na hasa wananchi wa Busokelo kwenda Hospitali ya Ikonda ambao wanaihitaji sana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru;

Je, ni lini Serikali itafanya upembuzi yakinifu kwa barabara ya Mwembe-Mbaga na hatimaye kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakazi wa milimani?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, barabara nyingi sana tunategemea kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Tukiwa tunajua tunaelekea mwisho wa utekelezaji wa ilani ya chama, kwa hiyo tunaamini barabara zote ambazo zimeainishwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tutazifanya kuanzia mwaka huu na mwaka ujao wa fedha, ikiwepo na barabara ya Mheshimiwa Mbunge aliyoisema, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, nilikutaja Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; Barabara ya Mpunze-sabasabini ipo Nyagholo mpaka Igwamanoni imekatikakatika haipitiki kabisa na imepandishwa kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*. Ni nini mkakati wa Serikali kwa ajili ya kuijenga barabara hii angalau hata kujua maeneo yaliyokatika ili wananchi waweze kupita kwa urahisi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara aliyoitaja ilikuwa inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*, na ndiyo kwanza imekuja sasa *TANROADS*. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa wa Ushetu pamoja na wananchi wa Ushetu, kwamba tumesikia, na ninamwagiza Meneja wa Mkoa wa Shinyanga, cha kwanza aende akahakikishe kwamba yale maeneo yote ambayo yamekatika anayarejesha ili kuwe na mawasiliano. Pia aweze kufanya tathmini ili maeneo yote yale korofi tuweze kuangalia namna ya kuyarakabati vizuri ili yaweze kupitika muda wote hata kipindi cha masika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikutaja Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Kuchauka atafuata.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya Mafinga Mgololo inapita katika majimbo matatu, kwa maana ya Mafinga Mjini, Mufindi Kaskazini na Mufindi Kusini. Katika majibu ya Serikali mara zote wanasema kwamba barabara hii iko chini ya

utaratibu wa *EPC+F,* na kwamba Wizara ya Ujenzi wao wameshamaliza kazi suala hili liko hazina. Sasa wananchi wa Wilaya ya Mufindi wanatuuliza sisi Wabunge wao watatu, kwamba;

Je, hawa wa ujenzi hawawezi kwenda huko fedha kuwaambia sasa watoe fedha hii barabara ianzwe kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwakikishie Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Kihenzile na Mheshimiwa Kigahe, kwamba barabara aliyoitaja ya hawa Wabunge wote ipo na hakuna barabara ambayo imeachwa katika huu mpango wa *EPC+F*. Kwa kweli taratibu zinakwenda vizuri tupo tunakamilisha taratibu na nadhani kipindi cha bajeti hizi barabara zote nategemea tutaziwakilisha na zianze utekelezaji, ikiwepo na barabara ya Mgololo hadi Mafinga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Kuchauka atamalizia na Mheshimiwa Furaha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Sera ya Taifa letu ni kuunganisha barabara za mikoa kwa lami, lakini sisi Mkoa wa Lindi haujaunganishwa na Mkoa wa Morogoro kwa barabara hata ya vumbi.

Je, Serikali inasema nini juu ya kuunganisha sisi Mkoa wa Morogoro na Lindi kwa barabara angalau ya changarawe pale Liwale na Mahenge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge Kuchauka, kwamba mwaka huu wa bajeti tumependekeza kwanza tufanye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kati ya Liwale, Ilonga hadi Mahenge ili hii barabara tuweze kuifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara inapita kwenye Mbuga ya Selous, na limekuwa ni ombi kubwa sana la wanalindi akiwepo Mheshimiwa Kuchauka sasa tumeiweka kwenye mpango wa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo kama bajeti yetu itapita tuna uhakika hiyo kazi itakuwa imeanza kuunganisha Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha nilikutaja.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mwanango kupita Kahama inayounganisha Mkoa wa Shinyanga ili kukuza uchumi na ipo kwenye ilani ya uchaguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tulishakamilisha usanifu wa kina na tumeanza kuijenga kwa hatua na hasa maeneo ambayo ni ya mijini, ikiwa ni mpango wa Serikali kutafuta fedha kuijenga barabara ya Mwanangwa-Solwa hadi Kahama kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 169

**Ahadi ya ujenzi wa kivuko - Tunduma**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa kivuko cha waenda kwa miguu katika eneo la Kisimani barabara kuu itokayo *Custom* kwenda Sumbawanga itaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika eneo la Kisimani lililoko kwenye Barabara ya Tunduma kwenda Sumbawanga,

kumewekwa alama za kuvuka (Pundamilia – *Zebra Crossings*) na Taa za kuongoza magari na watembea kwa miguu zimewekwa sehemu mbili; ya kwanza mita 300 kutoka eneo la Kisimani na ya pili mita 500 kutoka taa za kwanza za kuongozea magari na watembea kwa miguu (*Traffic Signals*). Aidha, Serikali ina mpango wa kujenga kivuko cha chini (*underpass*) katika eneo la Kisimani na utekelezaji wake unategemea upatikanaji wa fedha ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa kuwa kukosekana kwa hicho kivuko kumekuwa kunatokea ajali za mara kwa mara. Kwanza kwa wananchi vilevile kwa bajaji pamoja na magari. Sasa nilitaka nifahamu kwamba kwa nini Serikali isione kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuharakisha upatikanaji wa hizo fedha ili hicho kivuko kiweze kujengwa ili kuwapunguzia adha kubwa wanayopata wananchi wa Mji wa Tunduma; vilevile ikizingatiwa kwamba ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo analolisema na changamoto anayoisema mimi binafsi ninaifahamu na ni sehemu ambayo na mimi barabara hii naitumia sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba jitihada

zimeshaanza kuchukuliwa kuweka hizo alama za kusaidia kupunguza ajali. Mpango wa Serikali kwa sasa tayari wanafanya usanifu kuangalia namna ya kuweka kivuko cha chini badala ya kivuko cha juu kwa sababu tumekuja kuona kwamba mara nyingi vivuko vya juu havitumiki sana kuliko vivuko vya chini. Kwa hiyo nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua na iko tayari kuwalinda wananchi na kivuko hicho kitajengwa kama kilivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Asenga nimekuona.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwa wananchi wetu wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara kwa mafuriko makubwa ambayo wameyapata, na tunashukuru Mungu mpaka sasa hakuna kifo kilichotokea, tunapambana kupeleka misaada kwa wananchi ambao wameathirika sana. Mafuriko haya yamethibitisha kwamba kuna miundombinu ya *TANROADS* katika Kalavati la Sheli ya Madinga kwenda Rumomo na Kalavati la Kwa Shungu kwamba ni madogo na ndio yalichangia kupatikana kwa mafuriko.

Je, Serikali ina hatua gani za haraka za kurekebisha makalavati haya kama tulivyotembea na Mheshimiwa wa Wilaya na kujionea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake sijalisikia kitu ambacho anataka Serikali ilifanye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari rudia swali lako kwa ufupi.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafuriko ambayo yameikumbuka Halmashauri ya Mji wa Ifakara imethibitika kwamba kuna makalavati mawili, kalavati la kwa Sheli ya Madinga Rumemo na Kalavati la Sheli ya Kwa Shungu kwenye barabara hizo za *TANROADS* ni madogo kuliko wingi wa maji unaopita.

Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kurekebisha makalavati hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Meneja wa Mkoa wa Morogoro aende hilo eneo ambalo makalavati ni madogo atafute namna ambavyo anaweza akaongeza hayo makalavati kwa haraka ili kuondoa changamoto ambayo inawakuta wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa Mheshimiwa Asenga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya pamoja na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 170

**Kuwalinda watoto walio kwenye ndoa na umri mdogo**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MHE. HAWA S. MWAIFUNGA)** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda watoto walio tayari kwenye ndoa wakiwa na umri mdogo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshmiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasichana walioolewa pia wameunganishwa na fursa za kujiunga na vyuo na kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali kupitia vyuo vya ufundi *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Ustawi wa Jamii ambavyo vipo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mafunzo watakayopata yanaweza kuwasaidia kujiajiri au kuajiriwa katika ya Sekta ya Umma na Binafsi.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imekuwa ikiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wasichana kwenye fani mbalimbali za uwanagenzi zikiwemo shughuli za kilimo cha mazao ya muda mfupi, ufugaji, uhunzi wa vifaa na bidhaa, ususi, uchoraji, ushonaji, pamoja na shughuli nyingine sawa na mahitaji yatakayoibuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza miradi hii kwa lengo la kumwinua na kumwezesha mtoto wa kike ili aweze kuwa huru na kujitegemea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kwa niaba.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na kutaka kuwasaidia watoto hawa wa kike lakini mahakama ilisema sheria ya ndoa ibadilishwe;

Je, ni lini Serikali mtaanza kutekeleza sheria hiyo na kubadilisha ili tusiwe na watoto wengi ambao wanaozeshwa wakiwa na umri mdogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, umezungumzia suala la kusaidia *program* nyingi zinazoendelea mikoani. Ni kweli mmeweka ada ndogo nyingine hadi shilingi 10,000 lakini mahitaji ya wasichana hawa kwenda kusoma ni zaidi ya 400,000; kwamba, aje na godoro na mambo mengine mengi, hamuoni kwamba mnawaonea wasichana wa vijijini na wanakosa haki ya kuweza kuhudhuria mafunzo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanaidi, Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali la kwanza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali ilitoa maelekezo katika Bunge lako Tukufu, kwamba mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya kurekebisha sheria ya ndoa umekamilika, na kwamba tarehe 26 Aprili, yaani kesho, kutakuwa na kongamano la mwisho kupitia maoni hayo na baada ya hapo Serikali italeta muswada huo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la pili, Mheshimiwa Mwanaidi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la pili la Mheshimiwa Hawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya jitihada mbalimbali ya kuwapa mafunzo walengwa kwa kuwakwamua mabinti wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na kuwafikia katika vijiji vyao ili kuondokana na madhila na kujikwamua kiuchumi ili waweze kuimarika na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Pia hadi kufikia Februari, 2023, jumla ya vikundi 6,127 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu wameunganishwa na kupewa mikopo midogo midogo ambayo inawawezesha kuwainua kiuchumi ili waondokane na mashaka ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameelekeza asilimia 10 za Miradi ya Maendeleo zipelekwe katika mifumo ya kibenki kuwakwamua wananchi wote ili waweze kupata fedha hizo kwa ajili ya kujijengea uchumi na kuimarisha uchumi wao kwa maendeleo ya maisha yao, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara nimekuona, Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kiutaratibu Mahakama inapokuwa imetoa maelekezo kwenye jambo hili la watoto wa kike kuolewa chini ya umri, Mahakama ilishatoa maamuzi kwamba Serikali ilete mabadiliko ya sheria Bungeni.

Swali langu, Serikali imepata wapi nguvu ya kukiuka maamuzi ya Mahakama ya kuleta Muswada wa Sheria Bungeni

na badala yake inakwenda kukusanya maoni ya wadau kuhusiana na sheria hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mahakama ya Rufani kutoa maamuzi ya mwisho kuhusiana na jambo hili, Serikali ilileta Muswada hapa Bungeni. Muswada huo ulipokelewa na kwa maelekezo ya Bunge lako tukufu tulielekezwa na Bunge tukakusanye maoni zaidi. Kwa hiyo ilichokifanya Serikali ni maelekezo ya Bunge, *otherwise* Serikali ilishaleta Muswada hapa. Tumetekeleza hayo maelekezo ya Bunge na tuko tayari kurudi tena kupokea maoni mengine ya Bunge itakavyoona inafaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ubakaji na ulawiti kwa watoto ni zaidi ya uuaji. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuondoa dhamana kwa wale wanaume wanaolawiti na kubaka watoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naona kajiandaa tayari. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhamana ni haki ya

mtuhumiwa na inaweza ikaondolewa tu pale ambapo inaonekana ni muhimu na mazingira yanalazimisha lazima iondelewe. Katika kesi nyingine zote hizi *discretion* ya kuondoa dhamana inabakia kwa Mahakama, endapo Mahakama itaridhika kwenye mazingira haya, huyu mtu asipate dhamana, basi hatapata dhamana hata kesi hizo za ulawiti na ubakaji kama ambavyo Mheshimiwa ameuliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaidi naona maswali yako mengi leo yamegusa Katiba na Sheria.

Kwa hiyo tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 171

**Kuvitangaza Vita vya Majimaji katika Gazeti la Serikali**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatangaza kumbukizi za Vita vya Majimaji vilivyoanzia Kijiji cha Nandete katika Gazeti la Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vita ya Maji Maji ilipiganwa kuanzia Mwaka 1905 hadi 1907, kusini mwa nchi yetu katika baadhi ya Mikoa ya Lindi, Iringa, Morogoro na Ruvuma, ikiwa

na lengo la kupinga utawala na ukandamizaji wa ukoloni wa Mjerumani. Mwaka 2006, Makumbusho ya Taifa ilianza kuadhimisha kumbukizi ya miaka 100 ya Vita ya Maji Maji na inaendelea kuadhimishwa tarehe 26 Februari kila mwaka, katika Manispaa ya Songea kwenye eneo la Makumbusho ya Vita vya Maji Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, huadhimisha siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa tarehe 25 Julai kila mwaka, ili kuwaenzi mashujaa wetu waliopoteza maisha katika vita na operesheni mbalimbali za ukombozi wa nchi yetu na Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya kutangaza eneo lolote au lengo la kihistoria iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Mambo ya Kale, chini ya Kifungu cha Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 ya Mwaka 2002, kifungu cha 3(1) na (2). Sheria hiyo inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Malikale kutangaza eneo lenye sifa ya Urithi wa Taifa kwenye Gazeti la Serikali. Endapo Mheshimiwa Mbunge ana nia ya Kijiji cha Nandete kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya Kumbikizi ya Vita vya Maji Maji, basi namshauri awasilishe ombi hilo Wizara husika ili liweze kufanyiwa kazi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tangu mwanzo wakati Mheshimiwa Waziri, anatoa jibu nimeonyesha masikitiko makubwa sana kwa swali langu kutojibiwa, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri, katika *paragraph* ya mwisho ya swali lake ameeleza ukweli kwamba swali hili lilipaswa kujibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, tena ametaja mpaka sheria ambayo inaipa Mamlaka Wizara ya

Maliasili na Utalii, kutangaza hizi kumbukumbu za kihistoria kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikiombe kiti chako kwa kuwa swali halikujibiwa. Siku ya Ijumaa tarehe 28, saa tatu asubuhi niiombe Wizara ya Maliasili na Utalii, iweze kuja kujibu swali hili kwa ufasaha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu swali lako ambalo umeulizwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu mchango wa Mheshimiwa Francis Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunafanya kazi kwa kuwajibika kama Serikali moja na ndiyo maana nimemjibu Mheshimiwa Francis Ndulane kwamba pamoja na swali kuja Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikaelezea sheria ambayo inatuongoza. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi tutashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, kuhakikisha tunashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kumwongoza na kupitia utaratibu ambao nimeueleza wa kuangalia hiki Kijiji cha Nandete kama kina sifa ya kuingia kwenye kumbukumbu za nchi yetu za maeneo ambayo yalitumika katika vita vya maji maji, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamedi Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa maeneo mengi Mikoa ya Lindi na Mtwara yalihusika katika harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika hasa Kusini mwa Bara la Afrika.

Je, Serikali ina mpango gani kuharakisha maendeleo katika maeneo hayo ambayo yaliathirika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali la Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama yangu Tecla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa mchango wa wapigania uhuru kwa ajili ya nchi yetu kupata Uhuru kutoka kwa Mkoloni fidia yake haipimiki. Kwa sababu mashujaa hawa walijitoa kwa ajili ya nchi yetu kupata uhuru na tunajifunza kutoka kwao kwamba uzalendo huu lazima tuuendeleze na tuwe tayari kupigania nchi yetu bila kutegemea fidia, lakini vile vile nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mama yangu, Mheshimiwa Tecla, Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kutekeleza Ilani inapeleka maendeleo kote nchini ikiwemo maeneo ya Mikoa ya Kusini. Kwa hiyo ningependa kumwondoa wasiwasi Mipango ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi iko makini katika kuhakikisha maendeleo tunayapeleka kote ikiwemo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake kwa niaba Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 172

**Kukusanya madeni ya *TANESCO***

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukusanya madeni ya *TANESCO* katika taasisi kubwa ili shirika hilo liweze kujiendesha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia mwezi Machi, 2023, *TANESCO* inadai jumla ya shilingi bilioni 244 kutoka kwa wateja wake mbalimbali wakiwemo wateja wa umma na wateja binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia ukuaji na kuwezesha ukusanyaji wa deni, kwa upande wa Serikali, Serikali inahakikisha inatenga na kuweka fungu la fedha za kulipia huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* imeweka mikakati ya kukusanya na kuzuia madeni kwa kuweka mita za LUKU, kuhamasisha na kufuatilia madeni na inapobidi basi kukata huduma ya umeme kwa mteja mwenye deni kubwa na sugu ili liweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Tauhida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa mpango huu wa Serikali umekuwepo kwa siku kidogo lakini bado ulipaji wa madeni umesuasua. Je, ni mikakati gani ya dharura ambayo Serikali itachukua kuhakikisha kwamba ulipaji unafanyika kwa uharaka na kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa bilioni 244 ni pesa nyingi sana inazodai Serikali, je, Serikali ina mikakati gani ya kisheria ambayo itachukua kuhakikisha kwamba hizi pesa zinalipwa kwa kuwapeleka hawa watu Mahakamani au kwa njia nyingine yeyote, lakini pesa hizi zilipwe ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya shirika na nchi yetu kwa jumla?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme hizi pesa bilioni 244 kwa sehemu kubwa ni deni la nyuma na ni deni la siku nyingi. Ni deni ambalo lilikuwepo kipindi kile ambacho bado tulikuwa hatujaanza kutumia LUKU na tulikuwa hatujaweza kukusanya vizuri. Kwa hiyo ni madeni ya siku nyingi na tunaendelea kuhangaika nayo kama ambavyo Mheshimiwa amesema tuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba tunayakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mikakati iliyopo ya kukusanya pesa hizi kwanza ya dharura kabisa tayari *TANESCO* imeshakamilisha taratibu za kuwapata madalali wa kukusanya madeni wawili ambao taratibu zinakamilishwa na siku siyo nyingi wataanza kuingia mtaani na kukusanya fedha hizi ambazo ziko kwa watu mbalimbali ili kuweza kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili upande wa Serikali, Wizara na *TANESCO* tumeshirikiana na kuiomba Serikali kupitia Hazina ilipe pesa hii yote inayodaiwa kwa *TANESCO* ili *TANESCO* iweze kupata fedha ya kuweza kujiendesha. Sasa kwenye mikakati inayokuja ya nini kinafanyika pamoja na hizi LUKU ambazo tumeshaweka, lakini zinawekwa LUKU zinaitwa *boundaries meters* ambazo zitawekwa kwenye ngazi ya Mkoa ili kila Mkoa tujue inatumia umeme kiasi gani. Pia tunakwenda kwenye kuweka *smart meters* ambazo zitatusaidia kujua mtu anapogusa *meter* yetu moja kwa moja tukiwa ofisini tutaiona na kuhakikisha kwamba tunashughulikia suala hilo mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama, tusingependa tufike huko mapema kwa sababu Mahakama inachukua muda mrefu na *process* nyingi, lakini wale wateja ambao tunashindwana kabisa hata zile hatua za kukata umeme, basi tunapelekana Mahakamani. Zipo kesi kadhaa ambazo tumeenda Mahakamani na tumeshinda na tuna uhakika kwamba deni hili tutalikusanya lote ndani ya muda mfupi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Taasisi ambazo zinaongoza kudaiwa deni na *TANESCO* ni Taasisi za Serikali tena zile andamizi, za binafsi *either* hamna kabisa au ni moja, mbili au tatu, nataka kujua sasa kwa sababu kuna Taasisi zingine zinatoa huduma kwa wananchi,

haziwezi kukatiwa umeme. Je, ni kwa nini Serikali isiweke *pre-paid meter* kwa hizi Taasisi zote ili ziweze kuwajibika na kuona kipaumbele cha kwanza cha ku–*fine* kuweza kulipia umeme kuliko hivi sasa kuweza kuleta usawa kati ya wananchi na hizi Taasisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii bilioni 244 Serikali inadaiwa kama bilioni 86 hivi kwa hiyo bilioni mia moja ishirini na kitu zinazobakia wateja binafsi na watu mbalimbali ndiyo wanaodaiwa. Hao wateja binafsi ni wale wateja wadogo wadogo na kama nilivyotangulia kusema, madeni haya hasa ni ya kipindi kile ambapo hatukuwa na *meter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa utaratibu tunaokwenda nao tumeshaongea na wenzetu Serikalini kukubaliana kwamba pesa inayolipwa kwenye zile taasisi kwa ajili ya kulipia huduma ya umeme, hii ya deni ikatwe *at source* kwa maana ya kutoka Hazina, lakini hizi pesa nyingine zinazokuja basi tuweke utaratibu mzuri ambazo tutaweza kuzikusanya. *Pre paid meters* na na hizo *smart meters* zinazokuja tutahakikisha tunazi–*roll* kwenye maeneo yote ili kila mmoja aweze kuwa na wajibu wa kulipa deni lake kwa wakati tukihakikisha kwamba sasa ni kwa manufaa yetu sisi wazalishaji na watumiaji wa umeme tunaozalisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Byabato kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa

Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 173

**Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kuhusu Ndoa za Utotoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa Muswada wa Sheria ya Ndoa ulifikishwa kwenye Kamati ya Bunge lako Mwezi Februari, 2021, kufuatia maamuzi ya Mahakama ya Rufani kati kesi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Rebecca Gyumi, Rufaa Na.204/2017 iliyotokana na kesi Na.5/2016 ya Mahakama Kuu iliyotaka Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho ili umri wa mtoto kuingia katika ndoa iwe kuanzia miaka 18. Kamati ya Bunge baada ya kupitia iliona upo uhitaji wa kushirikisha wadau wengi zaidi ili kupata maoni zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumwarifu Mbunge kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeshakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa kidini, viongozi wa kimila, viongozi wa

vyama vya siasa, wanafunzi, wataalam mbalimbali wa afya, makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo watu wenye ulemavu. Aidha, tarehe 26 Aprili, 2023, Wizara imeandaa Kongamano la Sheria ya Ndoa litakalofanyika katika Hotel ya Morena, Jijini Dodoma, kesho saa saba. Naomba niwakaribishe Wabunge wote na itakuwa live *TBC* kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tu baada ya Serikali kukamilisha zoezi hili la mwisho, inatarajia kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa Bungeni katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naishukuru Serikali tunategemea kuletewa Muswada, lakini nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; sheria hizi zinazohusu ukiukwaji wa haki za kibinadamu ikiwepo ndoa za utotoni, ukeketaji, ubakaji, ulawiti, ukatili wa kijinsia pamoja na kutungiwa sheria kali ikiwepo miaka thelathini jela kwa kosa la ubakaji, lakini matendo haya yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kubwa. Sababu kubwa ni kutoa mwanya wa makosa hayo kusuluhishwa kijamii. Je, sasa Serikali inasimamiaje sheria hizi kuhakikisha kwamba inaondoa ukiukwaji wa haki za kibinadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Sheria ya Ndoa inasemaje kuhusu wanawake kumiliki mali? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleza vyema kwamba tatizo siyo sheria, tatizo ni sisi wanajamii kutokuwafikisha hao wahalifu kwenye vyombo vya dola. Nitoe rai kwa wanajamii kwamba makosa haya yanaumiza Watanzania wenzetu, Watoto, wasiyavumilie kwa kuyasuluhisha nyumbani na kuisha, wapeleke kwenye vyombo vinavyohusika hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria kama ambavyo sheria zetu zinataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge amehitaji kufahamu Sheria yetu ya Ndoa inasemaje katika umiliki wa mali. Sheria hii ya Ndoa siyo kwamba ni mbaya kiasi hiki ambavyo watu wanafikiria, ina vifungu zaidi ya 167, ni vizuri kabisa, vichache tu ndiyo vina usumbufu Kifungu cha 13 na 17. Sheria yetu hii imesema katika Kifungu kile cha 56 wanandoa wote wana haki ya kumiliki mali, iwe ni mke iwe ni mume wote wana haki sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah nilikuona na Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mahakama ilishatoa uamuzi kuhusu suala la umri la watoto wadogo kuolewa Tanzania. Serikali haioni kuendelea kukusanya maoni ni kukiuka amri ya Mahakama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria amesema vizuri kwamba, tulishaleta kwenye Bunge lako hili Tukufu na nimesema kwenye majibu yetu ya msingi, kwamba ni Bunge hili na Kamati hii ilitutaka turudi kwa wananchi ili tupate wigo mpana wa kuwahusisha Watanzania katika hili. Kwa sisi hatuna tatizo na niwakaribishe Waheshimiwa Wabunge kesho wenye nafasi mje tunamaliza hayo majadiliano katika Hoteli ya Morena kesho Saa Saba Mchana, tukishakamilisha tutaleta sheria hii Bungeni. Ilikuwa ni agizo la Bunge siyo la kwetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na utayari wa Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa lakini bado kuna Sheria za Kimila kandamizi kwenye mirathi. Je, ni kwa nini sasa Serikali isione haja ya kupitia upya Sheria za Kimila ili kuondoa ukatili wa kijinsia na ukandamizaji wa wanawake?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kwamba sheria zetu za kimila, tuna sheria tatu za mirathi, tuna ya kidini Sheria ya Kiislamu Sheria ya Kimila na *Indian Succession Act.* Hizi sheria zote zimekuwa zikizungumzia jinsi gani watu wananweza kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sheria ambazo tumezisema katika Bunge hili kwamba tunazifanyia marekebisho ni pamoja na sheria hizi za mirathi za kimila ili Watanzania wote wapate haki zao. Kwa sababu katika sheria ambayo Mheshimiwa Mbunge ame-*refer* wanawake wengi hawapati haki zao, wanakuwa katika *marriage* lakini watoto wanapewa mali wakati wale akina mama ambao wamezaa wale watoto wanakosa haki. Kwa hiyo, tunakuja na marekebisho ya sheria hizo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunamalizia Wizara yetu ya mwisho, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, aulize Sali lake.

Na.174

**Kudhibiti utapeli unaofanywa kupitia namba za simu za nje**

**MHE. MAULID SALEH ALI** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti utapeli unaofanywa kwa kutumia namba za simu za nje?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Jimbo la Welezo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utapeli ama kwa lugha nyingine ni udanganyifu unaofanywa kwa kutumia simu za nje hudhibitiwa kwa kushirikisha Mamlaka za Udhibiti kwenye nchi ambako namba zinazotumika zimegawiwa. Mamlaka hizo huchukua hatua stahiki kwa kadri wanavyopokea taarifa zinazohusiana na utapeli huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya za Kikanda na Kimataifa kama vile *ATU, EACO, CRASA, CTO, ITU, UPU, PAPU* na kadhalika. Ushirikiano uliopo kupitia Jumuiya hizi husaidia sana kwenye utatuzi wa masuala mengi yakiwemo yanayohusu utapeli unaofanyika kwenye mitandao ya simu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha mfumo wa TEHAMA na kudhibiti usalama wa mawasiliano nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inaongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari imeshatoa mkakati *(National Cyber Security Strategy)* ya mwaka 2018, mwaka 2023 ambao ni kuhakikisha kwamba kuna usalama katika huduma zote zinazofanyika katika mtandao. Vilevile

tunayo timu ambayo inaitwa Mwitikio wa Kukabiliana na Majanga ya Kompyuta (*TZ-CERT)* ambayo yenyewe kazi yake ni kuhakikisha kwamba pale changamoto kama hizi zinapotokea basi tunahakikisha tunaenda kuchukua hatua ili kuzuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine tunao mfumo wetu ambao unaitwa *Tele Traffic Management System* ambao kazi yake ni kuhakikisha kwamba inadhibiti mambo mawili, kwanza kabisa ni kufatilia miendendo ya mawasiliano yote yanayoingia ndani ya nchi, vilevile ni kuangalia namna mapato yanavyotokea na namna ambavyo tunaweza tukaya–*contrive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Daud, nilikuona.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utapeli hata hapa kwetu Tanzania unafanyika kwa kuomba michango na kadhalika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na *TCRA* ili kuweza kuwaelewa wahalifu hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi. Ni kwamba Serikali ina mkakati maalum na zaidi ya hapo Serikali kwa kushirikiana na Vyombo vya Dola vinaendelea kuratibu na kufatilia mienendo yote ya matumizi ya simu na zile ambazo zinahusika katika utapeli basi huwa

zinakamatwa na baadae tunazifungia, sambamba na hilo tunaendelea kutoa elimu kwa Watanzania ili kuelewa pale ambapo simu za namna hii zinapowafikia ili wajue kwamba ni hatua gani waweze kuchukua kwa kuwasiliana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - *TCRA*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau nilikuona. Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kwamba siyo utapeli wa simu za nje tu lakini pia kuna utapeli wa kiholela wa kuongezewa au kupandishwa vyeo humu nchini. Utapigiwa simu umeambiwa umepandishwa cheo kwa hiyo usubiri barua yako. Kwa hiyo na hili pia linatumika katika njia za simu. Je, Serikali ina mpango gani kuhusu suala hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utapeli unakuja kwenye picha tofauti tofauti. Kuna picha ya kutafutiwa kazi, picha ya kupandishwa vyeo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, lakini sana sana tunachokiomba tu kwa Watanzania ni kwamba pale wanapopokea changamoto kama hizi basi waweze kuwasiliana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ili tuweze kuchukua hatua stahiki nasi tukiwa tunaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kupitia kitengo chao cha *Cyber*

*Crime Act*. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa ushirikiano huu basi tutaweza kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita dhidi ya matapeli siyo vita dhidi ya Serikali peke yake, ni vita dhidi ya umma na kwa pamoja tukifanya kazi kwa pamoja tutahakikisha kweli tumetokomeza changamoto kama hii. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi atakuwa wa mwisho.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa matapeli wanaotumia *lane* za ndani ambazo zimesajiliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tuna mfumo unaoitwa *Tele Traffic Management System,* kwanza kabisa tunabaini simu ambazo zinafanya mambo ambayo hayastahiki na mpaka sasa tunatumia mfumo huo ambao unatumia simu za majaribio *(Test Calls)* na tukitumia baadae tunabaini na tangu Julai mwaka 2022 mpaka sasa ni takribani simu 826,951 zilibainika kufanya mambo ambayo yasiyostahili lakini kati ya hizo tayari tumeshachukua hatua na bahati mbaya sana tunapochukua hatua katika mambo haya huwa hatuyatangazi kwa sababu tunakuwa tumepeleka kwenye mamlaka ambayo yanatakiwa kutoa hukumu na katika mchakato huo bado kunakuwa na ukusanyaji wa taarifa na *evidences* ambazo zitafanya kwamba hukumu iweze kutoka vizuri, ndiyo maana

huwa hatutangazi lakini Serikali imejizatiti kuhakikisha kwamba jambo hili linaendelea kukomeshwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la mwisho.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Serikali ilianzisha mfumo wa usajili wa *biometric* tukawa tunatumia vile vile *finger prints* kwa lugha nyingine ili kuweza kuwa–*track* ama kuwe na *database* ya kila mtu ambaye ana namba ya simu. Lakini ukweli ni kwamba watu wanatapeliwa kwa namba za simu ambazo zimesajiliwa. Sasa swali kwenu Serikali, unataka kukiri mbele yetu kwamba wizi wa kwenye mitandao ya simu unafanyika kwa makusudi baina ya makampuni ya simu na matapeli na mfumo wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema, changamoto ya utapeli kwanza kabisa ni jukumu letu sisi sote kushirikiana, lakini Serikali tunaendelea kutoa elimu kwa umma ili waweze kujua namna ya kujidhatiti na kupambana na changamoto kama hii. Pamoja na hivyo Serikali sasa imeendelea kuwekeza Zaidi katika mifumo ya TEHAMA ili iweze kudhibiti katika picha ya ki–*technical* zaidi kuhakikisha kwamba mambo haya yanaendelea kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ki ukweli hasa kipindi cha *pandemic,* mambo kama haya ndiyo yanakuwa mengi zaidi, kwa sababu mawasiliano yanakuwa siyo ya moja kwa moja, simu ndiyo zinakuwa *medium of communication*. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa kuimarisha mifumo ya TEHAMA

tutaendelea kuhakikisha kwamba changamoto hii inaendelea kupungua katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la dharura.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawapa fursa naomba nimalizie kutangaza matangazo.

**MBUNGE FULANI:** Haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika na sasa ni wakati wa matangazo ya wageni waliopo Bungeni leo hii.

Kuna wageni ambao wapo kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika, ambao ni Ndugu Mary Makondo hawa wote ni kutoka Wizara ya Katiba na Sheria ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro kutoka Wizara ya Katiba na Sheria ambao ni Ndugu Mary Makondo, Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Khatibu Kazungu - Naibu Katibu Mkuu, karibu Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Elisante Ole Gabriel - Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu Mtendaji wa Tume ya Utumishi wa

Mahakama, karibu sana. Karibu sana Profesa na hongera kwa makofi hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Karibu sana Profesa naona Waheshimiwa Wabunge wanakufurahia sana Profesa Elisante Ole Gabriel. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Wilbert Martin Chuma - Msajili Mkuu wa Mahakama, karibu sana. Pia tunaye Jaji Gerson Mdemu - Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Dodoma, karibu sana. Tunaye Dkt. Adam Mambi - Jaji Mahakama Kuu Dodoma pia, karibu. Ndugu Shamilah Sarwat - Msajili wa Mahakama Kuu, karibu sana. Ndugu Enziel Mtei - Naibu Katibu Mkuu, Tume ya Utumishi wa Mahakama, yuko upande ule kule.*(Makofi)*

Ndugu Angela Anatory - Kabidhi Wasii Mkuu, Mtendaji Mkuu pia karibu sana. Ndugu Lina Msanga - Naibu Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Mtendaji pia Mkuu. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Silvia Matiku - Mwakilishi wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Karibu sana. Tunaye Ndugu. Michael Luena - Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. Boniphace Luhende - Wakili Mkuu wa Serikali. Karibu, Ndugu Goodluck Chuwa - Naibu Mkuu wa Chuo, Taaluma Tafiti na Ushauri, karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa January Msofe - Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, karibu. Ndugu Sylivester Mwakitalu - Mkurugenzi wa Mashtaka, karibu. Ndugu Javeline Rugailuza - Mwakilishi Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Profesa Zakayo Lukumay - Naibu Mkuu wa Taasisi ya *LST.,* Mheshimiwa Mathew P. M. Mwaimu - Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, karibu sana.

Mheshimiwa Mohamed Hamadi - Makamu Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Patience Ntwina - Katibu Mkuu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, karibu sana; Dkt. Amina Msengwa - Mwenyekiti wa Bodi ya *RITA*, karibu sana; Ndugu Lulu Ng'wanakilala - Katibu Mtendaji Kituo cha Huduma za Kisheria *(LSF)*, karibu sana; pia tuna Ndugu Christina Kamili Ruhinda - Mkurugenzi Mtendaji Mtandao wa Watoa Huduma na Msaada wa Kisheria *(TANLAP),* karibu sana; Ndugu Anna Henga - Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)*, karibu sana; Ndugu Mariam Othman - Mkurugenzi Mtendaji Chama cha Wanasheria Tanganyika, karibu sana na pia tuna Dkt. Ines Kajiru - Amidi wa Shule Kuu ya Sheria *UDOM*, karibu sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hao tunao wageni wengine hawa wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mke wa Waziri wa Katiba na Sheria Ndugu Florah Ndumbaro, karibu sana. Kwa makofi hayo inaonekana hao wote wawili mpo vizuri kwenye Bunge karibuni sana. Pia tuna watumishi kutoka Shule Kuu ya Sheria - *UDOM,* karibuni sana watumishi wetu kutoka Shule Kuu ya Sheria Dodoma *(UDOM)*. Wawakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka tunao pia hapa, wawakilishi wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao Watendaji Watumishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Watendaji wale pale karibuni sana. Pia tunao wadau kutoka Benki ya *NMB,* karibu, pale nimemuona Ndugu Msolo karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, kutoka Jimboni kwake, Songea Mjini, wakiongozwa na Meya wa Manispaa ya Songea; Mheshimiwa Mwinyi

Msolomi. Karibuni sana wageni hao wa Mheshimiwa wetu, Waziri wa Katiba na Sheria katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni 30 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. Wale kule, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, ambaye ni dada yake, Ndugu Daria Mwalitwangiro kutoka Jijini Dodoma, karibu sana Dada yake Mheshimiwa Ng'wasi. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Ndugu Morandi Mtani na mfanyabiashara wa madini kutoka Geita, Ndugu John Kishomba, karibuni sana wageni hao wa Mheshimiwa Kanyasu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kalenga, Mkoa wa Iringa, Ndugu Hamza Chang'a na Ndugu Ojuku Mgumba, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 60 wa Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kilimo Cha Sokoine *(SUA)* kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Nusrat Hanje, ambao ni wasanii wa *Stand Up Comedy* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wasanii wetu kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga, ambaye ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Jijini

Dodoma, Ndugu Billy Chidabwa, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia, tuna mgeni wa Mheshimiwa Rose Businga, ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Judith Muta, karibu sana Ndugu Judith. *(Makofi)*

Pamoja na wageni hao, tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wageni 100 na walimu 10 kutoka shule ya awali na msingi, *Green Harvest* ya Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu pamoja na walimu kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna Maafisa 15 wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanaotoa huduma katika viwanja vya Bunge, wakiongozwa na Ndugu James Mwanakatwe, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tangazo lingine lisilo la wageni ni tangazo ambalo linatoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na kikao cha ujumbe kutoka Uganda, leo tarehe 25 Aprili, 2023 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, uliopo ghorofa ya tano katika jengo la utawala. Kwa hiyo, hilo ni tangazo la hao wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Kuna wageni wengine watatu, wamesahaulika hapa nilikuwa sikupata majina yao, wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda katika Bunge letu. *(Makofi)*

Haya, tuna Miongozo. Mheshimiwa Godwin Kunambi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 (1) na Kanuni ya 55 (3)(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema siku ya jana barabara inayotoa huduma kwa mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini, Morogoro – *Njombe Border* ilikatika na hadi sasa hakuna mawasiliano kwa wananchi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, naomba urudie tena mwanzo.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee. Ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) na Kanuni ya 55(3)(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema siku ya jana...

**MWENYEKITI:** Jana siyo mapema Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya jana, barabara inayotoa huduma katika mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini, yaani Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Mbeya ilikatika. Ninavyozungumza, hadi sasa wananchi hawa wanaohudumiwa na barabara hii hawana mawasiliano eneo la Udagaji, Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja hii ili Bunge lako kama itakupendeza, liahirishwe kwa muda kujadili hoja hii, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sijampa ruhusa bado ya kusema kwa undani ili tuweze kujadili. Ehe, Mheshimiwa Kunambi, naomba nikupe dakika chache kwa ajili ya kuweza kutueleza kwa kina ili tuweze kujua kama ni dharura kweli na inahitaji kuahirisha Bunge.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia barabara ya Morogoro – *Njombe Border,* kwanza ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Ni barabara ambayo inategemewa kutoa mazao kwenye mikoa yote niliyoitaja kupeleka kwenye mikoa ambayo haishughuliki na shughuli za kilimo kama vile Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa mingineyo, hata kule Kilimanjaro. Ni barabara muhimu kwa Taifa letu kwa sababu ni barabara ya kimkakati na ni ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, barabara hii kwa wananchi wa Mlimba, hususan na Mkoa wa Njombe, wanategemeana. Mwananchi wa Mlimba ili apate huduma ya afya, rufaa yake ni Ikonda, Makete; na mwananchi wa Njombe ili apate huduma, rufaa yake halikadhalika, anaweza kuja Ifakara, *Saint Francis* ambayo iko Wilaya ya Kilombero, Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpaka sasa ninapozungumza, kama kuna watu wanaumwa, kama kuna akinamama wanataka wakajifungue Ikonda, hawawezi kwenda kujifungua na kama kuna watu wanataka kwenda Ifakara wakapate huduma hiyo ya afya, hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa mujibu wa kanuni hiyo niliyoitaja ya 55, hasa ya fasili ya (3)(a), jambo hili lina madhara makubwa, siyo tu kwa wananchi wa mikoa hiyo tajwa, basi kwa Taifa letu kwa ujumla, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Naona hoja imeungwa mkono na watu wengi. Pamoja na hayo, naomba nimjibu Mheshimiwa Godwin Kunambi kama ambavyo ameomba kwa mujihu wa Mwongozo huo wa Kanuni ya 54 (1).

Ni kweli, madhara kwa maeneo hayo ambayo ameyataja ni makubwa, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kwa nchi yetu sasa hivi, maeneo mengi yanapatikana na matatizo kama hayo. Hapa asubuhi tumesikia madaraja yamekatika, na maeneo mengine yameathirika kutokana na mvua ambazo zinanyesha bila mpangilio. Kwa hiyo, kutokana na tatizo hilo hilo, hatuwezi kujadili upande mmoja wa nchi na wakati maeneo mengine yanaendelea kuathirika.

Kwa hiyo, naamini Serikali wanaendelea kufuatilia na hata hivyo baada ya maelezo yako na ya wengine ambao wametoa asubuhi kwenye maswali, Serikali itaendelea kufanyia kazi na kuhakikisha kwamba maeneo yanakuwa salama na wananchi wanaendelea kupata huduma kama kawaida.

Nilimwona Mheshimiwa mwingine ambaye alikuwa na Mwongozo. Ni nani?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndulane.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 76 na 53 ya Kanuni zetu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, katika maswali ambayo yaliulizwa leo, mimi nilipata bahati ya kuuliza

swali la msingi namba 171, linalohusema: "Ni lini Serikali itatangaza kumbukizi za Vita vya Majimaji vilivyoanzia Kijiji cha Nandete katika Gazeti la Serikali." Kimsingi swali langu halikupata majibu ya ukweli. Halikupata majibu ambayo swali hili lililenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri, ali-*refer* kumbukizi zilizopo Songea, lakini kwa kawaida tuna kumbukizi za Nandete za Majimaji, na kumbukizi za Songea. Kwa hiyo, katika utangulizi wake alinijibu kwa ku-*refer* kumbukizi zilizopo Songea, hakwenda kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwenye kipengele cha mwisho, naomba nimnukuu, alisema hivi: "Mamlaka ya kutangza eneo lolote au lengo la kihistoria iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Mambo Kale chini ya Kifungu cha Sheria ya Mambo Kale, Sura Na. 333 ya Mwaka 2002, Kifungu cha 3(1) na (2). Sheria hiyo, inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya malikale kutangaza eneo lenye sifa ya urithi wa Taifa kwenye Gazeti la Serikali."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa muktadha huu ni kwamba, Waziri wa Ulinzi alishindwa kunijibu swali langu kwa kadiri ambavyo swali lilikuwa linaelekeza. Kwa sababu, suala lilikuwa ni *GN* ya *Majimaji Festival*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane, umeeleweka. Naomba nikupe majibu ya Mwongozo huo.

Mheshimiwa Ndulane, kama ambavyo amesimama kwa kanuni ambazo amezitaja ni za Mwongozo wa kutojibiwa kiusahihi ambavyo alitarajia yeye, sijui alikuwa ameshajua majibu? Haya.

Sasa naomba nirudi tena kwenye *Hansard,* tuweze kupitia vizuri swali hilo na tuone hayo majibu kama kweli hayajajitosheleza ama yamejitosheleza. Huo ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza mjadala wetu, kuna wageni wengine ambao walikuwa wamesahaulika.

Kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Naomba nitambue uwepo wao, karibuni sana katika Bunge letu. Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Justine Nyamoga ambao wamesahaulika, ambao ni Diwani wa Kata ya Ukwega akiongozwa na Ndugu Genro Myamba. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunakuja kwenye hoja za Serikali. Namkaribisha Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kuja kusoma hotuba yake ya bajeti. Karibu sana.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Mwelekeo wa

Mpango wa Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali, ikiwemo sekta ya sheria, ambapo tumeshuhudia kuimarika kwa mfumo wa utoaji haki, ulinzi wa haki za binadamu na watu, hususan kuimarika huduma za afya, elimu, maji, nishati na huduma za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwasilisha hotuba ambayo imefafanua utendaji wa Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na kutoa Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote waliotangulia kwa mawasilisho mazuri ya hotuba za Wizara wanazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu vizuri. Pia

nampongeza Mheshimiwa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na weledi mkubwa. Nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge hili. Vilevile nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wengine; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Ni matarajio yangu kwamba watatekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Naahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuendelea kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Pia, nampongeze Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Sheria na Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendeleza ushirikiano katika masuala mbalimbali ya Wizara hizi mbili, hususan masuala ya msaada wa kisheria. Nampongeza Mheshimiwa Geofrey

Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kipindi chote ambacho tumeshirikiana akiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria hadi ilipompendeza Mheshimiwa Rais kumhamishia Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nitoe pole kwa Dkt. Boniface Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali na familia kwa kumpoteza mtumishi wa ofisi hiyo muhimu kwa Wizara, marehemu Dkt. Abdul Mussa, Mkurugenzi wa Idara ya Mipango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, aliyefariki kwa ajali ya gari siku ya alfajiri, tarehe 23 Aprili, 2023 akiwa njiani kuja Jijini Dodoma kushiriki uwasilishaji wa hotuba ya bajeti. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umezingatia dira na miongozo mbalimbali ya kitaofa na kimataifa ambayo ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030, Mpango wa Maendeleo wa Afrika 2063, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati akihutubia Bunge la 12 mwaka 2021, Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imeendelea kutoa elimu ya Katiba na Sheria kwa umma kupitia vyombo vya habari vikiwemo redio, runinga, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara, sambamba na kugawa nakala za Katiba kwa wananchi. Aidha, elimu ya Katiba imetolewa kupitia maadhimisho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Wiki ya Sheria na Wiki ya Msaada wa Sheria.

Maeneo mengine ya utekelezaji yanaonekana katika ukurasa wa nane na wa tisa wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Kwa kipindi cha Mwezi Julai 2022 hadi 2023 kulikuwa na jumla ya mashauri 185,291 kati ya hayo mashauri 58,266 ni mashauri yaliyokuwepo mwanzoni mwa Mwezi Julai, 2022 na mashauri 127,025 yalifunguliwa. Kati ya mashauri hayo 185,291 mashauri 134,989 yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 53,264 yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhifadhi, kulinda na kukuza haki za binadamu ni kipaumbele muhimu katika kuhakikisha maendeleo ya Taifa letu. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilishiriki kwenye kikao cha 51 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Vilevile, Wizara iliratibu ziara ya Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu nchini ambapo ujumbe wa kamisheni hiyo ulitembelea eneo la Pori Tengefu la Loliondo, Hifadhi ya Ngorongoro na Kijiji cha Msomera ambapo walishuhudia zoezi la kuhama kwa hiari kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na utawala bora nchini. Ufafanuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu na utoaji huduma ya msaada wa kisheria umeoneshwa katika ukurasa wa 10 hadi wa 25 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea na jukumu la kutunga sera na sheria mbalimbali za masuala ya Kikatiba na kisheria ikiwa ni mikakati

ya kuimarisha na kuendeleza sekta ya sheria. Sera za sheria hizi zitatoa mchango kwa maendeleo ya Taifa na hivyo kufanikisha malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026). Ufafanuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa sera zinazohusu masuala ya kisheria unapatikana katika ukurasa wa 25 hadi ukurasa wa 27 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa miswada 12. Aidha, miswada ya sheria saba ilijadiliwa na kupitishwa kuwa sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki sheria kuu tatu yaani Sheria ya Maafa, Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Sheria ya Uwekezaji, ziliandaliwa katika Lugha ya Kiswahili huku sheria nyingine ndogo 405 zikiandikwa kwa Kiswahili. Taarifa kamili ya uandishi wa sheria imeoneshwa katika ukurasa wa 27 hadi wa 31 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika ngazi mbalimbali za mahakama. Jumla ya kesi za jinai 33,004 ziliendeshwa katika mahakama za wilaya na hakimu mkazi. Kati ya kesi hizo, jumla ya kesi 20,952 zilihitimishwa na kesi 12,052 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mahakama Kuu ofisi iliendesha jumla ya kesi 6,425. Kati ya kesi hizo, jumla ya kesi 1,338 zilihitimishwa na kesi 2,151 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama ya Rufani, ofisi iliendesha kesi za rufaa 1,535. Kati ya hizo, rufaa 267 zilihitimishwa na rufaa 1,268 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uendeshaji wa kesi hizo kiasi cha shilingi bilioni 2,103,868,730 kililipwa mahakamani kama faini katika kesi 5,440. Mali zilizotaifishwa ni pamoja na magari 25, nyumba nne, madini ya dhahabu gramu 3,290.39, tanzanite gramu 6,221.24 na fedha taslimu shilingi 1,494,472,436.75 na dola za Marekani 9,292.34. Taarifa kamili ya uendeshaji wa mashauri imeoneshwa katika ukurasa wa 31 hadi 35 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri ya madai na usuluhishi 6,477. Kati ya mashauri hayo, mashauri 6,440 ni ya Kitaifa na mashauri 37 ni ya kimataifa. Serikali ilikamilisha jumla ya mashauri 582 ambapo mashauri 572 ni ya Kitaifa na mashauri 10 ni ya kimataifa, na kuokoa fedha, jumla ya shilingi trilioni 13.33. Taarifa kamili ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi imeoneshwa katika ukurasa wa 35 hadi 38 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeboresha mfumo wa usuluhishi wa utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa kufanya mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 na kutafsiri Kanuni za Upatanishi na Maridhiano ambazo zinalenga kufanikisha utekelezaji wa usuluhishi wa migogoro nje ya mfumo wa mahakama. Vilevile, Wizara imeandaa miongozo ya mafunzo ya usuluhishi, upatanishi, uendeshaji maridhiano na majadiliano na mwongozo wa kuendesha vikao vya Jopo la Ithibati la Waendesha Usuluhishi, Upatanishi, Majadiliano na Maridhiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2023, Wizara imesajili jumla ya watatuzi wa migogoro 530 watakaotumika katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Kati ya hawa wasuluhishi ni 266, wapatanishi ni 172, waendesha maridhiano ni 35 na waendesha majadiliano ni 57. Taarifa kamili ya eneo hili imeoneshwa katika ukurasa wa 38 hadi wa 40 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi 2023, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini imesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa 767,164, imefanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa 84,133 na vyeti vya vifo 17,197 vya wazazi wa wanafunzi wanaoomba mkopo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hati 17 za watoto wa kuasili zilisajiliwa na kutolewa, jumla ya vifo 26,605 vilisajiliwa. Vilevile, jumla ya ndoa 31,579 na hati za talaka 410 zilisajiliwa. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana kuanzia ukurasa wa 40 hadi wa 44 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha elimu na uhamasishaji wa uandishi na uhifadhi wa wosia unafanyika kwa mujibu wa sheria, Wizara kupitia wakala imeweka kambi katika Viwanja vya Bunge kwa kuweka hema ambapo wataalam wa masuala ya wosia wanaendelea kuwahudumia waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge kuanzia tarehe 24 April, 2023 hadi tarehe 5 Mei, 2023. Naomba kutumia nafasi hii kuwakaribisha katika mabanda hayo ili kupata huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya mapitio ya mfumo wa sheria na tathmini ya utekelezaji wa sheria kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria zinaakisi mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia. Katika kipindi hicho Tume imefanya utafiti wa mfumo wa sheria unaosimamia masuala ya udhamini, mfumo wa sheria

unaosimamia utoaji wa haki katika mahakama za mwanzo, mfumo wa sheria unaosimamia uchaguzi na vyama vya siasa na sheria zinazosimamia usafiri wa majini. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana kuanzia ukurasa wa 44 hadi 48 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya maombi 13 yanayohusu urejeshwaji wa wahalifu wa kimataifa yalishughulikiwa yakiwemo saba ya kuwarejesha watuhumiwa wa makosa ya jinai waliokimbilia nchini kutoka katika mataifa ya nje. Aidha, maombi sita ya kuwarejesha watuhumiwa wa uhalifu waliokimbilia nchi za nje yameombwa na Tanzania kwa nchi ambazo tuna makubaliano ya kubadilishana taarifa za uhalifu. Ufafanuzi zaidi umetolewa katika ukurasa wa 50 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara pamoja na taasisi zake imeendelea kusimamia masuala mbalimbali yanayohusu watumishi kama vile uteuzi, ajira mpya, maslahi ya watumishi, bajeti na masuala ya nidhamu na maadili. Katika kipindi hicho, jumla ya watumishi 52 walipata uteuzi, watumishi 614 ajira mpya, watumishi 29 walipandishwa vyeo, watumishi 59 walihamia Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi 45 walihama, watumishi 319 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 106 walipata mafunzo ya muda mrefu. Watumishi 43 walithibitishwa vyeo, watumishi waliostaafu ni saba, watumishi waliothibitishwa kazini ni 26, watumishi waliopewa onyo ni wawili, watumishi waliofukuzwa kazi ni watatu na waliorejeshwa kazini ni 13. Ufafanuzi wa kina umetolewa katika ukurasa wa 51 hadi wa 57 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, taasisi ilidahili jumla ya wanafunzi 1,348 sawa na asilimia 89.9 ya lengo la udahili wa wanafunzi 1,500 kwa kundi la 35 na 36. Aidha, katika kipindi husika, taasisi imetoa wahitimu 363 wanaostahili kusajiliwa kuwa mawakili na kufanya idadi ya wahitimu waliopata mafunzo kupitia taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia 8,255.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wahitimu katika kipindi husika imeongezeka kwa asilimia 23.9 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Ufafanuzi wa kina kuhusu eneo hili unapatikana katika ukurasa wa 57 hadi wa 59 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; katika kipindi cha Julai, 2022, hadi Machi, 2023, Wizara kupitia chuo imeratibu mafunzo ya awali na elekezi kwa watumishi 237 wa mahakama ya Tanzania. Mafunzo haya yanajumuisha kada za majaji 20, mahakimu 20, madereva 35, makatibu mahususi 80, maafisa hesabu 17, wakaguzi wa ndani nane, maafisa tawala watano, maafisa utumishi nane, wasaidizi wa kumbukumbu 38, maafisa ugavi sita na maafisa TEHAMA wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kimeratibu mafunzo kwa waendesha mashtaka na wapelelezi kwa jumla ya washiriki 250 katika kuboresha utendaji wa kazi ili kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani. Ufafanuzi wa kina kuhusu eneo hili unapatikana katika ukurasa wa 59 hadi 62 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo; katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imetekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mashtaka. Vilevile, Wizara imetekeleza miradi inayohusiana na maboresho

ya mifumo ya huduma za mahakama na taasisi zake pamoja na miradi ya kuimarisha upatikanaji wa haki kwa jamii. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yameoneshwa kuanzia ukurasa wa 62 hadi wa 71 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria wa kikanda na kimataifa, Wizara ilishiriki kwenye Mkutano Maalum wa Saba wa Umoja wa Afrika, Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi za Jumuiya ya Madola, kufanya kikao na Taasisi ya Kimataifa inayosimamia Sheria Binafsi za Kimataifa *(The Hague Conference on Private International Law)* na kikao cha kufanya tathmini ya udhibiti wa fedha haramu na utakatishaji wa fedha na kumbanana na ugaidi. Maelezo zaidi yapo kwenye ukurasa wa 72 hadi 73 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bajeti na fedha zilizopokelewa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023; makusanyo ya maduhuli. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara pamoja na taasisi ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 12,676,201,000.00 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 6,798,115,487.74. Mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa unapatikana katika ukurasa wa 78 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 272,768,278,800.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya hizo shilingi 95,356,423,800.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 112,347,285,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 65,064,570,000.00 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, jumla ya shilingi 53,112,800,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 11,951,770,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea jumla ya shilingi 187,452,301,201.00 sawa na asilimia 68.7 ya shilingi 272,768,278,800.00 zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kati ya hizo shilingi 62,743,442,184.00 ni mishahara sawa na asilimia 66 ya bajeti iliyopitishwa na shilingi 83,054,287,447.00 ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 74 ya kiasi kilichoidhinishwa.

Aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 41,654,571,569.00 sawa na asilimia 64 ya fedha zilizoidhinishwa ambazo zinajumuisha shilingi 35,360,261,424.00 fedha za ndani na shilingi 6,294,310,145.00 ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi kwa kipindi husika zimeoneshwa kwenye Jedwali la pili, la tatu na la nne ambayo yanapatikana katika ukurasa wa 79 hadi 81 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na Kuimarika kwa haki za binadamu na watu za kisiasa na kidemokrasia kwa Serikali kuruhusu mikutano ya kisiasa, kuimarika kwa haki za binadamu katika masuala ya kiuchumi, kufungua fursa za kiuchumi na uwekezaji, kuimarika uhifadhi, ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu kumepelekea Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri wa Sheria wa Haki barani Afrika pia Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa mawaziri wa Sheria na Haki wa jumuiya ya madola wa mwaka 2024 Zanzibar na kuwa mwenyeji wa mkutano wa 77 wa kamisheni ya Afrika haki za Binadamu na Watu utakaofanyika Octoba mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria kupitia uzinduzi wa *Mama Samia Legal Aid Campaign*, ujenzi wa Mahakama za Wilaya 28, kusaidia kusogezwa kwa huduma za

mahakama karibu na wananchi na kuongeza usajili wa matukio muhimu ya kibinadamu ikiwemo vizazi na vifo kutoka asilimia 21 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 27 mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara na taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za sheria na utoaji haki kwa umma ili kuendana na mipango yake na hivyo kufikisha malengo yaliyopangwa katika kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo Wizara na taasisi zake zimeainisha maeneo mahsusi ya vipaumbele na kuyawekea malengo na shabaha kwa ajili ya utekelezaji. Vipaumbele vya Wizara na taasisi zake vimebainishwa kuanzia ukurasa wa 90 hadi ukurasa wa 93 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara na taasisi inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 12,676,205,000.00 ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5 katika ukurasa wa 93 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 383,619,511,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya hizo 97,815,618,000.00 ni mishahara ya watumishi, shilingi 176,148,324,000.00 matumizi mengineyo, shilingi 44,112,800,000.00 ni 3. miradi ya maendeleo fedha za ndani, shilingi 65,542,769,000.00 ni miradi ya maendeleo fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya randama za mafungu husika

ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia mfumo wa kielektroniki wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Pauline Gekul (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu, Dkt. Khatibu Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mheshimiwa Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwashukuru wakuu na watendaji wakuu wa taasisi za Wizara wakiwemo Mheshimiwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Profesa Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Jaji wa Mahakama Kuu Dkt. Benhajj Shaaban Masoud, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Dkt. Evaristo Longopa, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Angela Kemanzi Anatory, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Bwana Griffin Venance Mwakapeje, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Bwana Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria; Mheshimiwa Jaji Dkt. Gerlad Mbonimpa Ndika, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Mahakama Lushoto; Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Dkt. Amina Msengwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, *RITA* kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao katika Tume, Mabaraza na Bodi zao na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Wizara. Sambamba nao, nawashukuru wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake. Aidha, naishukuru familia yangu ikiwa ni pamoja na mke wangu Bibi Flora Ndumbaro na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho lakini si mwisho kwa umuhimu, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Songea Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika shughuli za kuleta maendeleo ya jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***Salamu za Pongezi na Shukrani***

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria, ambapo tumeshuhudia kuimarika kwa mfumo wa utoaji haki na ulinzi wa haki za Binadamu na Watu hususan kuimarika huduma za afya, elimu, maji, nishati na huduma za kisheria. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na

Wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

***4. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu.

***5. Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba ambayo imefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka 2022/23 na kutoa mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote waliotangulia kwa mawasilisho mazuri ya hotuba za Wizara wanazozisimamia.

***6. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge lako kwa umahiri na Weledi mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika katika kukusaidia kuliongoza Bunge lako. Vilevile, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran Mbunge wa jimbo la Babati Vijijini na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa jimbo la Mufindi Kusini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Ni matarajio yangu kwamba watatekeleza Majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na naahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao.

***7. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mabadiliko ya Wenyeviti na Wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge uliyoyafanya hivi karibuni na kuwateua tena Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala Katiba na Sheria na Mheshimiwa Sillo Daniel Baran Mbunge wa Babati Vijijini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, hivyo nitumie fursa hii kuwapongeza sana wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena kuendelea kuziongoza Kamati hizo. Niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote mbili kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

***8. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuendelea kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

## B. DIRA NA DHIMA

***9. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni *Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa*. Aidha, Dhima ya Wizara ni *kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa*.

## C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

***10. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA). Taasisi nyingine ni Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Aidha, Wizara inaratibu shughuli zinazotekelezwa na Bodi ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria na Baraza la Elimu ya Sheria Katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali vya maamuzi, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa

Mawaziri, kupitia Tangazo la Serikali Na. 534/2021 majukumu hayo ni: -

(i.) Kushughulikia masuala ya kikatiba;
(ii.) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;
(iii.) Kuratibu masuala ya haki za binadamu na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;
(iv.) Kutunga sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;
(v.) Uandishi wa sheria;
(vi.) Kuendesha mashtaka ya jinai;
(vii.) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi;
(viii.) Usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;
(ix.) Kuratibu usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini;

(x.) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria;
(xi.) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri na maliasilia za nchi;
(xii.) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;
(xiii.) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na
(xiv.) Kuratibu majukumu ya taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

## D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA

## BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

***11. Mheshimiwa Spika**,* utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umezingatia Dira na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambayo ni pamoja na; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (2030); Mpango wa Maendeleo wa Afrika (2063); Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Ahadi za Mheshimiwa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati akifungua Bunge la 11 mwaka 2021; maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/22-2025/26.

***12. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara na Taasisi zake ilibainisha masuala mahsusi ya kipaumbele kuwa msingi wa kutekeleza majukumu yake. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

### I. Kushughulikia Masuala ya Kikatiba

***13. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeendelea kutoa elimu ya katiba na sheria kwa umma kupitia vyombo vya habari vikiwemo redio,

runinga, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara sambamba na kugawa nakala za Katiba kwa wananchi. Aidha, elimu ya katiba imetolewa kupitia maadhimisho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Wiki ya Sheria, Wiki ya Msaada wa Sheria, makongamano, warsha, semina na midahalo.

***14. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha mfumo wa utoaji wa elimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kutoa Elimu ya Katiba kwa Umma (2023/24-2025/26). Mkakati huo unalenga kutoa elimu ya Katiba ya Nchi ili kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa Katiba na kuwajengea uwezo wa kufahamu haki na wajibu wao kwa Taifa na kuwawezesha kushiriki katika mijadala ya katiba.



**Picha Na. 1:** *Utoaji wa Elimu ya Katiba kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari ukiendelea*

## II. Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki

***15. Mheshimiwa Spika,*** Suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Kwa kipindi cha Mwezi Julai 2022 hadi Machi, 2023 kulikuwa na Jumla ya mashauri **252,882** kati ya hayo **58,266** ni mashauri yaliyokuwepo mwanzoni mwa mwezi Julai, 2022 na mashauri **194,616** yalifunguliwa. Kati ya mashauri **252,882,** mashauri **199,122** yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri **53,760** yanaendelea kusikilizwa. Katika mashauri yaliyobaki, mashauri **2,414** ni ya mlundikano, sawa na asilimia **4** ya mashauri hayo yaliyopo Mahakamani.

## III. Kuratibu Masuala ya Haki za Binadamu na Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria

### (a) Masuala ya Haki za Binadamu

***16. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki kwenye Kikao cha 51 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika mwezi Septemba hadi Oktoba, 2022. Katika kikao hicho, Wizara iliwasilisha taarifa ya nchi iliyoeleza namna Serikali inavyohifadhi, kulinda na kukuza haki za binadamu kwenye maeneo yote yaliyoridhiwa na nchi kuhusu haki za binadamu kama vile maeneo ya haki za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

***17. Mheshimiwa Spika,*** katika kikao hicho, Serikali ilipata fursa ya kutoa taarifa sahihi kuhusu hoja za Mtaalam Maalum wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Asilia, kwenye taarifa aliyoitoa kwenye Baraza hilo, kuhusu madai ya wananchi dhidi ya Serikali ya kukiuka haki za binadamu katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Pori Tengefu la Loliondo.

***18. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu nchini ambapo ujumbe wa Kamisheni hiyo ulitembelea Eneo la Pori Tengefu la Loliondo,

Hifadhi ya Ngorongoro na Kijiji cha Msomera ambapo walishuhudia zoezi la kuhama kwa hiari kwa wananchi wa maeneo hayo. Lengo la ziara hiyo, ni kuishirikisha Kamisheni ya hiyo katika shughuli za masuala ya haki za binadamu na hivyo kutekeleza wajibu wa Serikali wa kushirikiana na mifumo ya vyombo vya haki za binadamu ambavyo Serikali ni mwanachama. Kamisheni hiyo ilipata fursa ya kufanya majadiliano na wenyeji wa maeneo husika.

***19. Mheshimiwa Spika,*** Kamisheni hiyo ilipata fursa ya kufanya majadiliano na viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo: Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; Mawaziri wa Wizara za; Katiba na Sheria; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Maliasili na Utalii; Mambo ya Ndani ya Nchi; na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mkuu wa Mkoa wa Arusha; Mkuu wa Mkoa wa Tanga; Wabunge; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Chama cha Wanasheria wa Tanganyika; Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania; Asasi za Kiraia; Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Kutunza Mazingira. Katika kikao hicho ujumbe wa Kamisheni ulionesha kuridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia haki za binadamu.

***20. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki katika Kikao cha 73 cha Kawaida cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika Banjul Gambia tarehe 20 Oktoba, 2022 ikiwa ni pamoja na kusheherekea miaka 35 ya kuanzishwa kwa

Kamisheni hiyo. Katika kikao hicho, Wizara ilitoa taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuhifadhi, kulinda na kukuza haki za binadamu na watu na jinsi inavyotambua kazi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, Wizara ilieleza namna Serikali ya Awamu ya Sita inavyohifadhi, kulinda na kukuza haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, haki ya elimu ikiwemo elimu ya msingi, sekondari na elimu ya

juu, haki ya kuwa na afya bora. Serikali iliweza kutoa taarifa ya namna ilivyoshughulikia utatuzi wa migogoro mbalimbali kwa kushirikisha sekta zinazohusika kwenye changamoto hizo kwa kuwa na majadiliano na ushirikishwaji wa wananchi kwenye maeneo husika.

***21. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Serikali kwenye Kikao cha 52 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, Geneva Uswisi mwezi Februari 2023. Katika kikao hicho, taarifa ya nchi iliwasilishwa iliyoeleza namna Serikali inavyohifadhi, kulinda na kukuza haki za binadamu kwa kuzingatia misingi ya usawa bila kubagua. Aidha, Serikali ilitoa taarifa kwamba inaendelea kujenga mfumo wa utawala ambao umejikita kwenye nguzo nne ambazo ni, upatanishi, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya. Serikali iliwasilisha maelezo kuhusu jinsi inavyokuza na kulinda haki ya maendeleo, haki za Watoto, watu wenye ualbino na watu wenye ulemavu.




**Picha Na. 2:** *Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas D. Ndumbaro akiwasilisha taarifa ya nchi kuhusu jitihada ambazo Serikali inachukua katika kuhifadhi, kulinda na kukuza haki za binadamu katika kikao cha 52 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa*

***22. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliratibu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kitaifa yaliyofanyika Mkoani Dodoma. Katika maadhimisho hayo, Wizara ilitoa elimu na huduma kwa umma kuhusiana na masuala ya katiba, haki za binadamu, ndoa, mirathi, msaada wa kisheria, haki, na wajibu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara ilitoa elimu kuhusiana na tofauti ya haki za binadamu na haki za watu hususan kwa wananchi waliohudhuria.

***23. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki kwenye hafla ya ufunguzi wa shughuli za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu tarehe 20 Februari, 2023 jijini Arusha. Lengo la ushiriki huo, ni kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na vyombo vya Umoja wa Afrika ambapo Tanzania ni nchi mwanachama.

***24. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, Kanda ya Afrika Mashariki iliyoko Addis Ababa, Ethiopia ilitoa mafunzo kwa maafisa viungo **47** wa masuala ya Haki za binadamu kutoka Wizara na Idara za Serikali. Madhumuni ya mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Arusha, yalilenga kuwajengea uwezo maafisa viungo hao kuhusu utekelezaji wa majukumu yao hususan katika kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu ambayo ni pamoja na: jitihada za kukuza na kulinda haki za binadamu na kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu iliyoridhiwa na nchi.

***25. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora nchini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Hadi kufikia tarehe 1 Julai,

2022, THBUB ilikuwa na jumla ya malalamiko **1,524**. Kati ya hayo, malalamiko **725** yalihusu haki za binadamu na malalamiko **799** yalihusu utawala bora. Kati ya mwezi Julai 2022 hadi Machi, 2023, THBUB ilipokea malalamiko mapya **123.** Kati ya hayo, **39** yalihusu haki za binadamu na **84** yalihusu utawala bora. Aidha, katika kipindi hicho malalamiko yaliyofungwa yalikuwa **719,** yote ya miaka ya nyuma (Backlogs). Kati ya hayo, malalamiko **318** yalikuwa ya haki za binadamu na **401** ya utawala bora. Hivyo kufanya idadi ya malalamiko yanayoendelea na uchunguzi katika hatua mbalimbali kuwa **928** kati ya hayo, malalamiko **446** yalikuwa ya haki za binadamu na **482** ya utawala bora.

***26. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi husika, Serikali kupitia THBUB ilifanya uchunguzi wa zoezi la kuweka alama za mipaka katika Hifadhi ya Pololeti lililokuwa Pori Tengefu la Loliondo, katika uchunguzi huo Tume ilitembelea Hifadhi ya Pololeti na kukutana na baadhi ya mamlaka za Serikali, wananchi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo, wawekezaji, Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa ajili ya kupata maelezo ya namna zoezi zima la uwekaji alama lilivyofanyika. Aidha, ujumbe wa Tume ulikutana na Waandishi wa Habari Jijini Arusha kwa lengo la kusikiliza malalamiko yao kuhusiana na masuala ya Ngorongoro (NCA) na Hifadhi ya Pololeti. Lengo la uchunguzi huo ni kubaini iwapo kulikuwa na uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora katika zoezi hilo la uwekaji alama za mipaka katika Hifadhi ya Pololeti ili hatimaye kuweza kutoa mapendekezo kwenye mamlaka husika. Taarifa ya uchunguzi huo inaendelea kuandaliwa na ikikamilika itawasilishwa kwenye mamlaka husika.

***27. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia THBUB, ilifanya uchunguzi uliohusu mchakato mzima wa uhamishaji wa wananchi kutoka Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kuhamia kwenye Kijiji cha Msomera, Wilayani Handeni Mkoani Tanga.

Katika uchunguzi huo, Tume ilitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Kijiji cha Msomera mkoani Tanga, na kupata maelezo ya wananchi. Aidha, Tume ilikutana na mamlaka mbalimbali za Serikali na baadhi ya Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa ajili ya kupata maelezo zaidi. Lengo la uchunguzi huo ni kubaini iwapo kulikuwa na uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora katika zoezi hilo la wananchi kuhamia Kijijini Msomera kutokea Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ili hatimaye kuweza kutoa mapendekezo kwenye mamlaka husika. Taarifa ya uchunguzi huo inaendelea kuandaliwa na ikikamilika itawasilishwa kwenye mamlaka husika.

***28. Mheshimiwa Spika,*** Tume ilitoa mafunzo ya haki za binadamu na uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora kwa Masheha **144** wa Shehia za Wilaya ya Mjini iliyopo Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Kati iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja na Wilaya ya Kaskazini A iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa Masheha **130** kwa Shehia za Wilaya ya Wete na Micheweni zilizopo Mkoa wa Kaskazini na Wilaya ya Chakechake na Mkoani zilizopo Kusini Pemba. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza uwezo kwa Masheha kuhusu masuala ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora, ili kuimarisha utamaduni wa kuheshimu, kutetea, kukuza na kulinda haki za binadamu na misingi ya Utawala bora.

***29. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika ukaguzi maalum wa magereza mawili **(2)** ya Isanga na Msalato ya jijini Dodoma ulifanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Idara ya Ustawi wa Jamii. Lengo la ukaguzi huo ni kutoa elimu, kutathmini hali ya haki za wafungwa na mahabusi wanaozuiliwa katika magereza hayo, na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ziara za nyuma. Baada ya ukaguzi wa magereza. Taarifa ya ukaguzi

huo iliandaliwa na kuiwasilisha katika Mamlaka husika kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika Tume ilitembelea Vituo vya Kulelea Watoto na Wazee katika Mikoa ya Mwanza (Kituo cha kulelea watoto cha Suzan – Kisesa na Hasani-Busweru), Dar es Salaam (Kituo cha Wazee Nungwe, Vituo vya kulelea watoto Upanga na Kurasini) na Lindi (Kituo cha kulelea watoto cha Al-Hudaa Islamic Day Care). Tume ilifanya ukaguzi huu ili kuangalia uzingatiwaji wa haki za binadamu katika maeneo wanapohifadhiwa Watoto na Wazee. Aidha, Tume iliandaa taarifa na mapendekezo na kuyawasilisha kwenye Mamlaka husika.

***31. Mheshimiwa Spika,*** THBUB ilifanya Maadhimisho ya Miaka Ishirini Tangu kuanzishwa kwake, ambapo jumla ya wadau thelathini na sita (36) wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka Wizara, Idara, Mamlaka na Wakala za Serikali pamoja na AZAKi walitoa huduma mbalimbali kwa wananchi kuanzia tarehe 10/09/2022 hadi tarehe 14/09/2022 katika Viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma. Katika wiki hiyo ya Maadhimisho, jumla ya wananchi 3,257 walishiriki ambapo wanaume walikuwa 1,542 na wananwake walikuwa 1,715 ambapo walipatiwa huduma mbalimbali kwenye maonesho hayo ikiwa ni pamoja na; Msaada wa Kisheria; Usajili wa vyeti vya kuzaliwa; Upimaji wa awali wa magonjwa; udahili wa kozi za elimu ya juu kwa Mwaka 2022/23 Chuo cha Mipango; na elimu na ushauri kuhusu masuala mbalimbali kama vile, maadili ya Viongozi wa Umma, haki za binadamu na utawala bora, kujikinga na majanga ya moto, ufunguaji wa mashauri Mahakamani, VVU na UKIMWI, ndoa na mirathi na kadhalika. Aidha siku ya kilele cha maadhimisho takribani washiriki 3,500 walihudhuria. Kupitia maadhimisho hayo, Serikali kupitia Tume iliweza kuuelezea umma baadhi ya kazi zilizotekelezwa na Tume katika kulinda, kutetea na kuhifadhi

haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini tangu kuanzishwa kwake.

***32. Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kutekeleza misingi ya utawala bora na utawala wa sheria imekuwa ikiwahudumia wananchi bila upendeleo, udini, ukabila, jinsia na bila kujali vyama vyao vya siasa na misimamo mingine. Hivyo, hali ya siasa na demokrasia nchini imekuwa ikiimarika kutokana na utayari wa Serikali kukutana na kufanya majadiliano na vyama vyote vya siasa na wadau wa demokrasia.

***33. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinaenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Katika kukuza na kulinda haki za kiraia Serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki ili wananchi waendelee kunufaika na uhuru wa maoni na haki ya kupata na kutoa taarifa.

**(b) Masuala ya Msaada wa Kisheria**

***34. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kwa kushirikiana na Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria, AZAKI na Serikali za Mitaa, iliendesha kampeni za utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria Mkoani Arusha katika Halmashauri za Meru na Arumeru kwenye Kata za Ilking'a na Ngarenanyuki, mtawalia. Aidha, kampeni kama hiyo ilifanyika pia mikoa ya Ruvuma na Njombe, katika Halmashauri za Wilaya ya Songea, Njombe na Makete. Katika kampeni hizo, jumla ya wananchi **4,150** (wanaume **1,617**, wanawake **2,416** na watoto **117**) walipata huduma ya msaada wa kisheria pamoja na elimu kuhusu sheria ya ndoa, mirathi, madai, watoto, ardhi, jinai, rushwa, na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Jumla ya mashauri **366**

yalisajiliwa na kushughulikiwa ambapo mashauri **60** yalihitimishwa.



Picha Na. 3: *Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria wakiendelea kutoa Huduma katika Kampeni ya Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria Mkoani Arusha*

***35. Mheshimiwa Spika,*** kampeni hizo zilihusisha utayarishaji na usambazaji wa vipeperushi **2,360** vyenye ujumbe kuhusu masuala ya ndoa, haki za watoto, ardhi na mirathi.

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuimarisha huduma ya msaada wa kisheria, ilitoa mafunzo ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA kwa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kutoka Mikoa 10 ya Tanzania Bara. Madhumuni ya Mafunzo hayo yalikuwa ni kuwajengea uwezo wa kuzifikia huduma za Kisheria zinazotolewa kwa njia ya TEHAMA ambazo ni: -

(i) Usajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria;
(ii) Usajili wa wasaidizi wa kisheria;
(iii) Usajili wa watoa huduma za majadiliano, maridhiano, usuluhishi, na upatanishi;

(iv) Uwasilishaji wa malalamiko;
(v) Maombi ya kupatiwa huduma za msaada wa kisheria; na
(vi) Maombi ya kuongezewa muda wa kufungua mashauri mahakamani nje ya muda.

***37. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya washiriki **65** kutoka makundi ya Watoa Huduma za Kisheria, watumishi wa Wizara, Mawakili wa Serikali, Wasajili Wasaidizi, Maafisa Magereza kutoka Mikoa 10 ya Tanzania Bara walijengewa uwezo wa utumiaji wa mifumo hiyo inayoratibiwa na Wizara.

***38. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutoa elimu hii ili kuwawezesha wananchi kuifahamu na kuitumia mifumo hiyo kupata huduma zinazotolewa na Wizara kwa haraka, na kwa gharama nafuu.

***39. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupokea maoni kuhusu uimarishwaji wa huduma ya msaada wa kisheria, ikiwa ni pamoja na maoni ya Bodi ya Taifa ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria, kuhusu uboreshwaji wa sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 na Kanuni zake, kufutwa kwa ada ya usajili kwa Wasaidizi wa Kisheria, na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kutumia wanafunzi wake kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika maeneo wanayotoka. Wizara imeyafanyia kazi baadhi ya mapendekezo hayo ambapo imewezesha, ada ya usajili kwa Wasaidizi wa Kisheria kufutwa na inaendelea kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo mengine yaliyopo.

***40. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilizindua kampeni ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria (***Mama Samia Legal Aid Compaign***) ambayo inalengo la kuhakikisha wananchi wanapatiwa elimu ya huduma ya msaada wa kisheria, elimu ya Mirathi, Wosia na huduma ya msaada wa kisheria. Kampeni hii itafanyika kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia

2023/24-25/26 na inahusisha Tanzania Bara na Zanzibar katika mikoa na wilaya zote.




**Picha Na. 4:** *Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damasi D. Ndumbaro (Mb.), akizindua* ***Mama Samia Legal Aid Campaign***

***41. Mheshimiwa Spika,*** katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara iliendesha mafunzo ya Utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala katika mikoa ya Arusha na Mwanza. Kwa upande wa mkoa wa Arusha, jumla ya washiriki **30** walihudhuria mafunzo kati ya hao, washiriki wanawake walikuwa **sita (6)** na wanaume **24** kutoka katika makundi ya Wasaidizi wa Kisheria, Viongozi wa Dini na Viongozi wa Kimila kutoka jamii ya Wamasai katika Wilaya ya Longido. Kwa upande wa Mkoa wa Mwanza, Mafunzo haya yalitolewa kwa washiriki **25** kati ya hao, wanaume **20** na wanawake watano (**5)** kutoka katika makundi ya viongozi wa kimila na wenyeviti wa mitaa na vijiji katika wilaya za Sengerema, Ilemela, Nyamagana na Magu, ambao wanahusika zaidi na masuala ya upatanishi na utatuzi wa migogoro katika jamii zao. Lengo

la mafunzo ni kuongeza ufahamu wa sheria mbalimbali na masuala ya haki za binadamu.

**IV. Kutunga Sera Zinazohusu Masuala ya Kisheria na Kusimamia Utekelezaji wake**

***42. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea na jukumu la kutunga sera na sheria mbalimbali za masuala ya kikatiba na kisheria ikiwa ni mikakati ya kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Sheria. Sera na sheria hizi zitatoa mchango kwa maendeleo ya Taifa na hivyo kufanikisha malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

***43. Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kwa kushirikiana na wadau wa haki jinai, imeandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Mashtaka. Lengo la kuwa na sera hii ni kuweka misingi ya kusimamia mifumo na taratibu za uendeshaji wa mashtaka nchini. Wizara inaendelea kupokea maoni ili kukamilisha Sera husika.

***44. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha mfumo wa sheria nchini, Wizara inaendelea na uratibu wa kutunga Sheria ya Elimu ya Sheria na Sheria ya Ufilisi ili kuimarisha mfumo wa elimu ya sheria na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini mtawalia. Maandalizi hayo yameshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara, taasisi za sheria za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, vyuo vinavyotoa elimu ya sheria nchini, vyama vya wenye viwanda, vyama vya wafanyakazi na viongozi wa kampuni mbalimbali.

***45. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi za kupambana na uhalifu mkubwa wa kupangwa kwa kuzindua vikosi kazi viwili (2) kimoja kwa kila upande wa Muungano. Kwa upande wa

Tanzania Bara, kikosi kazi kinashughulikia uhalifu mkubwa wa kupangwa wa usafirishaji haramu wa binadamu na ukatili na udhalilishaji wa watoto kingono. Kwa upande wa Zanzibar kikosi kazi kinashughulikia makosa ya kupambana na uhalifu mkubwa wa kupangwa unaovuka mpaka.

***46. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa elimu ya Sheria nchini ikiwemo kutatua changamoto zilizopo za mfumo huo ambazo zimebainishwa na Kamati maalum ya kutathmini, mfumo wa elimu ya sheria nchini. Kamati hiyo iliyoundwa na Waziri wa Katiba na Sheria ilibaini changamoto mbalimbali za mfumo huo ambazo ni pamoja na kutokuwepo kwa mtaala wa taifa wa elimu ya sheria; kukosekana kwa Sheria inayosimamia utoaji wa elimu ya sheria nchini; na kupishana kwa vigezo vya udahili wa wanafunzi wanaosoma shahada ya kwanza ya Sheria.

***47. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha Mfumo wa Elimu ya Sheria nchini Kamati ilitoa mapendekezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha Baraza la Elimu ya Sheria, kwa kufanya mapitio ya muundo wake ili kuliwezesha kuwa na mamlaka ya kisheria ya kuweza kudhibiti na kusimamia ipasavyo utoaji wa elimu ya Sheria hapa nchini; na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa Elimu ya Sheria kwa kutunga sheria itakayosimamia mfumo huo. Kwa ujumla mapendekezo hayo ya Kamati yanaendelea kufanyiwa kazi na Wizara, Taasisi mbalimbali na wadau wengine wa Elimu ya Sheria hapa nchini.

***48. Mheshimiwa Spika,*** Wizara tayari imeanza utaratibu wa kuandaa Sheria ya Elimu ya Sheria kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**V. Uandishi wa Sheria**

***49. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi Sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi iliandaa Miswada **11**. Miswada iliyoandaliwa ni kama ilivyooneshwa kwenye ***Kiambatisho A***. Aidha, Miswada ya Sheria **saba (7)** ilijadiliwa na kupitishwa kuwa Sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hizo ni kama zilivyooneshwa kwenye ***Kiambatisho B***. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kuandika sheria kwa lugha ya Kiswahili. Katika kipindi hiki, Sheria Kuu tatu **(3)**; Sheria ya Maafa, Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Sheria ya Uwekezaji ziliandaliwa katika lugha ya Kiswahili huku Sheria Ndogo **405 *(Kiambatisho C)*** ziliandikwa kwa Kiswahili. Katika kipindi husika jumla ya Maazimio matatu **(3)** yalipitishwa na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama yalivyoainishwa kwenye ***Kiambatisho D***.

***50. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilihakiki na kuchapisha jumla ya Sheria Ndogo **631**, ikilinganishwa na Sheria Ndogo **542** zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia **16**. Sheria hizo zinajumuisha Kanuni **190**, Matangazo **141**, Amri **299**, na Tamko **moja (1)** la Serikali. Lengo la kutengenezwa kwa sheria ndogo ni kufafanua kwa kina na kwa undani maudhui yaliyobainishwa kwenye Sheria Kuu.

***51.*** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya Sheria nane **(8)** zilitafsiriwa kutoka lugha

ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho E.**

***52. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi husika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha uhakiki wa Sheria Kuu **445,** kama zilivyoorodheshwa katika ***Kiambatisho F.***

***53. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya Mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa **1,304** kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na Mikataba **1,171** iliyofanyiwa upekuzi katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 sawa ongezeko la asilimia **11**. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya Miradi ya Serikali na miradi inayofadhiliwa na Wadau wa Maendeleo. Aidha, Hati za Makubaliano **295** zilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na idadi ya Hati za Makubaliano **174** zilizofanyiwa upekuzi katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022. Ongezeko hili linaakisi jitihada za Serikali kuhamasisha uwekezaji na diplomasia ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Vilevile, kati ya Mikataba **1,304** iliyofanyiwa upekuzi, Mikataba **567** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali katika mchanganuo ufuatao: Mikataba **453** ilikuwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania trilioni **16.7**; Mikataba **83** ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani **31,913,579,603** sawa na Shilingi za Kitanzania trilioni **74.2**; na Mikataba **29** ilikuwa na thamani ya Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) **94,105,503** sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni **239.5**; na Mkataba Miwili **(2)** ulikuwa na thamani ya Paundi ya Kiingereza **59,213,185** sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni **172.5**.

***54. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali Kuu, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na kwa wananchi. Lengo ni kuhakikisha Serikali na Taasisi zake zinapata faida kutokana na utekelezaji wa majukumu yake na hivyo, kuikinga Serikali kuingia katika kesi mbalimbali kwa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya maombi ya ushauri wa kisheria **812** yalipokelewa na kufanyiwa kazi ikilinganishwa na maombi **1,129** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya maombi **812,** maombi **149** yalihusu malalamiko ya watu binafsi na maombi **663** yanatoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kuongezeka kwa maombi ya watu binafsi kunatokana na mwamko wa wananchi wanaoupata kupitia elimu inayotolewa na Wizara.

**VI. Kuendesha Mashtaka ya Jinai**

***55. Mheshimiwa Spika,* Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai **33,004** ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ikilinganishwa na kesi **44,364,** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Katika kipindi husika, kesi **20,952** zilihitimishwa sawa na asilimia **63** ikilinganishwa na kesi **13,339** sawa na asilimia **30** ya kesi zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya kesi zilizohitimishwa, **11,819** sawa na asilimia **56.4** zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani ikilinganishwa na kesi **8,103** sawa na asilimia **48** zilizohitimishwa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Aidha, kesi **12,052** sawa na asilimia **37** ya kesi zilizoendeshwa, zinaendelea mahakamani

katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na kesi **31,025** sawa na asilimia **70** ya kesi zilizoendeshwa, zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya kesi **783** ziliendeshwa katika Mahakama za watoto ambapo kesi **537** zilihitimishwa na kesi **246** zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi hicho, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya **kesi 6,116** katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya kesi hizo, **kesi 2,699** ni za vikao maalum vya Mahakama Kuu ikilinganishwa na **kesi 4,046** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Aidha, katika kipindi hicho, **kesi 1,521** zilihitimishwa ikilinganishwa na **kesi 917** zilizohitimishwa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 na **kesi 1,178** zinaendelea katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na **kesi 3,129** zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Vilevile, **kesi 3,166** zilihusu Rufaa za Mahakama Kuu ikilinganishwa na **rufaa 4,460** zilizokuwepo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Aidha, **kesi 1,541** zilihitimishwa ikilinganishwa na **kesi 1,460** zilizohitimishwa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 na **kesi 1,625** zinaendelea katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na **kesi 3,000** zilizokuwa zinaendelea katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai za **rufaa na maombi 1,599** katika Mahakama ya Rufani ikilinganishwa na **kesi 2,863** zilizoendeshwa Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya hizo, **rufaa 320** zilihitimishwa ikilinganishwa na **rufaa 362** zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, na **rufaa 1,279** zinaendelea katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na **rufaa 2,501** zilizokuwa zinaendelea katika hatua mbalimbali kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

***57.*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilivuka na kesi 154 na kufungua kesi 97 na kufanya jumla ya kesi kuwa 251 katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi 88 zilizofunguliwa za rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Aidha, kesi 57 zilihitimishwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Vilevile, kesi 194 zinaendelea katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na kesi 77 zilizokuwa zinaendelea katika hatua mbalimbali kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

***58. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi za jinai walipewa adhabu zikiwemo vifungo, faini na mali mbalimbali kutaifishwa. Kiasi cha **Shilingi 2,103,868,730** kililipwa mahakamani kama faini katika kesi **5,440** ikilinganishwa na **Shilingi 1,864,820,883.00** zilizolipwa kwenye kesi **4,495** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023. Katika kipindi hicho, mali zilizotaifishwa ni pamoja na magari ya aina tofauti **25**, nyumba **nne (4),** madini (dhahabu gramu **3,290.39**, tanzanite gramu **6,221.24**) na fedha taslim **Shilingi 1,494,472,436.75** na Dola za Marekani **9,292.34.**

***59.*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifanya ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi. Lengo la ukaguzi huu ni kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki kutatua changamoto zilizojitokeza. Katika kipindi husika, jumla ya magereza **63** na vituo vya Polisi **140** vilikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo, pamoja na mambo mengine, ulifanikisha kuachiwa kwa jumla ya Mahabusi **333** ikilinganishwa na mahabusi **809** walioachiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka uliopita wa 2021/2022, kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushahidi hafifu. Kufuatia zoezi hili kulisaidia kupunguza mlundikano wa maabusi katika magereza na vituo vya polisi. Taarifa ya magereza na

vituo vya polisi vilivyokaguliwa katika kipindi hicho ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho G.**




Picha Na. 5: *Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester A. Mwakitalu akiwa pamoja na Watumishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika ziara ya ukaguzi wa magereza Mkoa wa Tabora*

**VII. Kushughulikia Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi**

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri ya madai **6,320** kati ya mashauri hayo, mashauri **6,314** ni ya kitaifa na mashauri **sita (6)** ni ya kimataifa. Serikali ilikamilisha jumla ya mashauri **575** ambapo mashauri **570** ni ya kitaifa na mashauri **matano (5)** ni ya kimataifa na kuokoa jumla ya Shilingi **305,405,680,693.**

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi **157** ikilinganishwa na mashauri ya usuluhishi **111** yaliyoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya mashauri **157** yaliyoendeshwa, jumla ya mashauri **126** ni ya kitaifa na mashauri **31** ni ya kimataifa. Kati ya Mashauri yaliyoendeshwa mashauri **16** yamehitimishwa ambapo matano

**(5)** ni ya kimataifa na **11** ni ya kitaifa. Serikali iliweza kuokoa Dola za Marekani (USD) **3,082,855,894.74 (**ambazo ni sawa na Shilingi Trilioni 7.24**)** na Shilingi za Kitanzania **15,078,111,197.90** hivyo kufanya jumla ya kiasi kilichookolewa kwa mashauri ya usuluhishi kufikia **Shilingi Trilioni 7.26.** Fedha zote zilizookolewa kutokana na mashauri ya madai na usuluhishi kwa mwaka 2022/2023 ni **Shilingi Trilion 7.57** ambazo Serikali ingetakiwa kulipa endapo ingeshindwa katika mashauri husika.

***63. Mheshimiwa Spika:*** Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inawakilisha vyema Serikali kwa kuongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (GNT) ambazo zinaundwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kufanikisha kumaliza mashauri/migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi, na maridhiano nje ya Mahakama. Utaratibu huu umeweza kuvutia wawekezaji nchini kwa kumaliza mapema migogoro mbalimbali dhidi ya Wawekezaji na Wafanyabiashara kwa njia ya Majadiliano. Jambo hili limewezesha kuokoa fedha za Serikali ambazo zingetumika katika kuendesha migogoro tajwa zinazojumuisha gharama za usafiri, posho kwa Mawakili wa Serikali na mashahidi na ada za mahakama, kudumisha uhusiano kati ya Serikali na Wawekezaji, kujenga imani kwa wawekezaji kuhusu hali ya utoaji haki nchini, pamoja na kukuza diplomasia ya Uchumi.

## VIII. Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara, Sheria za Kimataifa na Mikataba

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilifanya mapitio ya sheria ya usuluhishi na kuandaa mapendekezo ya uboreshwaji wa sheria hiyo kwa kukusanya maoni ya wadau kuhusu mapendekezo ya maboresho na kuandaa rasimu ya marekebisho ya sheria hiyo kwa madhumuni ya kuimarisha mfumo wa usuluhishi wa migogoro ya kibiashara nchini.

***65. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na kazi hiyo, Wizara iliendesha zoezi la kutafsiri kanuni za Upatanishi na Maridhiano ambazo zinalenga kufanikisha utekelezaji wa sheria ya usuluhishi wa migogoro nje ya mfumo wa Mahakama. Hadi kufikia Machi, 2023 Wizara imesajili jumla ya Watatuzi wa Migogoro **530** watakaotumika katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Kati ya wataalam hawa Wasuluhishi ni **266**, Wapatanishi ni **172**, Waendesha Maridhiano ni **35** na waendesha majadiliano ni **57**. Vilevile, Wizara imeandaa miongozo ya mafunzo ya Usuluhishi, Upatanishi, Uendeshaji Maridhiano na Majadiliano itakayotumika kufundishia Wasuluhishi, Wapatanishi, Waendesha Maridhiano na Majadiliano pamoja na mwongozo wa kuendesha vikao vya Jopo la Ithibati la Waendesha Usuluhishi, Upatanishi, Majadiliano na Maridhiano.

***66. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utekelezaji wa Sheria za kimataifa, Wizara imeshiriki katika mikutano ya kimataifa ya masuala ya kisheria ikiwemo ya Umoja wa Afrika ambapo Tanzania imechaguliwa kuwa Makamu wa kwanza wa mwenyekiti kwa Mawaziri wa masuala ya Sheria wa Afrika. Aidha kwa kuwa ilikuwa ni zamu ya ukanda wa Kaskazini kutoa mwenyekiti, Tanzania kama Makamu Mwenyekiti imeongoza mikutano miwili ya Mawaziri wa Sheria wa Afrika iliyofanyika Addis Ababa na Accra mwaka 2022. Nafasi ya uenyekiti wa masuala ya Sheria wa Afrika inaipa Tanzania fursa ya kufikisha agenda zake kwa maslahi ya nchi. Sambamba hilo, Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola mwaka 2024.

***67. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imesimamia na kushiriki katika majadiliano ya migogoro 31 yanayohusu masuala ya ajira, kazi, manunuzi, uwekezaji wa Ardhi na miradi ya rasilimali za mafuta na gesi ikilinganishwa na

majadiliano ya migogoro **nane (8)** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Ongezeko hilo linatokana na kuwepo na maboresho ya Sheria mbalimbali katika Sekta ya Madini ambapo Serikali inaendelea na jitihada za kutatua migogoro hiyo kwa njia ya Usuluhishi na migogoro **saba (7)** imehitimishwa.

## IX. Kuratibu Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Usimamizi wa Ufilisi na Udhamini

***68. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imeendelea kuimarisha shughuli za Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Ufilisi na Udhamini kwa ajili ya mipango na maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wakala imesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **767,164** pamoja na vyeti vya vifo **26,605**. Aidha imefanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa vya wanafunzi **84,133** na vyeti vya vifo **17,197** vya wazazi wa wanafunzi wanaoomba mkopo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

***69. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Wakala ilishiriki katika mkutano wa wataalam wa masuala ya usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu Barani Afrika, uliofanyika nchini Eithiopia na kutoa taarifa ya mafanikio yaliyopatikana Tanzania katika kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto Chini ya Umri wa Miaka Mitano unaotekelezwa katika mikoa **23** ya Tanzania Bara. Mpango huo umewezesha kuongeza kiwango cha usajili katika kundi hili kwa takribani asilimia **65** katika kipindi hiki.



**Picha Na. 8:** *Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb.), akimkabidhi mwananchi cheti cha kuzaliwa*

***70. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kampeni ya Kitaifa ya kulinda maadili, haki na ukatili dhidi ya watoto, jumla ya hati **17** za watoto wa kuasili zilisajiliwa na kutolewa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 baada ya kupokea amri ya Mahakama.

***71. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini inaendelea na usajili wa matukio ya ndoa na talaka ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, umepokea jumla ya marejesho **31,379** ya ndoa zilizofungwa na nakala za hukumu za talaka **410** na kusajiliwa

***72. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala imeendelea na jukumu ya usimamizi na usajili wa bodi za wadhamini ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya bodi za wadhamini **68** zilisajiliwa. Katika kuboresha utendaji wa bodi hizo, Wakala iliandaa Katiba Mfano ambayo inatakiwa

kufuatwa na bodi zote za wadhamini zilizosajiliwa RITA na zinazotarajiwa kusajiliwa RITA.

***73. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala iliendelea na jukumu la kuhamasisha wananchi kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya kugombea mali inayojitokeza katika jamii baada ya mzazi mmoja kufariki. Hivyo, kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya wosia **97** zilitayarishwa na kuhifadhiwa. Aidha, Wakala ilifanya utafiti kuhusu uwepo wa mwamko mdogo wa kuandika Wosia katika Jamii, lengo likiwa ni kubainisha sababu zinazofanya Wananchi wengi kutoandika na kuhifadhi wosia. Utafiti huo, ulifanyika kwa kuchagizwa na kaulimbiu ya "*Familia kwanza andika Wosia sasa*". Taarifa ya matokeo ya utafiti huo, inatarajiwa kutolewa hivi karibuni na inatarajiwa kutumika katika mipango na mikakati ya kuimarisha huduma za menejimenti ya uandishi na utunzaji wa Wosia kwa umma wa watanzania.

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha elimu na uhamasishaji wa uandishi na uhifadhi wa Wosia unafanyika kwa mujibu wa Sheria, Wizara kupitia Wakala imeweka Kambi katika Viwanja vya Bunge kwa kuweka Hema ambapo wataalam wa masuala ya Wosia wanaendelea kuwahudumia waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kuanzia tarehe 24 April 2023 hadi 5 Mei,2023.

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Wakala iliweza kuhudhuria mashauri **49** yaliyopo katika mahakama mbalimbali pamoja na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yanayohusu masuala ya mirathi na Bodi za Wadhamini zinazosimamiwa na Wakala. Jumla ya mashauri **41** yamemalizika hivyo kuruhusu kuendelea na taratibu za usimamizi, uhakiki na ufungwaji wa mirathi. Aidha, Wakala inasimamia jumla ya mirathi 130 ambapo kati ya hiyo, kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023 imepokea mirathi mipya

**nane (8).** Vilevile, Wakala imefanikiwa kufunga mirathi **mbili (2)** baada ya kugawa mali kwa wanufaika.

**X. Kuratibu Tathmini na Maboresho ya Sheria**

***76. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya Mapitio ya Mfumo wa Sheria na Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria zinaakisi mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia. Tume imefanya utafiti wa mfumo wa sheria unaosimamia masuala ya udhamini kwa lengo la kubaini changamoto na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo huo. Utafiti umefanyika katika Mikoa **minne (4)** ya Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga na Mwanza ili kupata maoni ya wadau.

***77. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya mapitio ya mfumo wa Sheria unaosimamia utoaji haki katika Mahakama za Mwanzo ili kuona endapo kuna haja ya kutumia Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai na Sheria ya Ushahidi katika Mahakama hizo badala ya kutumia kanuni za Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, kanuni za Mwenendo wa Mashauri ya madai na kanuni za Ushahidi. Utafiti umefanyika kwa sampuli ya mikoa sita (06) ya Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Tabora, Iringa na Mbeya

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha masuala ya Uchaguzi na Demokrasia nchini, Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya mapitio ya mfumo wa Sheria Unaosimamia Uchaguzi na Vyama vya Siasa kwa lengo la kubainisha changamoto mbalimbali zinazokabili michakato ya uchaguzi na uendeshaji wa Vyama vya Siasa. Aidha, mapitio hayo yalilenga kubaini endapo mfumo wa sheria uliopo unatoa fursa stahiki kwa wanawake na makundi maalum kushiriki katika masuala ya uongozi na uchaguzi na kubainisha changamoto zinazokabili utaratibu wa

upatikanaji wa wabunge na madiwani wanawake wa viti maalum.

***79. Mheshimiwa Spika,*** utafiti umefanyika kwenye wilaya 39 katika mikoa 17 ambayo ni Dar es Salaam (Temeke, Ilala, Ubungo, Kinondoni na Kigamboni), Kusini Pemba (Chakechake na Mkoani), Kaskazini Pemba (Wete na Micheweni) Kusini Unguja(Kati na Kusini), Mjini Magharibi (Mjini Magharibi 'A' na Mjini Magharibi 'B'), Kasikazini Unguja (Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B'), Mtwara (Mtwara na Nanyumbu), Ruvuma (Songea na Tunduru), Tanga (Tanga na Korogwe), Arusha (Arusha na Karatu), Iringa (Iringa na Mufindi), Mbeya (Mbeya Mjini na Kyela), Tabora (Tabora na Nzega), Kigoma (Kigoma na Kasulu), Mwanza (Ilemela na Ukerewe), Mara (Musoma na Tarime).

Aidha, Taarifa ya Mapitio imekamilika na kuwasilishwa na kuwasilishwa kwangu kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Nakala ya taarifa hiyo imewasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu na katika taasisi nyingine za umma ili kuendelea kuipitia na kuona namna ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa. Baada ya kuipitia na kuichambua taarifa hiyo, nitaiwasilisha Bungeni kwa mujibu wa kifungu cha 15(2) cha sheria tajwa na kutoa taarifa ya namna Serikali itakavyoyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa.

***80. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya Tathmini ya utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Usafiri wa majini kwa lengo la kubaini changamoto za utekelezaji na kutathmini kama malengo yaliyokusudiwa wakati wa kutungwa kwa sheria hizo yamefikiwa. Tathmini hiyo imefanyika kwa kufanya vikao na Wadau wanaosimamia utekelezaji wa Sheria za usafiri wa Majini katika mikoa **minne (4)** ya Dar es Salaam, Tanga, Mwanza na Kigoma.

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kutoa kutoa elimu ya sheria kwa umma kwa lengo la kuwajengea uwezo wananchi katika masuala ya mbalimbali ya kisheria. Katika kutekeleza hilo, Tume imetumia njia mbalimbali zikiwemo kuchapisha na kugawa kalenda na vitabu vya kumbukumbu ambavyo vina taarifa muhimu kuhusu Tume, kurusha vipindi vya redio, runinga, mitandao ya kijamii, kuandaa jarida pamoja na kuendelea kutumia tovuti kukusanya maoni na kuhabarisha umma. Elimu hiyo ililenga kutoa uelewa wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, nafasi ya Tume katika maboresho ya sheria, haki za watoto na Mpango wa Mapitio ya Sheria wa mwaka 2023 hadi 2025.

Vilevile, Tume ilishiriki katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika jijini Dodoma na Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Wilaya ya Kondoa ambapo vipeperushi 370 vilitolewa kwa watu mbalimbali. Aidha, Tume iliandaa Kongamano la Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria za Makosa Dhidi ya Maadili Tanzania lililofanyika jijini Dodoma ambapo wadau 112 walihudhuria na mada nane (8) zilitolewa. Lengo la Kongamano hili ni kuiwezesha Tume kufanya utafiti wa makosa ya mmomonyoko wa maadili na kuangalia namna bora ya kuimarisha vifungu vya sheria vinavyozuia makosa hayo. Aidha, tayari Bunge lako limekwisha iagiza Wizara yangu kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya mambo ya Ndani, na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kufanya utafiti wa kina katika eneo hili ili kuondoa upungufu katika sheria hiyo na kutunga sheria huku tukielewa ukubwa wa tatizo hili ndani ya jamii yetu.

## XI. Kuratibu Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria za Utajiriasili na Maliasilia za Nchi

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara iliendelea na kazi za kuimarisha mfumo wa uangalizi wa masuala ya usimamizi na uendelezwaji wa utajiriasili na maliasilia za nchi, kwa mujibu wa Sheria Sura 449 na 450 zinazohusu umiliki wa nchi wa utajiriasili na maliasilia za nchi.

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Wizara ilikamilisha kazi ya kuandaa taarifa ya Tathmini ya Uzingatiwaji wa Sheria hizo kwa Wizara, Taasisi na mamlaka mbalimbali zilizokasimiwa mamlaka ya usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa utajiriasili na maliasilia za nchi kwa manufaa ya umma. Madhumuni ya tathmini hiyo ni kubainisha kiwango cha uzingatiwaji wa Sheria hizo. Tathmini hii imebaini uwapo wa mafanikio makubwa hususani kuimarishwa kwa masuala ya ulinzi wa utajiriasili na maliasilia za nchi katika mifumo mbalimbali ya kisekta kama vile kujenga ukuta katika eneo la uchimbaji wa madini aina ya Tanzanite Mirerani; kuanzishwa kwa masoko ya madini; kuanzishwa kwa mfumo wa Jeshi Usu katika ulinzi wa wanyamapori na misitu; Pato la Taifa limeongezeka kutokana na uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za nchi; kuongezeka kwa ushiriki wa watanzania katika fursa zinazopatikana kwenye uwekezaji wa utajiri asili na maliasilia za nchi; na kuondolewa masharti hasi katika Mikataba ya uwekezaji katika utajiri na maliasilia za nchi imeendelea kupungua tangu kuanza utekelezaji wa sheria hizi kwenye sekta zilizochukua hatua ya kuzingatia misingi ya Sheria hizo.

***84. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mwongozo wa Usajili wa Mikataba inayohusu, matumizi, uvunaji au uendelezaji wa utajiriasili na maliasilia za nchi. Lengo la mwongozo huo ni kuweka utaratibu jumuishi wa kushughulikia mikataba,

maazimio na itifaki mbalimbali zinazogusa masuala ya utajiriasili na maliasilia za nchi ili kurahisisha ufuatiliaji wa pamoja.

***85. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya maboresho ya mfumo wa ki-elekroniki wa usajili wa mikataba ya utajiriasili na maliasilia za nchi ambao utaziwezesha sekta kuingiza taarifa zinazohusu utajiriasili na maliasili za nchi.

## XII. Kushughulikia Urejeshwaji wa Wahalifu na Masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Makosa ya Jinai

***86. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kusimamia kurejeshwa kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika kipindi hicho, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi **13** yakiwemo **saba (7)** ya kuwarejesha watuhumiwa wa makosa ya jinai waliokimbilia nchini kutoka katika mataifa ya nje na maombi **sita (6)** ya kuwarejesha watuhumiwa wa uhalifu waliokimbilia nchi za nje yameombwa na Tanzania Kwenda nchi za nje ambazo tuna makubaliano ya kubadilishana taarifa za uhalifu.

***87. Mheshimiwa Spika,*** lengo la kurejesha watuhumiwa wa uhalifu ni kuimarisha ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala ya jinai na kudhibiti watuhumiwa wa uhalifu kukimbilia katika mataifa mengine. Aidha Wizara imepitia mikataba ya urejeshwaji wa wahalifu watoro kutoka nchi mbalimbali na kujadili namna bora ya kuboresha mikataba husika.

## XIII. Kuboresha Utendaji na Maendeleo ya Rasilimaliwatu iliyo chini ya Wizara

### (a) Wizara ya Katiba na Sheria

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara inaendelea kusimamia maendeleo ya Watumishi kwa kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Katika kipindi hicho, watumishi **tisa (9)** walipandishwa vyeo; **watatu (3)** walipata uteuzi; **30** walithibitishwa vyeo, mtumishi mmoja (**1**) ajira mpya; Watumishi **25** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu; **31** walihamia wizarani; **10** walihama; na wawili (**2**) walistaafu. Katika kipindi husika Wizara imeendelea kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwapatia watumishi vitendea kazi vikiwemo kompyuta na magari.

### (b) Tume ya Utumishi wa Mahakama

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kusimamia uendeshaji wa Mahakama ikiwa ni pamoja na masuala mbalimbali yanayohusu watumishi wa Mahakama kama vile uteuzi, ajira mpya, maslahi ya watumishi, bajeti na masuala ya nidhamu na maadili. Katika kipindi husika, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliajiri katika Masharti ya Kudumu na Malipo ya Pensheni pamoja na kuwathibitisha kazini watumishi **158**. Aidha kwa upande wa watumishi wa Tume waliajiriwa watumishi watatu **(3)** na uteuzi wa Naibu Katibu wa Tume anayeshughulikia Nidhamu na Maadili ya watumishi wa Mahakama. Aidha, Tume ilifanya vikao **vitatu (3)** na kushughulikia masuala mbalimbali ikiwemo kumshauri Mhe. Rais kuhusu Uteuzi wa Majaji **22** wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Msajili wa Mahakama ya Rufani pamoja na kuteua Katibu wa

Msajili Mkuu wa Mahakama kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Mahakama. Tume ilishughulikia mashauri **18** ya kinidhamu ambapo watumishi watatu **(3)** walifukuzwa kazi kati ya hao **mmoja (1)** ni Hakimu, watumishi wawili **(2)** ambao ni Mahakimu walipewa onyo na watumishi 13 walirejeshwa kazini kati ya hao wawili **(2)** ni Mahakimu.

***90. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi za Mikoa na Wilaya, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilifanya ziara kwenye Mikoa minne ya Dodoma, Singida, Shinyanga na Simiyu. Lengo la ziara hiyo ni kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama pamoja na elimu kwa umma kuhusu uwepo wa Kamati hizi. Aidha, watendaji wa Tume walifanya ukaguzi kwenye mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu na Mara kwa Lengo la kuangalia namna Kamati zinavyotekeleza majukumu yake pamoja na kupokea maoni ya kuboresha utendaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama.

### (c) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliajiri watumishi wapya **47** ambapo watumishi **45** ni Mawakili wa Serikali na watumishi **wawili (2)** ni maafisa TEHAMA. Aidha watumishi **13** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu.

### (d) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

***92. Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya rasilimaliwatu. Hadi kufikia Machi, 2023 Ofisi ilikuwa na jumla ya watumishi **886** kati ya hao, Mawakili wa

Serikali ni **603,** Makatibu Sheria ni **84** na kada nyingine ni **199.** Kati ya watumishi hao, watumishi **354** ni ajira mpya ambao wameajiliwa katika kipindi hiki (Mawakili **282,** Makatibu Sheria **70,** Mchumi **1** na Katibu Mahsusi **1**). Aidha, Ofisi imeweza kuthibitisha kazini mtumishi **mmoja (1),** kupandishwa vyeo watumishi **sita (6),** kuratibu uteuzi kwa watumishi **watano (5**) na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi **56.**



**Picha Na.9:** *Naibu Waziri wa Katiba na Sheria,Mheshimiwa Pauline P. Gekul(Mb.), akifungua Mafunzo ya Utangulizi (Indunction Course) kwa Waajiri Wapya* ***354*** *wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka*

## (e) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kusimamia masuala mbalimbali yanayohusu watumishi kama vile uteuzi, ajira mpya, maslahi ya watumishi, mafunzo na masuala ya nidhamu na maadili. Katika kipindi husika, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jumla watumishi **220** kati ya

watumishi **312** wanaohitajika kulingana na Ikama ya Taasisi. Kati ya watumishi waliopo mawakili **ni 128** na kada nyingine ni **92**. Aidha, Ofisi imewathibitisha kazini watumishi **24**, watumishi **watatu (3)** waliteuliwa, na ajira mpya katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni watumishi **44**. Vilevile watumishi **27** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi **28** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

### (f) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Mhe. Rais aliteua makamishna **sita (6)** wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imefanya uteuzi wa Wakurugenzi watano **(5)**; imewapandisha vyeo watumishi wanne **(4)**; imepokea watumishi watano **(5)** wa ajira mpya; watumishi wawili **(02)** wamestaafu kwa mujibu wa sheria; watumishi **12** wamehamia; watumishi watano **(5)** wamehama na watumishi **30** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

### (g) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

***95. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi, 2023 Mhe. Rais amemteua Katibu Mtendaji wa Tume pamoja na Makamishna Wawili (2) wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Aidha, watumishi **(3)** walipata uteuzi, watumishi **20** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi **(2)** wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi wanne **(4)** wamehamia na mtumishi **mmoja (1)** ameajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni. Katika kipindi husika Tume imeendelea kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwapatia watumishi vitendea kazi vikiwemo kompyuta, vishikwambi na magari.

**(h) Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini**

***96. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2023 Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini ilipandisha vyeo watumishi **wawili (2),** watumishi **163** walipatiwa mafunzo kwa mchanganuo wa watumishi **160** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi **watatu (3)** muda mrefu, watumishi **wawili (2)** walihamia, watumishi **23** walihama na watumishi **watatu (3)** wamestaafu kwa mujibu wa sheria.

**(i) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo**

***97. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi, 2023 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeajiri watumishi watatu **(3),** watumishi sita **(6)** wamepandishwa vyeo, watatu **(3)** wamepata uteuzi, watano **(5)** walihamia na sita **(16)** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

**(j) Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto**

***98. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 mtumishi **mmoja (1)** wa kada ya ustawi wa wanachuo ameajiriwa, watumishi **sita (6)** wamepandishwa vyeo, watumishi **watano (5)** wamehamia, watumishi **saba (7)** wamehamishwa, mtumishi **mmoja (1)** amethibitishwa kazini na watumishi **tisa (9)** wamethibitishwa katika vyeo vyao. Aidha, jumla ya watumishi **45** wamepata mafunzo ambapo, watumishi **39** walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi **sita (6)** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu.

## XIV. Kuratibu Majukumu ya Taasisi, Mipango na Miradi

(a) **Kuratibu utekelezaji wa Majukumu ya taasisi zinazosimamiwa na Wizara**

### *i. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania*

***99. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi ilidahili jumla ya wanafunzi **1,348** sawa na asilimia **89.9** ya lengo la udahili wa wanafunzi **1,500** kwa kundi la 35 na 36. Aidha, katika kipindi husika, Taasisi imetoa wahitimu **363** wanaostahili kusajiliwa kuwa mawakili na kufanya idadi ya wahitimu waliopata mafunzo kupitia Taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia **8,255**. Idadi ya wahitimu katika kipindi husika imeongezeka kwa asilimia **23.9** ikilinganishwa na wahitimu **293** wa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Vilevile, Taasisi ilipata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na kuanzisha programu ya mafunzo ya watoa huduma ya msaada wa kisheria ngazi ya cheti. Katika kipindi husika, Taasisi ilidahili kwa mara ya kwanza jumla ya wanafunzi **15** katika programu hiyo.



Picha Na. 10: *Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania wakifanya mazoezi ya uendeshaji wa Mashauri Mahakamani*

***100. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mfumo wa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha lengo la kuanzishwa kwa Taasisi hiyo linatekelezwa kwa maendeleo ya tasnia hiyo ya sheria nchini. Mojawapo ya hatua muhimu zilizochukuliwa katika kipindi hicho ni kuchukuliwa kwa hatua muhimu na za haraka za kutafuta ufumbuzi wa malalamiko ya baadhi ya wanafunzi na wadau mbalimbali wa tasnia ya sheria kuhusu ufaulu wa kiwango cha chini wa wanafunzi katika Taasisi hiyo hususan baada ya kutangazwa kwa matokeo ya mitihani ya Kundi la 33 tarehe 5 Oktoba, 2022.

***101. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliunda Kamati ya Tathmini ya Mafunzo yanayotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo. Jukumu kuu la kamati hii ilikuwa kuchunguza na kutathmini hali na mwenendo wa mafunzo na mfumo wa kutahini wanafunzi wa mafunzo uanasheria kwa vitendo yanayotolewa na Taasisi hiyo. Kamati hiyo ilikamilisha kazi yake

na kutoa taarifa ambayo imeiwezesha Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mafunzo hayo na pia kuchukua hatua za kuimarisha elimu ya sheria nchini.

***ii. Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto***

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha watumishi wa Mahakama na wa sekta ya sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha katika kutimiza wajibu wao wa utoaji haki kwa ufanisi, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kuratibu na kutoa mafunzo endelevu na elekezi kwa watumishi wa Mahakama na wadau wa sekta ya sheria nchini. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Chuo kimeratibu mafunzo ya awali na elekezi kwa watumishi wapya **237** wa Mahakama ya Tanzania, mafunzo hayo yanajumuisha kada za Majaji **20**, mahakimu **20**, madereva **35**, makatibu muhtasi **80**, maafisa hesabu **17**, wakaguzi wa ndani nane (**8)**, Maafisa tawala **watano** (**5)**, Maafisa utumishi **nane** (**8)**, wasaidizi wa kumbukumbu **38**, Maafisa Ugavi **sita** (**6)** na maafisa TEHAMA **wanne** (**4)**.

Chuo kimeratibu mafunzo kwa waendesha mashtaka na wapelelezi kwa jumla ya washiriki **250** katika kuboresha utendaji wa kazi ili kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani. Pia katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Chuo kimeratibu mafunzo kwa waandishi wa Habari wa Mahakama ya Tanzania kwa washiriki **55** wakiwemo waandishi **34** wa habari za ndani ya Mahakama **21** waandishi wa habari za nje ya Mahakama.



**Picha Na.11:** *Mkufunzi kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto akiendesha mafunzo endelevu na elekezi kwa watumishi wa Mahakama na wadau wa sekta ya sheria nchini*

***103. Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimeendelea kuratibu mafunzo mbalimbali endelevu ya Kimahakama ambapo watumishi **1,101** wa Mahakama ya Tanzania waliweza kupatiwa mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo katika maeneo mbalimbali. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa njia ya ana kwa ana au kwa njia ya mtandao ili kuwafikia watumishi wengi zaidi. Vilevile, chuo kimeratibu mafunzo kwa wananchi wenye nia ya kuwa madalali wa Mahakama na wasambaza nyaraka za Mahakama **31**. Katika jukumu la kufanya tafiti za kimkakati Chuo kimefanikiwa kufanya utafiti kuhusu Tamaduni za Kimahakama Tanzania (*Judicial culture*) kwa lengo la kuzijua tamaduni hizo ili kuboresha utendaji kazi na kujua njia bora zaidi za kuboresha mahakama.

***104. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo, Chuo kwa kupitia Mahakama ya Tanzania kimekamilisha ujenzi wa Hosteli ya wanachuo wa kiume ambayo inatoa huduma ya malazi kwa jumla ya wanachuo **400** ndani ya Chuo ambayo ni ongezeko kutoka wanachuo **435** kwa mwaka wa masomo 2021/2022 hadi wanachuo **835** kwa mwaka wa masomo 2022/2023 waliopata malazi ndani ya Chuo na kuweza kutatua changamoto ya upungufu wa malazi kwa wananchuo kwa **92%.** Aidha, Chuo kimeweza kuongeza mapato ya ndani kwa kiasi cha **Shilingi 117,600,000** kutokana na ada za wanafunzi wanaoishi kwenye hosteli hizo. Hata hivyo Chuo kimejipanga kufanya ukarabati wa vyumba vya malazi vilivyoharibika katika majengo yake ili kutatua changamoto za malazi kwa wanachuo wanaoishi hosteli binafsi.

## (b) Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zake

***105. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na taasisi zake imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ya ujenzi wa majengo, kuimarisha mifumo ya utoaji haki, uwajibikaji wa kitaasisi katika kupambana na rushwa na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika utoaji wa Huduma za Kimahakama. Miradi hiyo inayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

### (a) Miundombinu ya Utoaji Haki

***107. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama, ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi,

2023 miradi **36** ilitekelezwa katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

### i. Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama iliyokamilika

***108. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama **tatu (3)** za hakimu mkazi katika Mikoa ya Lindi, Songwe na Katavi. Aidha, ujenzi wa Mahakama za Wilaya **28** katika Wilaya za Same, Mwanga, Tandahimba, Nanyumbu, Namtumbo, Mvomero, Gairo, Ngara, Kilombero, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'hwale, Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Bunda, Kilindi, Rungwe na Sikonge umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mahakama ya mwanzo katika Wilaya ya Kilindi eneo la Kimbe na ukarabati wa Mahakama Kuu ya Tabora pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi umekamilika. Kukamilika kwa miradi hiyo kumewezesha kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi.



**Picha Na. 12:** *Majengo ya Mahakama za Wilaya yaliyokamilika na yanaendelea kutoa huduma kushoto ni Mahakama ya Wilaya Chemba na Kulia ni Mahakama ya Wilaya Mwanga*

***109. Mheshimiwa Spika,*** miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama inayoendelea na asilimia ya ukamilishaji kwenye mabano ni pamoja na Ujenzi wa Jengo la

Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania Jijini Dodoma **(asilimia 85),** Ujenzi wa nyumba za Majaji Iyumbu-Jijini Dodoma (**asilimia 54**); ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma (**asilimia 10)**; Ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Ulanga (asilimia 35), Ubungo (**asilimia 40**), Liwale (**asilimia** 70), na Kwimba (**asilimia** 80); ukarabati wa jengo la Mahakama ya Wilaya Maswa (**asilimia 80);** na Ujenzi wa Mahakama za mwanzo **nane (8)** za Kinesi (**asilimia 95**), Mahenge (asilimia 95), Luilo (**asilimia** 80), Newala (**asilimia** 75), Usevya (**asilimia** 95), Nyakibimbili (**asilimia** 90) na Kabanga (**asilimia** 80) na Madale (**asilimia** 75).

***110.* Mheshimiwa Spika,** miradi mingine inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa jengo la Huduma Jumuishi za Sheria linalojengwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jijini Mwanza (**asilimia 45)**; ujenzi wa majengo ya Huduma Jumuishi za Sheria yanayojengwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika mikoa ya Kimashtaka ya Morogoro (**asilimia** 7**5)**, Ilala (Kinyerezi) (**asilimia 98)**, Pwani (asilimia **98)** na Mbeya (**asilimia** 75), Shinyanga (**asilimia 35),** Manyara (**asilimia 35**), Njombe (**asilimia 10),** Katavi (**asilimia 10)** na Rukwa (**asilimia 15).**




**Picha Na. 13:** *Ujenzi wa Jengo la Huduma Jumuishi za Sheria linalojengwa na Ofisi ya Taifa Mashtaka katika Mkoa wa Kimashtaka wa Ilala, eneo la Kinyerezi, ukiendelea kukamilishwa.*

**ii. Mradi wa maboresho ya Mifumo ya Huduma za Mahakama**

***111. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unaotekelezwa na Mahakama unalenga katika kuimarisha utoaji wa huduma za haki kwa wananchi. Kazi zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ni pamoja na ujenzi wa mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri, na kuboresha mifumo mingine ya TEHAMA, utoaji wa mafunzo kwa watumishi **1,036**, maboresho ya kanuni **tisa (9)** na uchambuzi wa sheria na taratibu zinazosabishwa ucheleweshaji wa utoaji wa Haki.

**(b) Miradi mingine ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara**

***112. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na miradi ya ujenzi, Wizara na Taasisi zake imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuboresha huduma za Sekta ikiwemo:-

**i. Mradi wa UNICEF Multisectoral Support**

***113. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na Wizara, Wakala ya Usajili Ufilisi na Udhamini na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Lengo la mradi huu ni kuimarisha ulinzi wa haki za mtoto. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia mradi huu ilitekeleza yafuatayo: Kuratibu kikao cha Jukwaa la Haki Mtoto lililohusisha wadau kutoka taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kwa lengo la kujadali utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Haki Mtoto; Kuratibu zoezi la kukusanya maoni ya wananchi kuhusu maboresho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na kuchambua maoni hayo na kuandaa taarifa kuhusu maoni hayo; Kuratibu kikao kazi cha wadau wanaotekeleza Eneo Na. 5 la MTAKUWWA la Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wanawake na Watoto; na Kuzindua Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia “***Mama Samia Legal Aid Campaign***” pamoja na mkakati wa utekelezaji wake. Kampeni hiyo itakuwa ya miaka mitatu (2023/242025/26) na inalenga

kutoa elimu ya kisheria, mirathi, ndoa, na taratibu za upatikanaji wa haki na wajibu kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi.

***114. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia RITA ilisajili jumla ya watoto **319,624** wenye umri chini ya miaka mitano katika mikoa **23** ya Tanzania Bara inayotekeleza mpango huo.

***115. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuhusu mradi huu ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

**i.** Kuendesha kikao kazi cha Mawakili wanaoshughulikia masuala ya Watoto wanaokinzana na sheria kutoka katika Ofisi za Mashtaka za Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Lengo la kikao kazi hicho lilikuwa ni kuboresha mfumo wa utoaji Haki – Jinai kwa Watoto. Maazimio ya kikao kazi hicho ni pamoja na kuhakikisha kwamba watoto wote wanaokinzana na sheria wanapata haki zao ikiwemo kutokupewa adhabu ya kifungo cha kwenda magerezani na kesi zao zinamalizika kwa wakati kwa mujibu wa sheria;

**ii.** Kufanya ukaguzi wa watoto wanaokinzana na sheria katika vizuizi vya magereza, vituo vya polisi, mahabusu za watoto na shule za maadilisho ikiwa ni njia ya utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Miaka Mitano wa Haki za Mtoto. Ukaguzi huo ulifanyika kwa kushirikiana na wadau kutoka Polisi Dawati la Jinsia, Magereza na Ustawi wa Jamii na Wakili anayeshughulikia masuala ya Watoto katika Ofisi ya Mashtaka ya mkoa husika. Aidha, ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa **26** ya Tanzania Bara na mikoa mitatu **(3)** ya Kimashtaka ambayo ni Temeke, Kinondoni na Ilala. Ukaguzi ulifanyika katika Magereza **37**, Vituo vya Polisi **36**, Mahabusu za watoto Tano **(5)** na Shule ya maadilisho Moja **(1)**. Lengo la ukaguzi huo ni kutekeleza Sheria ya Huduma za Mashtaka, Sura ya 430 na Sheria ya Mtoto Na. 21

ya mwaka 2009. Hatua zilizochukuliwa baada ya ukaguzi huo ni pamoja na kuelekeza watoto ambao walishtakiwa katika Mahakama ya kawaida, washtakiwe katika Mahakama ya watoto na wale wote ambao umri wao una utata majalada yao yasomwe upya na umri wao ufanyiwe uchunguzi na mahakama itoe maamuzi juu ya umri wao sahihi.

**ii. Mradi/Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa**

**Tanzania (Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania - BSAAT**):-

***116. Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi zake, zimetekeleza mradi wa BSAAT wenye lengo la kujenga mifumo ya kuzuia vitendo vya rushwa hapa nchini. Hadi kufikia Machi, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuandaa rufaa za viashiria vya rushwa na kuviwasilisha TAKUKURU;

ii. Kukamilisha kushughulikia Mashauri 15 ya Rushwa Kubwa katika Mahakama ya Rushwa na Uhujumu Uchumi;

iii. Kufanya uratibu wa upatikanaji na urejeshwaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu;

iv. Kuandaa na kushiriki kwenye kikao cha kupokea maoni ya wadau kwenye Rasimu ya Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Rushwa na kesi nyinginezo (*Standard Operating Procedures – SOPs*);

v. Kufanya mapitio ya majalada **55** ya kesi za rushwa kwa ajili kuwajengea uwezo Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa mitano (5) ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya na Mwanza

ya Programu ya Kujenga mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania;

vi. Kuendesha mafunzo elekezi kwa Waendesha Mashtaka wa Mikoa kuhusu Mwongozo wa Kiutendaji kwa Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Rushwa na kesi nyinginezo (Standard Operating Procedures – SOPs) na Mwongozo wa Maridhiano ya Kukiri (Plea Bargaining Guidelines). Mafunzo hayo yamewezesha Waendesha Mashataka wa mikoa kuwa na uelewa wa kutosha kusimamia utekelezaji wa miongozo husika;

vii. Kuratibu vikao **viwili (2)** vya kazi na kuwakutanisha wataalam kwa ajili ya kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Ndani wa Kushughulikia Maombi ya Msaada wa Kisheria (Internal Guidelines on Mutual Legal Assistance) na pia Mwongozo wa Ulinzi wa Mashahidi;

viii. Kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa SOPs katika katika mikoa mitano **(5)** ambayo mpango wa BSAAT unatekelezwa ili kupima utekelezaji wa Mwongozo huu. Mikoa hiyo ni pamoja na Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma na Iringa; na

ix. Uzinduzi wa Kanuni za Kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa za Mwaka 2023 na kutoa mafunzo kuhusu kanuni hizo kwa taasisi wadau wa Haki Jinai.

## XV. Utekelezaji wa Masuala ya Kisheria katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa

***117. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria wa kikanda na kimataifa, Wizara ilishiriki kwenye Mkutano Maalum wa Saba wa Umoja wa Afrika. Katika mkutano huo jumla ya itifaki **tatu (3)** zilipitiwa na kupitishwa ikiwemo Itifaki ya Ushindani, Itifaki ya Uwekezaji

kwenye kuanzisha Soko la Pamoja na Itifaki ya Haki Miliki na Ubunifu.




**Picha Na. 14**: *Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi.Mary G. Makondo akishiriki Mkutano Maalum wa Saba wa Umoja wa Afrika wa Wataalam wa Sheria kwa ajili ya kupitisha Itifaki za Kisheria*

***118. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilishiriki katika mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi za Jumuia ya Madola ulifanyika nchini Mauritius. Katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano ujao, unaotarajiwa kufanyika visiwani Zanzibar. Sambamba na hilo, Wizara imefanya kikao na Taasisi ya Kimataifa inayosimamia Sheria Binafsi za kimataifa (The Hague Conference on Private International Law - HCCH). Lengo lilikuwa kuishawishi Tanzania iwe mwanachama katika taasisi hiyo ambapo Serikali inaendelea kulifanyia kazi ombi hilo. Vilevile, Wizara ilishiriki katika kikao cha kufanya tathimini ya udhibiti wa fedha haramu na utakatishaji wa fedha na kupambana na ugaidi. Kikao hicho kilifanyika Zambia ambapo Tanzania iliwasilisha taarifa iliyowezesha nchi kuondolewa kuwa katika uangalizi maalum.

## E. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2020-2025

***119. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa ikiwa ni pamoja na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake imetekeleza maelekezo mbalimbali ya Ilani ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo: -

### I. Kuendeleza Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ubadhirifu

***120. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi katika kusikiliza mashauri. Katika kipindi hicho, jumla ya mashauri **19** yalifunguliwa na kufikisha jumla ya mashauri **40** yaliyosajiliwa. Hadi Machi 2023 mashauri **14** yamehitimishwa na **26** yanaendelea kusikilizwa.

### II. Kuchukua hatua zaidi za kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani

***121. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi kufikia Machi, 2023 mlundikano wa kesi umepungua kwa asilimia **25** kutoka kesi **9,399** mwezi Machi, 2022 hadi Mashauri **6,994** mwezi Machi, 2023. Hatua zilizochukuliwa ili kupunguza mlundikano wa kesi ni pamoja na;

a) Kufuta kesi zisizokuwa na ushahidi;

b) Kutumia mfumo wa kumaliza kesi kwa njia ya makubaliano na majadiliano (plea bargaining);
c) Kuimarisha mfumo wa ufifishaji wa makosa;
d) Kutumia mahakama zinazotembea (mobile court) na mahakama mtandao *(virtual court)* katika kuendesha kesi; na
e) Kutekeleza mkakati wa kumaliza kesi za muda mrefu.

**III. Kuhakikisha huduma bora za sheria zinapatikana kwa wakati na kwa gharama nafuu kwa kuongeza wataalam, miundombinu, vitendea kazi na kusogeza huduma karibu na wananchi**

***122. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tatu **(3)** umekamilika. Mahakama hizo ni Matiri (Mbinga), Hydom (Mbulu) na Kibaigwa (Kongwa). Vilevile, mahakama inaendelea na ujenzi wa mahakama za mwanzo katika maeneo ya Mlimba na Mang'ula (Morogoro), Chanika (Dar es Salaam), Kabanga (Ngara), Nyakibimbiri (Bukoba) na Kimbe (Kilindi). Mahakama inaendelea na Mpango wa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo **60** katika kata ambazo zipo makao makuu ya tarafa kwa lengo la kusogeza huduma ya utoaji haki karibu na wananchi.

**IV. Kuimarisha mfumo wa wasajili wasaidizi katika halmashauri zote ili kuwezesha uratibu na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi, ikiwemo msaada wa huduma za kisheria kwa masuala ya mirathi na ndoa**

***123. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imesajili Wasaidizi wa Sheria **305** katika mikoa ya Rukwa, Mtwara, Songwe, Singida, Pwani, Mara, Kilimanjaro, Tanga, Lindi, Iringa, Kigoma, Njombe, Tabora, Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Ruvuma, Manyara na Geita

ambao wanatoa huduma ya msaada wa kisheria ikiwemo masuala ya mirathi na ndoa.

**V. Kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa huduma za kimahakama na kwenye uandishi wa nyaraka za kisheria**

***124. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, idadi ya Sheria Kuu zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kuwa Kiswahili kwa hatua ya rasimu ya awali ni **244**. Aidha, Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania imekamilisha kuandaa mfumo wa akili bandia ambao unarekodi na kutafsiri mwenendo wa usikilizwaji wa mashauri kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza. Mfumo huo uko katika hatua za majaribio.

**VI. Kujenga mifumo ya TEHAMA na kuendelea kuhimiza matumizi ya mfumo katika utoaji haki**

***125. Mheshimiwa Spika,*** Wizara, Mahakama ya Tanzania pamoja na taasisi **tano (5)** ambazo ni Wakala ya Usajili Ufilisi na Udhamini, Tume ya Utumishi Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zimeimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki ikiwemo wananchi kuweza kufungua na kufuatilia malalamiko; kuwezesha kufungua mashauri kwa njia ya kielektroniki; kusajili vizazi, vifo na bodi za wadhamini kielektroniki; kusajili, kutambua na kusimamia madalali wa Mahakama na kutoa mrejesho wa huduma zitolewazo na Mahakama kupitia simu janja. Huduma nyingine ni; Huduma ya kupokea malalamiko, usajili wa watoa huduma wa msaada wa kisheria, usajili wa watatuzi wa migogoro kwa njia mbadala za usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano, na maombi ya kupatiwa msaada wa kisheria.

## F. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### (i) Makusanyo ya Maduhuli

***126. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara pamoja na Taasisi ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 12,676,201,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na ada ya watoa huduma za msaada wa kisheria pamoja na ada za kusajili mashauri, ada za mawakili na faini zinazotokana na mashauri mbalimbali pamoja na pango la ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara ilikusanya jumla ya **Shilingi 6,798,115,487.74** Kama linavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1 Mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa kwa kila Fungu kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023**

| MAFUNGU | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOKUSANYWA JULAI 2022-MACHI, 2023 |
|---|---|---|
| Fungu 35 | 60,000,000.00 | 56,400,000.00 |
| Fungu 40 | 12,571,199,000.00 | 6,720,995,487.74 |
| Fungu 41 | 45,000,000.00 | 20,720,000.00 |
| Fungu 55 | 2,000.00 | 0 |
| **JUMLA** | **12,676,201,000.00** | **6,798,115,487.74** |

### (ii) Bajeti Iliyoidhinishwa

***127. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 272,768,278,800.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 95,356,423,800.00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, **Shilingi 112,347,285,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 65,064,570,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi

ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya **Shilingi 53,112,800,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 11,951,770,000.00** ni fedha za nje.

**(iii) Fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi**

***128. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 187,452,301,201.00** sawa na asilimia **68.7** ya **Shilingi 272,768,278,800.00** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya hizo **Shilingi 62,743,442,184.00** ni mishahara sawa na asilimia **66** ya bajeti iliyopitishwa na **Shilingi 83,054,287,447.00** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **74** ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 41,654,571,569.00** sawa na **asilimia 64** ya fedha zilizoidhinishwa ambazo zinajumuisha **Shilingi 35,360,261,424.00** fedha za ndani na **Shilingi 6,294,310,145.00** ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2, 3 na 4.**

**G. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA**

***129. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:-

a. Kuimarika kwa haki za binadamu na watu za kisiasa na kidemokrasia kwa Serikali kuruhusu mikutano ya kisiasa;

b. Kuimarika kwa haki za binadamu katika masuala ya kiuchumi kwa kufungua fursa za kiuchumi na uwekezaji;

c. Kuimarika uhifadhi, ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu kulikopelekea Tanzania kuwa mwenyekiti wa Mawaziri wa Sheria wa Haki Umoja wa Afrika na kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa mawaziri wa Sheria na Haki wa jumuia ya madola wa mwaka 2024 na kuwa mwenyeji wa

mkutano wa 77 wa kamisheni ya Afrika ya haki za Binadamu na Watu mwaka 2023;

d. Kuimarika kwa ushirikiano na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuweza kuratibu ziara ya Makamishina wa Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu katika maeneo ya Kijiji cha Msomera, Ngorongoro na Loliondo nchini katika mwaka 2022/2023. Katika ziara hiyo Kamisheni ilijionea jinsi Tanzania inavyolinda na kuhifadhi haki za wakazi waliohamia Kijiji cha Msomera kutoka Ngorongoro na Loliondo.

e. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa umma hadi kufikia ngazi za mikoa, wilaya, tarafa na vijiji;

f. Kuongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria kupitia uzinduzi wa ***Mama Samia Legal Aid Campaign*;**

g. Kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa kutafsiri kanuni za Upatanishi na Maridhiano, kuandaa miongozo ya mafunzo ya Usuluhishi, Upatanishi, Uendeshaji Maridhiano na Majadiliano na mwongozo wa kuendeshea vikao vya Jopo la Ithibati la Waendesha Usuluhishi, Upatanishi, Majadiliano na Maridhiano;

h. Kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi tatu (3), Mahakama za Wilaya **28** na Mahakama ya Mwanzo **moja (1)** pamoja na ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu moja (1) na jengo la **moja (1)** la Mahakama ya Hakimu Mkazi hivyo kusaidia kusogezwa Huduma za Mahakama karibu na wananchi;

i. Kupungua Mlundikano wa Mashauri kutoka **5,242** katika mwaka 2021/22 hadi kufikia Mashauri **2,706** kwa mwaka 2022/23;

j. Uteuzi wa majaji **22** wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Msajili wa Mahakama ya Rufani;



**Picha Na. 15:** *Mheshimiwa Dkt. Samia Suliuhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa kitaifa na Majaji wapya walioapishwa*

k. Kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za utoaji haki ambayo (i) imeimarisha upatikanaji wa huduma kwa wakati na kwa gharama nafuu; (ii) imepunguza mlundikano kutoka asilimia 11 Desemba, 2021 hadi asilimia nne (4) Machi, 2023 ; (iii) imepunguza wastani wa siku tangu kufunguliwa hadi kuisha kwa mashauri kutoka siku 119 hadi siku 95; (iv) imeongeza uwezo wa kumaliza mashauri kutoka asimilia 99 hadi 106; (v) imeongeza uwezo wa uondoshaji wa mashauri kutoka asilimia 78 hadi 84; na (vi) imepunguza wastani wa mzigo wa mashauri kwa jopo kwa jaji kwa asilimia 3 Mahakama ya Rufani na asilimia 11 Mahakama Kuu;

l. Kukamilika kwa Mfumo wa Akili Bandia utakaorahisisha mwenendo wa usikilizaji wa mashauri kwa lugha ya Kiswahili, Kingereza pamoja la lugha nyingine kulingana na mahitaji;

m. Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwa ufanisi katika mashauri ya madai **6,320** (ikiwa ni pamoja na mashauri ya Kikatiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi) na usuluhishi **157** na hivyo kufanikiwa kurejesha mali mbalimbali za Serikali zilizokuwa zimechukuliwa isivyo halali pamoja na kuepuka gharama kubwa za Mawakili wa kujitegemea;

n. Kuongezeka kwa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano takriban asilimia **65** hadi kufikia mwaka 2023;

o. Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi katika huduma zinazotolewa na taasisi za Wizara kwa kupitia matangazo na vipindi vya redio na runinga zaidi ya 30 na mafunzo ya haki za binadamu na uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora kwa Masheha 144 kwa Tanzania Zanzibar;

p. Kuimarika kwa utawala wa sheria kupitia kaguzi zilizofanywa katika magereza, mapitio ya majalada pamoja na kaguzi za utendaji kazi katika Ofisi za Mashtaka Mikoa na Wilaya. Katika kaguzi hizo jumla mahabusi **333** waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka mbalimbali ya jinai walifutiwa mashtaka na kuachiwa huru.

q. Kusogeza huduma za mashtaka kwa wananchi kwa kuanzisha Ofisi ya Mkoa wa Kimashtaka wa Tarime pamoja na kuwapatia vibali Waendesha Mashtaka **783** kutoka taasisi na ofisi mbalimbali za Serikali;

r. Kuimarisha utendaji wa sekta ya sheria kwa kuajiri watumishi wapya **434,** wakiwemo Mawakili wa Serikali **358**, Makatibu Sheria **74** na Maafisa TEHAMA **wawili (2)** ambao wameongeza idadi ya watumishi kwenye sekta ya sheria na hivyo kuimarisha upatikanaji haki;

s. Kuimarika kwa shughuli za utafiti, mapitio tathmini na elimu ya sheria kwa umma hali iliyowezesha kutolewa kwa mapendekezo ya kuimarisha mfumo wa sheria unaosimamia masuala ya udhamini, mapitio ya mfumo wa Sheria unaosimamia utoaji haki katika Mahakama za Mwanzo, pamoja na mapitio ya mfumo wa Sheria Unaosimamia Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Demokrasia;

t. Kuandaa miswada ya Sheria **10** ambapo **8** kati ya hiyo ilipitishwa na Bunge kuwa Sheria. Sheria zilizopitishwa zinaimarisha maeneo mbalimbali ya utendaji ikiwemo Usimamizi wa Maafa; Usimamizi wa Rasilimali ya Maji, Usimamizi wa Fedha; Ulinzi wa Taarifa Binafsi; na kuimarisha Uwekezaji;

u. Kuchangia katika kuwezesha utekelezaji wa Sheria za kisekta zilizotungwa kwa kuhakiki Sheria ndogo **489** ambazo zinaweka utaratibu wa kutekeleza Sheria Kuu;

v. Kuimarika kwa usimamizi wa Mawakili wa Serikali kwa kuanzisha Chama cha Mawakili wa Serikali;

w. Kuimarika kwa utoaji haki kwa kuwaweka wadau wa utoaji haki katika jengo moja kupitia majengo ya Vituo Jumuishi vya Mahakama Dodoma, Arusha, Temeke, Ilala, Morogoro na Mwanza;

x. Kusogeza Huduma za kisheria karibu na wananchi kwa kuanza programu ya ujenzi wa majengo jumuishi ya Huduma za kisheria katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Ilala, Pwani, Mbeya, Shinyanga, Manyara, Njombe, Katavi, Dodoma na Rukwa;

y. Kumaliza mashauri kwa njia mbadala za utatuzi wa migogoro ikiwemo usuluhishi, majadiliano, na maridhiano. Kwa mfano katika kipindi husika, mashauri matatu ya kimataifa

yamehitimishwa kwa njia majadiliano na kuweza kuokoa **Shilingi trillion 7.57** ambazo Serikali ingelipa kama ingeshindwa mashauri hayo pamoja na kuepuka gharama nyingine za uendeshaji wa mashauri ambazo zinajumuisha usafiri na posho kwa Mawakili wa Serikali na mashahidi; ada za mahakama; na

z. Kuimarika kwa mifumo mbalimbali ya usimamizi wa Sheria kupitia mapitio ya Sheria yaliyofanyika katika sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa, 2023; Sheria zinazosimamia Masoko ya Mazao ya Kilimo Tanzania, 2022; Sheria Zinazosimamia Vyama vya Kijamii, 2022; Sheria Zinazosimamia Wazee wa Mahakama, 2021; Sheria Zinazosimamia Uwakilishi Mahakamani, 2021; Sheria inayosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kazi, 2021.

## H. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

***130. Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kisheria ikiwemo elimu ya sheria, uwakilishi Mahakamani na uandaaji wa nyaraka za kisheria ikilinganishwa na uwezo wa kuwafikia umma unaohitaji huduma hiyo;

ii. Wananchi kutojua wajibu wao wakati wa kudai haki;

iii. Kuendelea kujitokeza kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, dhidi ya watoto na uvunjifu wa haki za binadamu; na

iv. Kuongezeka kwa makosa ya mtandaoni ikilinganishwa na uwezo wa kuyabaini.

## I. MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

***131. Mheshimiwa Spika,*** Katika kutatua changamoto zilizotajwa, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

i. Kuandaa Kampeni ya kutoa huduma ya msaada wa kisheria ijulikanayo kama ***Mama Samia Legal Aid Compaign*** ambayo inalenga kutoa Elimu ya sheria, mirathi, wosia pamoja na huduma ya msaada wa kisheria Tanzania Bara na Zanzibar katika mikoa na wilaya zote;

ii. Kukamilisha Mkakati wa kutoa Elimu kwa umma kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kikatiba;

iii. Kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya uzingatiwaji wa sheria katika uhifadhi na ulinzi wa haki za binadamu; na

iv. Kuwapatia mafunzo endelevu wataalamu wa sekta ili kuweza kukabiliana na uwapo wa makosa yanayotendeka kwa kutumia teknolojia za kisasa.

## J. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

***132. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara na Taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za Sheria na Utoaji Haki kwa umma ili kuendana na mipango yake na hivyo kufikia malengo yaliyopangwa kwa kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo Wizara na Taasisi zake zimeainisha maeneo mahsusi ya vipaumbele na kuyawekea malengo na shabaha kwa ajili ya utekelezaji. Maeneo ya vipaumbele muhimu vilivyoanishwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu Mchakato wa Katiba Mpya;

ii. Kutekeleza Mkakati wa Kutoa Elimu ya Katiba kwa umma;
iii. Kutekeleza Kampeni ya Mama Samia Legal Aid Campaign kwa wananchi kote nchini;
iv. Kufanya marekebisho ya Sheria za Uchaguzi na Demokrasia;
v. Kuwasilisha taarifa kwenye vikao 16 na majukwaa ya Haki za Binadamu na Watu katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa;
vi. Kutekeleza Programu ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika utoaji Haki Nchini;
vii. Kuwasilisha taarifa tatu (3) za nchi kuhusu Utekelezaji wa Mikataba mitatu ya Haki za Binadamu ambayo Serikali imeridhia;
viii. Kuendelea kutafsiri Sheria za nchi kutoka lugha ya Kingereza kuwa katika lugha ya Kiswahili;
ix. Kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;
x. Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro; xi. Kuimarisha mfumo wa elimu ya sheria;
xii. Kuratibu mapitio na marekebisho ya sheria za sekta ya sheria
xiii. Kuandaa sera mahsusi zinazosimamia mifumo ya utoaji haki
xiv. Kuendelea kuimarisha mfumo wa uangalizi wa utajiriasili na maliasilia za nchi;
xv. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria nchini;
xvi. Kuendelea na ujenzi wa vituo jumuishi vya taasisi za sheria;
xvii. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kikatiba na utawala wa sheria;

xviii. Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki nchini;

xix. Kuimarisha mifumo ya kuhamasisha, kuzingatia na kulinda haki za binadamu na watu;

xx. Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto 2020/2021-2024/2025;

xxi. Kuendelea kuimarisha Usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu pamoja na shughuli za ufilisi na udhamini.

xxii. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya

xxiii. Kufanya Tafsiri, Uandishi na Urekebu wa sheria;

xxiv. Kutoa ushauri wa kisheria na kufanya Upekuzi na Marejeo ya Mikataba;

xxv. Kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa kesi za jinai;

xxvi. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai;

xxvii. Kuimarisha mfumo wa utaifishaji mali, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu;

xxviii. Kuimarisha utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

xxix. kuratibu, kusimamia na Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi; na

xxx. Kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

## (a) Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara na Taasisi inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 12,676,205,000.00** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Mpango wa Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa Wizara na Taasisi zake**

| FUNGU | KIASI CHA MADUHULI | |
|---|---|---|
| Fungu 19 | Sh. | 4,000.00 |
| Fungu 35 | Sh. | 60,000,000.00 |
| Fungu 40 | Sh. | 12,571,199,000.00 |
| Fungu 41 | Sh. | 45,000,000.00 |
| Fungu 55 | Sh. | 2,000.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **12,676,205,000.00** |

## (b) Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

***134. Mheshimiwa Spika,*** Ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 383,619,511,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu nane **(8)** ya Wizara na taasisi zake ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Mafungu yake kwa mwaka wa fedha, 2023/2024**

| Fungu la Matumizi | | Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|
| 1. | Mishahara ya watumishi | 97,815,618,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Matumizi mengineyo | 176,148,324,000.00 |
| 3. | Miradi ya Maendeleo-Ndani | 44,112,800,000.00 |
| 4. | Miradi ya Maendeleo- Nje | 65,542,769,000.00 |
| **JUMLA** | | **383,619,511,000.00** |

***135. Mheshimiwa Spika,*** kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama inavyoonekana hapo chini: -

**(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 734,606,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 4,861,300,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 0.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **5,595,906,000.00** |

**(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 4,072,737,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 12,290,130,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 2,000,000,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 455,000,000.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **18,817,867,000.00** |

**(iii) Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 3,629,161,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 13,446,669,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 0.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **17,075,830,000.00** |

**(iv) Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

| | | |
|---|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 14,766,538,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 47,172,391,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 6,000,000,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 860,000,000.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **68,798,929,000.00** |

**(v) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 63,579,252,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 69,620,476,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 31,002,000,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 53,777,027,000.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **217,978,755,000.00** |

**(vi) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria (RITA na LST)**

| | | |
|---|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 7,234,664,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 19,208,535,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 5,110,800,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 10,450,742,000.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **42,004,741,000.00** |

**(vii) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | | |
|---|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 2,847,924,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 5,303,614,000.000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 0.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **8,151,538,000.00** |

**Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | Sh. | 950,736,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | Sh. | 4,245,209,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | Sh. | 0.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **5,195,945,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **SH.** | **383,619,511,000.00** |

***136. Mheshimiwa Spika,*** Kwa ujumla, kiasi kinachoombwa kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu ya Wizara na Taasisi zake ni **Shilingi 383,619,511,000.00.**

***137. Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

***138. Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiwemo Mhe. Pauline Gekul (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu; na Dkt. Khatibu Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara.




**Picha Na. 15:** Viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria

***139. Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kumshukuru Mhe. Prof. Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania.




**Picha Na. 16:** *Viongozi wa Mhimili wa Mahakama ya Tanzania*

***140. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hao, napenda pia kuwashukuru Wakuu na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara wakiwemoMhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Prof. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu Dkt. Benhajj Shaaban Masoud, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Dkt. Evaristo Longopa, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali; Bi. Angela Kemanzi Anatory, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bw. Griffin Venance Mwakapeje, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Bw. Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.




**Picha Na. 17:** *Viongozi wa Taasisi chini ya Wizara ya Katiba na Sheria*

***141. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nawashukuru Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria; Mhe. Jaji Dkt. Gerlad Mbonimpa Ndika, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Mahakama Lushoto; Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Dkt. Amina Msengwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili Ufilisi na UdhaminiRITA kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao katika Tume, Mabaraza na Bodi zao na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Wizara. Sambamba nao, nawashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, naishukuru familia yangu ikiwa ni pamoja na mke wangu Bibi. Flora Ndumbaro na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. Mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu,

naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru Wapiga kura wa Jimbo langu la Songea Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika shughuli za kuleta maendeleo ya jimbo letu.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

***KIAMBATISHO A***

**MISWADA YA SHERIA ILIYOANDALIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

1. Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022;
2. Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka, 2022;
3. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Rasilimali Maji ya Mwaka, 2022;
4. Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Fedha wa Mwaka 2022;
5. Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022;
6. Muswada wa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022;
7. Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka, 2022;
8. Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa Mwaka, 2022;
9. Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma wa Mwaka 2023;
10. Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023; na
11. Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023.

***KIAMBATISHO B***

**MISWADA YA SHERIA ILIYOJADILIWA NA KUPITISHWA NA BUNGE KUWA SHERIA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

1. Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022;
2. Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka, 2022;
3. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Rasilimali Maji ya Mwaka, 2022;
4. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Fedha (Financial Provisions) ya Mwaka 2022;
5. Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022;
6. Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022; na
7. Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka, 2022.

***KIAMBATISHO C***

**ORODHA YA SHERIA NDOGO ZILIZOANDALIWA KWA LUGHA YA KISWAHILI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Kituo Kikuu cha Mabasi za Halmashauri ya Jiji la Dodoma, za Mwaka 2022. | 468 of 2022 |
| 2. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Jiji la Dodoma za Mwaka 2022. | 469 of 2022 |
| 3. | Sheria Ndogo za Usimamizi wa Masoko za Halmashauri ya Jiji la Dodoma za Mwaka 2022. | 470 of 2022 |
| 4. | Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Dodoma za Mwaka 2022. | 471 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Marekebisho ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya Mwaka 2022. | 472 of 2022 |
| 6. | Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya Mwaka 2022. | 473 of 2022 |
| 7. | Marekebisho ya Sheria Ndogo za Udhibiti wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya Mwaka 2022. | 474 of 2022 |
| 8. | Marekebisho ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli za Mwaka 2022. | 475 of 2022 |
| 9. | Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya Ya Ngara za Mwaka, 2022. | 476 of 2022 |
| 10. | Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara za Mwaka 2022. | 477 of 2022 |
| 11. | Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Jiji la Dodoma za Mwaka 2022. | 478 of 2022 |
| 12. | Kanuni za Usajili wa watoa Huduma za Kielektroniki wasio Wakaazi za Mwaka, 2022. | 478M of 2022 |
| 13. | Kanuni za Usajili wa Wauzaji wa Huduma za Kielektroniki Wasio Wakaazi, 2022. | 478N of 2022 |
| 14. | Kanuni za tozo ya miamala ya fedha ya kielektroniki, 2022. | 478O 2022 |
| 15. | Kanuni za Michezo ya Kubahatisha Mtandaoni, 2022. | 478P of 2022 |
| 16. | Kanuni za Ada na Tozo za Nguvu za Atomu, 2022 | 478X of 2022 |
| 17. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za | 480 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| | Mwaka, 2022. | |
| 18. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Meru za Mwaka, 2022. | 481 of 2022 |
| 19. | Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Mazao ya Misitu) Halmashauri ya Wilaya ya Meru za Mwaka, 2022. | 482 of 2022 |
| 20. | Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Meru za Mwaka 2022. | 483 of 2022 |
| 21. | Sheria Ndogo za (Ada ya Vibali vya Ujenzi) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 488 of 2022 |
| 22. | Sheria Ndogo za ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 489 of 2022 |
| 23. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kuegesha Magari (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022. | 490 of 2022 |
| 24. | Sheria Ndogo za ((Kilimo cha Kahawa) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 491 of 2022 |
| 25. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 492 of 2022 |
| 26. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Kodi ya Vibanda vya Biashara (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 493 of 2022 |
| 27. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 494 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 28. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kuegesha Magari (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022. | 490 of 2022 |
| 29. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2022. | 494 of 2022 |
| 30. | Sheria Ndogo za (Afya na Usimamizi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa Ubungo za Mwaka, 2022. | 495 of 2022 |
| 31. | Sheria Ndogo za (Vituo vya Mabasi na Maegesho ya Vyombo vya Moto) Za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka, 2022. | 496 of 2022 |
| 32. | Sheria Ndogo za (Ushuru ya Huduma) za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka, 2022. | 497 of 2022 |
| 33. | Sheria Ndogo za Ada Na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka, 2022. | 498 of 2022 |
| 34. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Maswa za Mwaka, 2022. | 499 of 2022 |
| 35. | Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022. | 503 of 2022 |
| 36. | Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka, 2022. | 504 of 2022 |
| 37. | Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022. | 505 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 38. | Amri ya Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala Katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Marekebisho) ya Mwaka 2022. | 512A of 2022 |
| 39. | Amri ya Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala Katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Marekebisho) ya Mwwaka 2022. | 512B of 2022 |
| 40. | Notisi ya Kutangaza Viwango Vya Hiari ya Mwaka, 2022. | 515 of 2022 |
| 41. | Notisi ya Msamaha wa Kusafirisha Magogo ya Mkurungu (Pterocarpus Tinctorius) ya Mwaka 2022. | 517 of 2022 |
| 42. | Amri ya Kufuta Mamlaka ya Pamoja ya Mahakama ya Wilaya Mpanda Katika Wilaya ya Tanganyika la Mwaka 2022. | 519 of 2022 |
| 43. | Amri ya Kuanzisha Masijala Ndogo za Mahakama ya Rufani ya Tanzania ya Mwaka, 2022. | 520 of 2022 |
| 44. | Tamko la siku ya Sensa ya Watu na Makazi kuwa siku ya Mapumziko la Mwaka 2022 | 521 of 2022 |
| 45. | Amri ya Kutenga Maeneo kwa Ajili ya Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Madini kwa Wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini la Mwaka 2022. | 522 of 2022 |
| 46. | Hati ya Uhamisho wa Viwanja Vilivyosajiliwa kwa Majina ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Kwenda Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 2022. | 523 of 2022 |
| 47. | Notisi ya Msamaha kwa Wamiliki wa Silaha Kinyume cha Sheria ya Mwaka, 2022. | 537 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 48. | Kanuni za Kutoza Ada Kwenye Matumizi ya Kisimbuzi Cha Runinga za Mwaka 2022. | 537A of 2022 |
| 49. | Kanuni za Msamaha wa Riba ya Malimbikizo ya Kodi ya Pango la Ardhi za Mwaka 2022. | 537B of 2022 |
| 50. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2022. | 545 of 2022 |
| 51. | Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2022. | 546 of 2022 |
| 52. | Sheria Ndogo za Ada ya Vibali vya Ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2022. | 547 of 2022 |
| 53. | Sheria Ndogo za Udhibiti wa Mifugo za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2022. | 548 of 2022 |
| 54. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2022. | 545 of 2022 |
| 55. | Kanuni za Madini (Ufifilishaji wa Makosa) za Mwaka 2022. | 549 of 2022 |
| 56. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Erick Benjamini Mahenge ya Mwaka, 2022. | 550 of 2022 |
| 57. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Rashidi Saidi Khalifa (Akifanya Biashara Kama Ksk Filling Station) ya Mwaka, 2022. | 551 of 2022 |
| 58. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Boniphace Maregesi Mwikala ya Mwaka 2022. | 552 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 59. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Panone & Company Limited-Bonite ya Mwaka, 2022. | 553 of 2022 |
| 60. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Washington Jared Benasius (Akifanya Biashara Kama Mukendo Agrovet & General Supply) ya Mwaka, 2022. | 554 of 2022 |
| 61. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Furahisha France Msigwa Singida ya Mwaka, 2022. | 555 of 2022 |
| 62. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Richard Cherd Kafyulilo ya Mwaka 2022. | 556 of 2022 |
| 63. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Emmanuel Wilfred Matsinde ya Mwaka, 2022. | 557 of 2022 |
| 64. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Herryad Malewo ya Mwaka, 2022. | 558 of 2022 |
| 65. | Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka, 2022. | 560 of 2022 |
| 66. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka, 2022. | 561 of 2022 |
| 67. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka, 2022. | 562 of 2022 |
| 68. | Sheria Ndogo za Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka, 2022. | 563 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 69. | Sheria Ndogo za Udhibiti wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka, 2022. | 564 of 2022 |
| 70. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero za Mwaka, 2022. | 565 of 2022 |
| 71. | Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero za Mwaka, 2022. | 566 of 2022 |
| 72. | Sheria Ndogo (Ada Na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero za Mwaka, 2022. | 567 of 2022 |
| 73. | Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga za Mwaka, 2022. | 568 of 2022 |
| 74. | Sheria Ndogo za Kuzuia Upotevu na Uharibifu wa Nafaka Wakati na Baada ya Kuvuna ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga za Mwaka, 2022. | 569 of 2022 |
| 75. | Sheria Ndogo za Kilimo na Hifadhi ya Chakula za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima (Marekebisho) za Mwaka, 2022. | 570 of 2022 |
| 76. | Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima (Marekebisho) za Mwaka, 2022. | 571 of 2022 |
| 77. | Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya Mvomero za Mwaka, 2022. | 572 of 2022 |
| 78. | Kanuni za Kudumu Halmashauri ya Wilaya Msalala (Marekebisho) Mwaka, 2022. | 573 of 2022 |
| 79. | Notisi ya Kuteua Mahali Pa Vikao vya Mahakama Kuu Katika Utekelezaji wa Mamlaka yake ya Awali ya Kijinai ya Mwaka 2022. | 576 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 80. | Notisi ya Uteuzi wa Wachunguzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2022. | 577 of 2022 |
| 81. | Notisi ya Uteuzi wa Wakaguzi wa Magari na Watathmini wa Madereva ya Mwaka 2022. | 578 of 2022 |
| 82. | Hati ya Uanzishwaji wa Daftari la Mawakili wa Serikali ya mwaka 2022. | 583B of 2022 |
| 83. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za Mwaka 2022. | 586 of 2022 |
| 84. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za Mwaka 2022. | 587 of 2022 |
| 85. | Sheria Ndogo za (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za Mwaka 2022. | 588 of 2022 |
| 86. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya Nsimbo za Mwaka 2022. | 589 of 2022 |
| 87. | Sheria Ndogo (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2022. | 590 of 2022 |
| 88. | Sheria Ndogo (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2022. | 591 of 2022 |
| 89. | Sheria Ndogo ya Ushuru Wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2022. | 592 of 2022 |
| 90. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Nsimbo za Mwaka 2022. | 593 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 91. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za Mwaka 2022. | 594 of 2022 |
| 92. | Sheria Ndogo za (Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za Mwaka 2022. | 595 of 2022 |
| 93. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Mlele za Mwaka 2022. | 596 of 2022 |
| 94. | Notisi ya Maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya Wanyama (Maeneo ya Malisho yaliyotengwa, Kupimwa na Kutangazwa) ya Mwaka 2022. | 597 of 2022 |
| 95. | Amri ya Tangazo La Pori La Akiba Pololeti ya Mwaka, 2022. | 604 of 2022 |
| 96. | Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka 2022. | 605 of 2022 |
| 97. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi na Shughuli za Madini ya Vito) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka, 2022. | 606 of 2022 |
| 98. | Sheria Ndogo za (Kilimo Kwanza na Usalama wa Chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka 2022. | 607 of 2022 |
| 99. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Gulio) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka, 2022. | 608 of 2022 |
| 100. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka, 2022. | 609 of 2022 |
| 101. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Mwaka, 2022. | 610 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 102. | Amri ya Mpango wa Jumla wa Eneo la Biashara la Kwala ya Mwaka, 2022. | 633 of 2022 |
| 103. | Kanuni za Uwindaji wa Kujikumu wa Wenyeji za Mwaka, 2022. | 635 of 2022 |
| 104. | Notisi ya Orodha ya Watu Waliosajiliwa, Walioandikishwa au Walioorodheshwa chini ya Sheria ya Famasi ya Mwaka 2022. | 641 of 2022 |
| 105. | Notisi ya Tarehe ya Kuanza Kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022. | 658 of 2022 |
| 106. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Misunkumilo ya Mwaka 2022. | 662 of 2022 |
| 107. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kitisi ya Mwaka 2022. | 663 of 2022 |
| 108. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Mjimwema ya Mwaka 2022. | 664 of 2022 |
| 109. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Uwemba ya Mwaka 2022. | 665 of 2022 |
| 110. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kambarage ya Mwaka 2022. | 666 of 2022 |
| 111. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Sitalike ya Mwaka 2022. | 667 of 2022 |
| 112. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Nsemulwa ya Mwaka 2022. | 668 of 2022 |
| 113. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Magamba ya Mwaka 2022. | 669 of 2022 |
| 114. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kivukoni ya Mwaka 2022. | 670 of 2022 |
| 115. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo La Kawajense ya Mwaka 2022. | 671 of 2022 |
| 116. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Shanwe ya Mwaka 2022. | 672 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 117. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kigamboni ya Mwaka 2022. | 673 of 2022 |
| 118. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Majalila ya Mwaka 2022. | 674 of 2022 |
| 119. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Mtemibeda ya Mwaka 2022. | 675 of 2022 |
| 120. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Sekondari ya Mwaka 2022. | 676 of 2022 |
| 121. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Karema ya Mwaka 2022. | 677 of 2022 |
| 122. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Ikola na Mchangani ya Mwaka 2022. | 678 of 2022 |
| 123. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Ifukutwa ya Mwaka 2022. | 679 of 2022 |
| 124. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Itenka ya Mwaka 2022. | 680 of 2022 |
| 125. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kikula ya mwaka 2022. | 681 of 2022 |
| 126. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Magula ya Mwaka 2022. | 682 of 2022 |
| 127. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Mgendela na Kihesa ya Mwaka 2022. | 683 of 2022 |
| 128. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kasekese ya Mwaka 2022. | 684 of 2022 |
| 129. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Igereke ya Mwaka 2022. | 685 of 2022 |
| 130. | Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Tambuka Reli ya Mwaka 2022. | 686 of 2022 |
| 131. | Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara ya Mwaka 2022. | 687 of 2022 |
| 132. | Amri ya Kupanga Eneo la Uhuru ya Mwaka 2022. | 692 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 133. | Amri ya Kupanga Eneo la Sitalike ya Mwaka 2022. | 693 of 2022 |
| 134. | Amri ya Kupanga Eneo la Matandalani ya Mwaka 2022. | 694 of 2022 |
| 135. | Notisi ya Uteuzi wa Wakaguzi wa Viwango na Udhibiti Usalama na Ubora ya mwaka 2022. | 695 of 2022 |
| 136. | Amri ya Kupanga Eneo la Mtisi ya Mwaka 2022. | 696 of 2022 |
| 137. | Amri ya Kupanga Eneo la Itenka ya Mwaka 2022. | 697 of 2022 |
| 138. | Amri ya Kupanga Eneo la Igagala ya Mwaka 2022. | 698 of 2022 |
| 139. | Amri ya Kupanga Eneo la Igandu, Chibwe na Chimwaga ya Mwaka 2022. | 699 of 2022 |
| 140. | Amri ya Kupanga Eneo la Mwese ya Mwaka 2022. | 700 of 2022 |
| 141. | Amri ya Kupanga Eneo la Loya ya Mwaka 2022. | 701 of 2022 |
| 142. | Amri Ya Kupanga Eneo La Igalula ya Mwaka 2022. | 702 of 2022 |
| 143. | Amri ya Kupanga Eneo la Mabama ya Mwaka 2022. | 703 of 2022 |
| 144. | Amri ya Kupanga Eneo la Tura ya Mwaka 2022. | 704 of 2022 |
| 145. | Amri ya Kupanga Eneo la Kigwa ya mwaka 2022. | 705 of 2022 |
| 146. | Amri ya Kupanga Eneo la Pangale ya Mwaka 2022. | 706 of 2022 |
| 147. | Amri ya Kupanga Eneo la Goweko ya Mwaka 2022. | 707 of 2022 |
| 148. | Amri ya Kupanga Eneo la Kiloleli ya Mwaka 2022. | 708 of 2022 |

| | | |
|---|---|---|
| 149. | Amri ya Kupanga Eneo la Ndogowe, Mlazo na Chiboli ya Mwaka 2022. | 709 of 2022 |
| 150. | Amri ya Kupanga Eneo la Ugansa ya Mwaka 2022. | 710 of 2022 |
| 151. | Amri ya Kupanga Eneo la Membe ya Mwaka 2022. | 711 of 2022 |
| 152. | Amri ya Kupanga Eneo la Tutuo ya Mwaka 2022. | 712 of 2022 |
| 153. | Amri ya Kupanga Eneo La Sibwesa ya Mwaka 2022. | 713 of 2022 |
| 154. | Amri ya Kupanga Eneo la Majalila ya Mwaka 2022. | 714 of 2022 |
| 155. | Amri ya Kupanga Eneo la Karema ya Mwaka 2022. | 715 of 2022 |
| 156. | Amri ya Kupanga Eneo la Ipole ya Mwaka 2022. | 716 of 2022 |
| 157. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa Kampuni ya Eacop ya Mwaka 2022. | 719 of 2022 |
| 158. | Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Vincent Fire Mwamakimbula ya Mwaka 2022. | 720 of 2022 |
| 344. | The Insurance (Vesting of Interests and Regulation) Act | 349 |
| 345. | The International Development Association Act | 350 |
| 346. | The Statistics Act | 351 |
| 347. | The Probate and Administration of Estates Act | 352 |
| 348. | The Education Act | 353 |
| 349. | The Foreign Service Fees and Charges Act | 354 |
| 350. | The Urban Planning Act | 355 |
| 351. | The Diplomatic and Consular Immunities and Privileges Act | 356 |
| 352. | The Tanzania Citizen Act | 357 |
| 353. | The Judicature and Application of Laws Act | 358 |
| 354. | The Investment in Tanganyika Government Securities Act | 359 |
| 355. | The Public Officers (Salaries and Allowances) Act | 360 |
| 356. | The Preventive Detention Act | 361 |
| 357. | The Transfer and Delegation of Powers Act | 362 |
| 358. | The Bretton Woods Agreements Act | 363 |
| 359. | The Tanzania Tourist Board Act | 364 |
| 360. | The Airport Service Charge Act | 365 |
| 361. | The Employment and Labour Relation Act | 366 |
| 362. | The Government Leaseholds (Conversion to Rights of Occupancy) Act | 367 |
| 363. | The Extradition Act | 368 |
| 364. | The Customs (Dumping and subsidies: Rates) Act | 369 |

| | | |
|---|---|---|
| 365. | The Treasury Registrar (Powers and Functions) Act | 370 |

| KIAMBATISHO F<br>SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU KUANZIA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023 | | |
|---|---|---|
| **NA.** | **JINA LA SHERIA** | **SURA** |
| 366. | The Public Service Social Security Fund Act | 371 |
| 367. | The Dodoma Capital City (Declaration) Act | 372 |
| 368. | The Export Processing Zones Act | 373 |
| 369. | The Tax Reserve Certificates Act | 374 |
| 370. | The Islamic Law (Restatement) Act | 375 |
| 371. | The Pyrethrum Act | 376 |
| 372. | The Customary Leaseholds (Enfranchisement) Act | 377 |
| 373. | The Fertilizers Act | 378 |
| 374. | The Tanzania Commission for AIDS Act | 379 |
| 375. | The Deportation Act | 380 |
| 376. | The Exports Control Act | 381 |
| 377. | The District Development Corporation Act | 382 |
| 378. | The Statutory Bodies (Change of Names) Act | 383 |
| 379. | The Traditional Liquor (Control of Distillation) Act | 384 |
| 380. | The Public Order Act | 385 |
| 381. | The National Economic Empowerment Act | 386 |
| 382. | The Transfer of Prisoners Act | 387 |
| 383. | The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act | 388 |
| 384. | The Destitute Persons Act | 389 |
| 385. | The Potable Spirits (Compounding) Act | 390 |
| 386. | The Commission for Human Rights and Good Governance Act | 391 |

| | | |
|---|---|---|
| 387. | The Petroleum Act | 392 |
| 388. | The Freehold Titles (Conversion) and Government Leases Act | 393 |
| 389. | The Insurance Act | 394 |
| 390. | The National Health Insurance Fund Act | 395 |

*KIAMBATISHO F*

**SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU KUANZIA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

| NA. | JINA LA SHERIA | SURA |
|---|---|---|
| 391. | The Local Government Training Institute Act | 396 |
| 392. | The Regions and Districts (Establishment Procedure) Act | 307 |
| 393. | The Public Leadership Code of Ethics Act | 398 |
| 394. | The Tanzania Revenue Authority Act | 399 |
| 395. | The Parole Boards Act | 400 |
| 396. | The Agricultural Imputes Trust Fund Act | 401 |
| 397. | The Eastern Africa Statistical Training Centre Act | 402 |
| 398. | The Custom (Management and Tariff) Act | 403 |
| 399. | The National Bank of Commerce (re-organization and vesting of Assets and Liabilities Act | 404 |
| 400. | The Institute of Judicial Administration Lushoto Act | 405 |
| 401. | The Tanzania Intelligence and Security Service Act | 406 |
| 402. | The Microfinance Act | 407 |
| 403. | The Tax Revenue Appeals Act | 408 |
| 404. | The Community Health Fund Act | 409 |
| 405. | The Public Procurement Act | 410 |
| 406. | The Treaty for the Establishment of the East African Community Act | 411 |

| | | |
|---|---|---|
| 407. | The Education Fund Act | 412 |
| 408. | The Land Transport Regulatory Authority Act | 413 |
| 409. | The Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act | 414 |
| 410. | The Tanzania Shipping Agencies Act | 415 |
| 411. | The Unit Titles Act | 416 |
| 412. | The Financial Leasing Act | 417 |
| 413. | The Public Audit Act | 418 |

***KIAMBATISHO F***

**SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU KUANZIA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

| NA. | JINA LA SHERIA | SURA |
|---|---|---|
| 414. | The National Leader's Funeral Act | 419 |
| 415. | The Special Economic Zones Act | 420 |
| 416. | The meat Industry Act | 421 |
| 417. | The Universal Communications Services Access Act | 422 |
| 418. | The Anti-money Laundering Act | 423 |
| 419. | The Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act | 424 |
| 420. | The Law School of Tanzania Act | 425 |
| 421. | The Town Planners (Registration) Act. | 426 |
| 422. | The Fire and Rescue Force Act | 427 |
| 423. | The Environmental Health Practitioners (Registration) Act | 428 |
| 424. | The Medical Radiology and Imaging Professionals Act | 429 |
| 425. | The National Prosecutions Service Act | 430 |
| 426. | The HIV and AIDS (Prevention and control) Act. | 431 |
| 427. | The Anti-Trafficking in persons Act | 432 |
| 428. | The UNESCO National Commission Act. | 433 |

| | | |
|---|---|---|
| 429. | The Tanzania Livestock Research Institute Act. | 434 |
| 430. | The National Irrigation Act. | 435 |
| 431. | The Non-citizens (Employment Regulation Act. | 436 |
| 432. | The National Payment System Act. | 437 |
| 433. | Tax Administration Act. | 438 |
| 434. | The Budget Act. | 439 |
| 435. | The Referendum Act. | 440 |
| 436. | The National Youth Council Act. | 441 |
| 437. | The Electronic Transactions Act. | 442 |
| 438. | The Cybercrimes Act. | 443 |
| 439. | The One Stop Border Posts Act. | 444 |

***KIAMBATISHO F***

**SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU KUANZIA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

| NA. | JINA LA SHERIA | SURA |
|---|---|---|
| 440. | The Commodity Exchange Act. | 445 |
| 441. | The Whistleblower and Witness Protection Act. | 446 |
| 442. | The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act. | 447 |
| 443. | The Teacher s' Service Commission Act. | 448 |
| 444. | The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act. | 449 |
| 445. | The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act. | 450 |

## TAARIFA YA MAGEREZA NA VITUO VYA POLISI VILIVYOTEMBELEWA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023

| SN | Mkoa | Magereza | | Vituo vya Polisi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyote mbelewa | Idadi ya Mahabusi Walioachiwa | Yaliyote mbelewa | Idadi ya Mahabusi Walioachiwa |
| | | | | | |
| 1 | Arusha | 1 | 0 | 9 | 8 |
| 2 | Dar es Salaam | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 3 | Ilala | 1 | 0 | 4 | 0 |
| 4 | Kinondoni | 2 | 16 | 13 | 7 |
| 5 | Temeke | 2 | 3 | 7 | 8 |
| 6 | Dodoma | 4 | 10 | 3 | 6 |
| 7 | Geita | 2 | 29 | 10 | 5 |
| 8 | Iringa | 4 | 9 | 11 | 6 |
| 9 | Kagera | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | Katavi | 1 | 13 | 4 | 0 |
| 11 | Kigoma | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 | Kilimanjaro | 4 | 0 | 5 | 0 |
| 13 | Lindi | 5 | 30 | 5 | 46 |
| 14 | Manyara | 3 | 18 | 5 | 6 |
| 15 | Mara | 3 | 0 | 3 | 0 |
| 16 | Mbeya | 3 | 3 | 3 | 0 |
| 17 | Morogoro | 2 | 31 | 4 | 0 |
| 18 | Mtwara | 1 | 2 | 3 | 10 |
| 19 | Mwanza | 5 | 6 | 10 | 10 |
| 20 | Njombe | 3 | 0 | 10 | 0 |
| 21 | Pwani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 22 | Rukwa | 1 | 17 | 9 | 17 |
| 23 | Ruvuma | 5 | 0 | 1 | 0 |
| 24 | Shinyanga | 2 | 0 | 11 | 7 |
| 25 | Simiyu | 1 | 0 | 1 | 1 |
| 26 | Singida | 2 | 0 | 3 | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 27 | Songwe | 1 | 1 | 0 | 0 |
| 28 | Tabora | 3 | 1 | 3 | 5 |
| 29 | Tanga | 2 | 2 | 2 | 0 |
| 30 | Tarime | 0 | 0 | 1 | 0 |
| | **Jumla** | **63** | **191** | **140** | **142** |

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha hoja yako na imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria ili aweze kuja kuwasilisha taarifa yake. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utawala Katiba na Sheria naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Jalali Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kutujalia uhai na uzima na kutujalia Ramadhan na sikukuu yake kwenda kwa salama na amani. Tumwombe Mwenyezi Mungu atujalie Ramadhan nyingine tuwe wazima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa uchambuzi; Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6(2)(d) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawanda ya Uchambuzi; Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni yafuatayo: -

i. Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria,

ii. Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama,

iii. Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

iv. Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,

v. Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,

vi. Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na

vii. Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi na makusanyo ya maduhuli; Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kukusanya jumla ya shilingi 105,002,000. Kati ya fedha hizo Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya shilingi milioni 45, Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya shilingi milioni 60, na Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ililenga kukusanya shilingi elfu mbili (2000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

i. Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) hadi kufikia mwezi Februari, 2023 imekusanya kiasi cha shilingi 18,020,000 sawa na asilimia 40 ya lengo la Makusanyo. Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili haujafika lengo kwa kuwa Wizara imeondoa tozo za usajili kwenye vyeti vya kuzaliwa kwa watoto na vyeti vya vifo.

ii. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (Fungu 35) hadi kufikia mwezi Februari, 2023 imekusanya kiasi cha shilingi 56,400,000 sawa na asilimia 94 ya lengo la Makusanyo.

iii. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) ililenga kukusanya shilingi elfu mbili (2000). Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili halikukusanya kiasi chochote. Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea mauzo ya vitabu vya zabuni ambapo hadi kufikia Februari, 2023 hapakuwa na mauzo ya vitabu vya zabuni yaliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 74,420,000 sawa na asilimia 70 ya lengo. Mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli kwa kila

Fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2023 unaonekana katika Jedwali Namba. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matumizi ya bajeti, Fungu Na. 41 – Wizara ya Katiba na Sheria; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 27,239,369,000, kati ya fedha hizo shilingi 14,512,799,000 ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo bilioni 7.6 ni mishahara na bilioni 6.8 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, bilioni 12.7 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo bilioni 5.1ni fedha za ndani kwa ajili ya kujenga mfumo wa kutoa haki kwa njia ya mtandao *(e-justice)* na mfumo wa upatikanaji wa haki nchini kwa shilingi bilioni 7.6 ni fedha za nje kwa ajili ya programu ya ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (*BSAAT*), Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji wa Haki *(IMPACT)* na kuendeleza programu ya wanawake na wasichana kupata haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya bilioni 15.2 sawa asilimia 56. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.6 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 3.6 sawa na asilimia 52.6 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni nne sawa na asilimia 52 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 7.6 sawa na asilimia takribani 60 zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo bilioni 1.7 ni fedha za ndani na bilioni 5.8 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha pungufu katika Wizara hii kulitokana na kutokuajiriwa kwa watumishi wapya waliopangwa kuajiriwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Mahakama, hakukuwa na jambo la msingi; nitakwenda kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 14.3. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 9.8 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 2.9 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 6.9 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha shilingi bilioni 4.5 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya ujenzi wa kituo jumuishi cha taasisi za kiesheria mkoani Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya shilingi bilioni 6.4 sawa na asilimia 45.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.7 ilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 3.4 sawa na asilimia 50 ilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.2 sawa na asilimia 76.8 ilipokelewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, milioni 747 sawa na asilimia 16.6 tu ilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi milioni 633 zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha taasisi za kisheria katika Mkoa wa Mwanza na shilingi milioni 114.3 zilipokelewa kwa ajili ya Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania *(BSAAT)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha za maendeleo pungufu ya jengo kulitokana na mkandarasi kutowasilisha kwa wakati hati za malipo kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la taasisi za kisheria mkoani Mwanza na kuchelewa kuanza kazi ya ujenzi wa jengo la taasisi za kisheria katika mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.4 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na bilioni 3.3 zilitengwa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya shilingi bilioni 7.6 sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia takribani 60 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na bilioni 1.9 sawa na asilimia 60 vilevile zilipokelewa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ilielezwa kuwa sababu ya kupokea fedha pungufu ya wastani wa asilimia 66.6 hadi kufikia Februari, 2023 kulitokana na kuchelewa kupokelewa kwa watumishi wapya waliotarajiwa kufika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 45.2. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 36.6 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi Bilioni 22.1 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi Biioni 14.5 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, Shilingi Bilioni 8.6 ilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi Bilioni 8.0 ni fedha za ndani na Shilingi Milioni 630 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, Ofisi hii ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni 27.4, sawa na asilimia 60.6 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 22.9, sawa na asilimia 62.6 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Shilingi Bilioni 16.1, sawa na asilimia 72.8 zilipokelewa

kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Bilioni 6.8 sawa na asilimia 47.2 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, Shilingi Bilioni 4.4 ya fedha za ndani, sawa na asilimia 51.8 zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2023 hakukuwa na fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa sababu iliyopelekea fungu hili kupokea bajeti ya maendeleo chini ya wastani wa asilimia 66.6 hadi kufikia Februari, 2023, ni kunatokana na mkandarasi wa Jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka lililopo Mkoani Shinyanga kutokuwasilisha hati za malipo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 6.5. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6.3 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi bilioni 4.1 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 2.29 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi milioni 115, fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, Tume ilipokea jumla ya shilingi bilioni 3.8, sawa na asilimia 59.5 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.2, sawa na asilimia 53.7 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 1.6, sawa na takribani asilimia 70 zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara. Aidha, hakukuwa na fedha iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha pungufu katika Fungu hili kulitokana na kuhama kwa baadhi ya watumishi na kutopokelewa kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3.4. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.7 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 730 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara. Aidha, Tume haikuwa na bajeti kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, Tume ilipokea jumla ya shilingi 2,043,000,000, sawa na asilimia 59 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 482,274,000 sawa na asilimia 66 zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 57.3 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchanganuo wa fedha hizo kwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3 kwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2022/2023; Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 25,971,570,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mkoa wa Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga; Mkataba wa ujenzi wa Mradi huu ulisainiwa Mwezi Novemba, 2022 na unatakiwa kukamilika ifikapo Mwezi Juni, 2023 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.1. Hadi mwezi Machi, 2023, mradi ulikuwa umetekelezwa kwa asilimia 35 na muda wa mkataba umebakia miezi minne. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa mradi huo umechelewa kwa asilimia 15, sawa na muda wa mwezi mmoja. Aidha, malipo yaliyokuwa

yamekwishafanyika ni Shilingi Milioni 323, sawa na asilimia 15 tu ya gharama za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati inashauri Serikali ihakikishe inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika katika muda uliopangwa na ikibidi kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kukata gharama za ucheleweshaji *(liquidated damages)* ikiwa mradi utachelewa kukamilika katika muda wa mkataba kwa uzembe wa Mkandarasi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kufanya malipo kwa wakati mara tu baada ya kupokea hati ya malipo ili kuwezesha utekelezaji wa mradi kukamilika katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria - Buswelu, Ilemela - Mwanza (Namba ya Mradi 6389). Mradi unatekelezwa kwa Mkataba wa miezi 18 kuanzia Aprili, 2022 hadi Oktoba, 2023 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.1. Hadi kufikia Machi, 2023 utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 45 na kupelekea mradi kuchelewa kwa siku 30. Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi ni uwepo wa mawe yaliyobainika wakati wa kuchimba msingi jambo lililopelekea kutumia muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mkandarasi kubainisha kuwa atakuwa na ratiba za ujenzi wakati wa usiku ili kufidia muda uliopotea, Kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika katika muda uliopangwa na kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kukata gharama za ucheleweshaji (*liquidated damages*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Namba ya Mradi 6314. Kazi ya kutekeleza mradi ilianza Juni, 2021 na kukamilika Septemba, 2022. Kukamilika kwa mradi huo kumewezesha kuboreshwa kwa jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Tabora. Jengo hilo kwa sasa linatumika kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu likiwa na miundombinu ya kisasa ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na utekelezaji pamoja na matumizi ya mradi husika. Aidha, uboreshaji wa jengo hilo utapelekea jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Tabora lililojengwa mwaka 1963 kuendelea kutumika katika kipindi kirefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa malipo ya utekelezaji wa mradi huu yalikuwa yamefanyika kwa 61% tu licha ya mradi kukamilika. Kamati inashauri malipo ya utekelezaji wa kazi husika yafanyike kwa wakati ili kuiepusha hasara zinazoweza kujitokeza. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuboreshaji majengo mengine ya mahakama ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za kimahakama na kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii. Kwa sehemu kubwa, utekelezaji wake umekuwa wa kuridhisha katika mafungu yote isipokuwa Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, mfano wa maoni ambayo hayakufanyiwa kazi na Tume hiyo ni yafuatayo:-

(a) Tume kufanya uchunguzi wa mambo yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu na kutoa mrejesho wa ripoti za kiuchunguzi pale inapostahili ili kukemea vitendo viovu na kuboresha misingi ya utawala bora nchini; na

(b) Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya Sheria na kuainisha Sheria zinazokinzana na sheria zinazotoa haki za binadamu na kuzifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki ambapo kumekua na ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili nchini, Kamati inashauri Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kufanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha inakuwa kimbilio la kwanza kwa wananchi waliothirika na vitendo vya ukatili hususani wananchi wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu; Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; Maduhuli; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 105,002,000. Kiasi hiki kitatokana na makusanyo ya shilingi 45,000,000 kutoka Fungu 41, shilingi 60,000,000 kutoka Fungu 35 na shilingi 2,000 kutoka Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu. Kiasi hiki ni sawa kabisa na kiasi kilichopangwa mwaka 2022/2023 kama inavyobainishwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa Wizara na taasisi zake kwa kawaida msingi wa kazi zake ni kutoa huduma kwa taasisi za Serikali na usaidizi kwa jamii, jambo ambalo halitegemewi kukawa na maduhuli makubwa yanayoweza kukusanywa na baadhi ya taasisi kutokuwa na maduhuli yoyote. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kukosekana kwa maduhuli kwa baadhi ya Ofisi huenda kunatokana na Ofisi hizo

kushindwa kubuni vyanzo vya mapato ambavyo vingeendana na kazi za ofisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla shilingi 140,764,214,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 34,236,366,000 ni Mishahara na shilingi 106,527,848,000 ni Matumizi Mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 6

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa shilingi 53,943,330,000, sawa na asilimia 62.13 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo bajeti ya Matumizi ya Kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa shilingi 86,820,884,000. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze watumishi kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria, hususani Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Sababu nyingine ni Wizara kuweka bajeti ya kuanza mchakato wa Katiba mpya ikiwa ndio ni kipambele chake cha kwanza kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaarifiwa kuwa, watumishi wapya 47 wameajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watumishi 354 katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na watumishi 44 katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ongezeko hilo pamoja na uwepo wa kazi nyingine mpya ikiwemo kazi ya kuratibu mchakato wa Katiba mpya linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi na kuongezeka kwa mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na Serikali yake kwa ujumla kwa kuajiri watumishi wapya wengi katika taasisi chini ya Wizara hii. Mathalani, Kamati ilielezwa kuwa, waajiriwa wapya 354 katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni ongezeko kubwa zaidi lililofanyika kwa muda wa miezi tisa tu na halijawahi kutokea katika kipindi chochote cha Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa watumishi wapya kumepunguza kwa kiasi upungufu uliokuwa umekithiri wa watumishi kwenye baadhi ya taasisi. Aidha, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kutawezesha kuanzishwa kwa Ofisi mpya katika wilaya 50 ambazo hazikuwa na Ofisi hii na hivyo kufanya Ofisi hiyo kuwa na Ofisi katika wilaya 94 nchini na kubakia wilaya 45 pekee**.**

*Mjesjimiwa Mwenyekiti,* aidha, Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo limepelekea mahitaji makubwa ya vyumba vya Ofisi kwenye baadhi ya wilaya jambo linaloweza kupelekea Ofisi kuwekwa katika vyumba vya kupanga. Pia kumepelekea mahitaji makubwa ya vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa watumishi, vielelezo na nyaraka nyingine muhimu. Kwa sababu hii, Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi na haraka za kuandaa Ofisi katika wilaya zote ambako Ofisi mpya zimeanzishwa pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi muhimu.

*Mjesjimiwa Mwenyekiti,* Miradi ya Maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.24,876,800,000 kwa ajili ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 13.1 ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni 11.7 ni fedha za nje.

*Mjesjimiwa Mwenyekiti,* bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, imepungua kwa Shilingi Bilioni

1,094,770,000 sawa na asilimia 4.2 ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Sababu ya kupungua huku kunatokana na miradi mingi iliyopangwa kwenda kutekelezwa kwa mwaka 2023/2024, tayari ipo katika hatua za utekelezaji kutoka mwaka 2022/2023 kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani na inaendelea kuishauri Serikali kuzidi kupunguza matumizi ya fedha za nje kadri itakavyowezekana. Aidha, Kamati…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nenda kwenye hitimisho.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba dakika mbili tatu nizungumzie Maoni na Ushauri wa Kamati kwa haraka, halafu nihitimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ibuni njia za kuongeza maduhuli kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuongeza kiwango cha makusanyo katika Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake;

(ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Bajeti kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha Ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi;

(iii) Serikali iongeze vipindi vya elimu ya Sheria kwa umma ili kuwawezesha wananchi kutambua wajibu na haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na wewe mwenyewe kwa Uongozi wenu na kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Damasi Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi mkubwa pamoja na ushirikiano wa hali ya juu alioupatia Kamati hii wakati ikitekeleza majukumu yake. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kumsaidia vyema Waziri kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kwa ushirikiano alioipatia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Mary Gaspar Makondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na

taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Mary Gaspar Makondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndugu Praisegod Lukio na Ndugu Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**25 APRILI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha Msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

c) Sehemu ya tatu inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

d) Sehemu ya nne ni Hitimisho.

1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6(2)(d) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni: -

a) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
b) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
c) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
d) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
e) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
f) **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na
g) **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo;-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Katiba na Sheria; na
(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kukusanya jumla ya **Sh. 105,002,000.** Kati ya fedha hizo **Fungu 41**- Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya **Sh. 45,000,000, Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya **Sh. 60,000,000** na **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ililenga kukusanya **Sh. 2000**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo:-

(a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria hadi kufikia mwezi Februari, 2023 imekusanya kiasi cha **Sh. 18,020,000** sawa na **asilimia 40** ya lengo la Makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili haujafika lengo kwa kuwa Wizara

imeondoa tozo za usajili kwenye vyeti vya kuzaliwa kwa watoto na vyeti vya vifo.

(b) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hadi kufikia mwezi Februari, 2023 imekusanya kiasi cha **Sh. 56,400,000** sawa na **asilimia 94** ya lengo la Makusanyo.

(c) **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ililenga kukusanya **Sh. 2000** hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili halikukusanya kiasi chochote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea mauzo ya vitabu vya zabuni. Hadi kufikia Februari, 2023 hapakuwa na mauzo ya vitabu vya zabuni yaliofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2023, Wizara ilikusanya jumla ya **Sh. 74,420,000** sawa na **asilimia 70.87** ya lengo. Mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli kwa kila Fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2023 unaonekana katika **Jedwali Namba. 1**.

**Jedwali Na. 1-**Mchanganuo wa maduhuli kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023

| FUNGU | KIASI KILICHOIDHINISHWA 2022/2023 | KIASI KILICHOKUSANYWA JULAI 2022-FEB.2023 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| Fungu 35-Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 56,400,000 | 94 |
| Fungu 41-Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 18,020,000 | 40 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Fungu 55-Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **105,002,000** | **74,420,000** | **70.87** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023*
*Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

**2.3.1 Fungu Na. 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 27,239,369,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 14,512,799,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 7,647,528,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 6,865,271,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 12,726,570,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Sh. 5,110,800,000** ni fedha za ndani kwa ajili ya kujenga mfumo wa Kutoa haki kwa njia ya mtandao *(e-justice)* na mfumo wa upatinaji wa haki nchini na **Sh. 7,615,770,000** ni fedha za nje kwa ajili ya programu ya ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (*BSAAT*), Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji wa Haki *(IMPACT)* na kuendeleza programu ya wanawake na wasichana kupata haki nchini.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 15,265,382,921.12** sawa **asilimia 56**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 7,632,691,462.56** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 3,614,648,475 sawa na asilimia 52.65** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 4,018,042,987.56** sawa na **asilimia 52.54** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 7,632,691,458.56** sawa na **asilimia 59.97** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo

**Sh. 1,793,501,646.63** ni fedha za ndani na **Sh. 5,839,189,811.93** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha pungufu katika Wizara hii kulitokana na kutokuajiriwa kwa watumishi wapya waliopangwa kuajiriwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**2.3.2** Fungu Na. 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Tume hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,161,128,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Sh. 2,700,000,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 461,128,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara(PE). Hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Tume ilipokea jumla ya **Sh 1,511,648,060** sawa na **asilimia 48** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,165,502,500** sawa na **asilimia 43.16** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 346,145,560** sawa na **asilimia 75** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE).

**2.3.3** Fungu Na. 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 14,371,341,000.** Kati ya fedha hizo **Sh. 9,871,341,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 2,928,360,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 6,942,981,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha **Sh.4,500,000,000** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya ujenzi wa kituo jumuishi cha taasisi za kiesheria mkoani Mwanza na Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 6,497,766,420.3** sawa na **asilimia 45.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 5,749,896,696.30** ilipokelewa kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 3,498,739,108.30** sawa na **asilimia 50.39** ilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 2,251,157,588** sawa na **asilimia 76.87** ilipokelewa kwa ajili ya Mishaharana (PE). Aidha, **Sh. 747,869,724** sawa na **asilimia 16.6** tu ilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Sh. 633,491,677.27** zilipokelewa kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria katika Mkoa wa Mwanza na **Sh. 114,378,047.04** zilipokelewa kwa ajili ya Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania *(BSAAT)*.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha za maendeleo pungufu ya lengo kulitokana na mkandarasi kutokuwasilisha kwa wakati hati za malipo kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la taasisi za kisheria mkoani Mwanza na kuchelewa kuanza kazi ya ujenzi wa jengo la taasisi za kisheria katika mkoa wa Arusha.

**2.3.4** Fungu Na. 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 12,812,816,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 9,473,018,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 3,339,798,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 7,668,306,719.62** sawa na **asilimia 59** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 5,673,759,719.62** sawa na **asilimia 59.89** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 1,994,547,000** sawa na **asilimia 59.7** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa sababu ya kupokea fedha pungufu ya wastani wa asilimia 66.6 hadi kufikia Februari, 2023 kulitokana na kuchelewa kupokelewa kwa watumishi

wapya waliotarajiwa kufika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**2.3.5** Fungu Na. 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 45,262,695,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 36,617,695,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 22,068,944,000** zilitengwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 14,548,751,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE)**.** Aidha, **Sh. 8,630,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Sh. 8,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 630,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hii ilipokea jumla ya **Sh. 27,464,835,923.83** sawa na **asilimia 60.6** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 22,934,669,491.56** sawa na **asilimia 62.6** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 16,066,779,099.96** sawa na **asilimia 72.8** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 6,867,890,391.60** sawa na **asilimia 47.2** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 4,473,766,432.27** ya fedha za ndani sawa na **asilimia 51.8** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2023 hakukuwa na fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa sababu iliopelekea fungu hili kupokea bajeti ya maendeleo chini ya wastani wa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2023 ni kunatokana na mkandarasi wa jengo la ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliopo Mkoani Shinyanga kutokuwasilisha hati za malipo kwa wakati.

**2.3.6** Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya Sh. **6,505,776,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 6,390,776,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 4,098,680,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 2,292,096,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 115,000,000** fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Tume ilipokea jumla ya **Sh. 3,806,064,052.56** sawa na asilimia **59.5** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 2,202,297,646.56** sawa na **asilimia 53.7** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 1,603,766,406** sawa na **asilimia 69.96** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, hakukuwa na fedha iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa kupokelewa kwa fedha pungufu katika fungu hili kulitokana na kuhama kwa baadhi ya watumishi na kutokupokelewa kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo.

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,454,329,000**. Kati ya fedha hizo Sh. **2,724,009,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 730,320,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, Tume haikuwa na bajeti kwa ajili ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Tume ilipokea jumla ya **Sh. 2,043,862,987.50** sawa na **asilimia 59** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 482,274,000** sawa na **asilimia 66** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara (PE) na **Sh.**

**1,561,588,987.50** sawa na **asilimia 57.3** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3** kwa bajeti ya Matumizi ya kawaida na maendeleo mtawalia.

**JEDWALI NA.2** – Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2022/2023

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria | 14,512,799,000 | 7,632,691,462.56 | 52.59 |
| **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 3,161,128,000 | 1,511,648,060 | 48 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 9,871,341,000 | 5,749,896,696.3 | 58.3 |
| **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 12,812,816,000 | 7,668,306,719.62 | 59.8 |
| **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 36,617,695,000 | 22,934,669,491.56 | 83.5 |
| **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 6,390,776,000 | 3,806,064,052.56 | 59.5 |
| **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria | 3,454,329,000 | 2,043,862,987.50 | 59 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **86,820,884,000** | **51,347,139,470.1** | **59.1** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

**JEDWALI NA. 3** – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2022/2023

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria | 12,726,570,000 | 7,632,691,458.56 | 59.97 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,500,000,000 | 747,869,724 | 16.6 |
| **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 8,630,000,000 | 4,473,766,432.27 | 51.8 |
| **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 115,000,000 | 0.00 | 0.00 |
| **JUMLA KUU** | **25,971,570,000** | **12,854,327,614.83** | **49.49** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya **Sh 25,971,570,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na. 4.

**JEDWALI NA. 4** – Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha 2022/2023

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|
| **Fungu 41 –** Wizara ya Katiba na Sheria | **NA. 5502:** Programu ya ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) | 730,000,000 |
| | **NA.6517:** Miradi inayosifadhiliwa na UNICEF ikiwemo usajili wa Watoto na miradi ya ulinzi kwa watoto | 1,914,000,000 |
| | **NA 6201:** Mfumo wa haki mtandao (e-justice) | 2,550,000,000 |
| | **Na. 6207:** Mfumo wa kuboresha uwajibikaji kupitia mapambano dhidi ya Rushwa na uongezekaji wa fursa za kupata haki– (IMPACT) | 1,400,000,000 |
| | **Na. 5507:** Mfumo wa fursa za kupata haki kwa wanawake na Wasichana nchini | 3,921,770,000 |

| | | |
|---|---|---|
| | **NA 5508:** Mradi wa fursa za kupata haki kwa ajili ya maendeleo endelevu Nchini | 2,210,800,000 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | **NA 6389** – Ujenzi wa vituo jumuishi wa taasisi za kisheria za Serikali Mwanza na Arusha | 4,000,000,000 |
| | **NA 6210** -Programu ya ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) | 500,000,000 |
| **Fungu 35 –** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | **NA 6389:** Ujenzi wa Ofisi katika mikoa mbalimbali | 8,000,000,000 |
| | **NA 6210 -**Programu ya ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) | 600,000,000 |
| | **NA.6517:** Miradi inayofadhiliwa na UNICEF ikiwemo usajili wa Watoto na miradi ya ulinzi kwa Watoto | 30,000,000 |
| **Fungu 55 –** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | **NA.6517:** Miradi inayofadhiliwa na UNICEF ikilenga kuangalia haki za Watoto na biashara | 115,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **25,971,570,000** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii pamoja na taasisi

zake iliyofanyika mwezi machi, 2023, Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi minne. Uchambuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**2.4.1** Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) Mkoa wa Shinyanga-Manispaa ya Shinyanga (Namba ya Mradi 6389).

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa ujenzi wa mradi huu ulisainiwa Mwezi Novemba, 2022 na unatakiwa kukamilika ifikapo Mwezi Juni, 2023 kwa gharama ya **Sh. 2,100,000,000**. Hadi mwezi Machi, 2023, mradi ulikuwa umetekelezwa kwa asilimia thelathini na tano **(35%)** na muda wa mkataba umebakia miezi minne. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa utekelezaji wa mradi huo umechelewa kwa asilimia kumi na tano **(15%)** sawa na muda wa mwezi mmoja. Aidha, malipo yaliyokuwa yamekwishafanyika ni **Sh.323,000,000** sawa na asilimia kumi na tano **(15%)** tu ya gharama za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati inashauri Serikali ihakikishe inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika katika muda uliopangwa na ikibidi kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kukata gharama za ucheleweshaji (*liquidated damages*) ikiwa mradi utachelewa kukamilika katika muda wa mkataba kwa uzembe wa mkandarasi. Aidha, kamati inashauri Serikali kufanya malipo kwa wakati mara tu baada ya kupokea hati ya malipo ili kuwezesha utekelezaji wa mradi kukamilika katika muda uliopangwa.

**2.4.2** Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria - Buswelu, Ilemela- Mwanza (Namba ya Mradi 6389).

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kwa Mkataba wa miezi kumi na nane (18) kuanzia Aprili, 2022 hadi Oktoba, 2023 kwa

gharama ya **Sh. 3,181,548,096.83**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 45** na kupelekea mradi kuchelewa kwa siku thelathini (30). Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi ni uwepo wa mawe yaliyobainika wakati wa kuchimba msingi jambo lililopelekea kutumia muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya mkandarasi kubainisha kuwa atakuwa na ratiba za ujenzi wakati wa usiku ili kufidia muda uliopotea, Kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi na sababu hizo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika katika muda uliopangwa na kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kukata gharama za ucheleweshaji (*liquidated damages*) ikiwa mradi utachelewa kukamilika katika muda wa mkataba.

**2.4.3** Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Tabora - Tabora (Namba ya Mradi 6314).

**Mheshimiwa Spika,** Kazi ya kutekeleza mradi ilianza Juni, 2021 na kukamilika Septemba, 2022. Kukamilika kwa mradi huo kumewezesha kuboreshwa kwa jengo la mahakama kuu kanda ya Tabora. Jengo hilo kwa sasa linatumika kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu likiwa na miundombinu ya kisasa ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na utekelezaji pamoja na matumizi ya mradi husika. Aidha, uboreshaji wa jengo hilo utapelekea jengo la Mahakama Kuu kanda ya Tabora lililojengwa mwaka 1963 kuendelea kutumika katika kipindi kirefu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa malipo ya utekelezaji wa mradi huu yalikuwa yamefanyika kwa asilimia sitini na moja

(61%) tu licha ya mradi kukamilika. Kamati inashauri malipo ya utekelezaji wa kazi husika yafanyike kwa wakati ili kuiepusha hasara zinazoweza kujitokeza. Aidha, kamati inashauri Serikali kuendelea kuboreshaji majengo mengine ya mahakama ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za kimahakama na kudumu kwa muda mrefu.

**2.4.4** Mradi wa Ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Kutoa Haki (Integrated Justice Centre-IJC) - Buswelu, Ilemela-Mwanza (Namba ya Mradi 6389).

***Mheshimiwa Spika*****,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo moja lenye Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama maalum ya Watoto, Mahakama Kuu, mahabusu maalum ya Watoto na mahabusu za kisasa za watu wazima. Pia jengo lina vyumba maalum kwa ajili ya kunyonyesha, miundombinu mingine muhimu kwa ajili ya mahakama na wadau wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa kazi ya ujenzi wa Kituo hicho ilianza mwezi Januari, 2020 hadi Mwezi Februari, 2022. Kamati iliridhika na ubora wa ujenzi. Aidha, kamati inaipongeza mahakama kwa kutumia fedha za ndani kuchimba kisima cha maji kwa ajili ya kuhudumia jengo na kupunguza gharama za maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Serikali juu ya ujenzi wa jengo zuri na lenye hadhi kwa ajili ya huduma za mahakama. Aidha, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa jengo hili pamoja na majengo yote maalum ya mahakama yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa ili yaendelee kuwa na ubora uliopo na kudumu kwa muda mrefu.

2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii. Kwa sehemu kubwa, utekelezaji wake umekuwa wa kuridhisha katika mafungu yote isipokuwa **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, mfano wa maoni ambayo hayakufanyiwa kazi na Tume hiyo ni; -

(c) Tume kufanya uchunguzi wa mambo yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu na kutoa mrejesho wa ripoti za kiuchunguzi pale inapostahili ili kukemea vitendo viovu na kuboresha misingi ya utawala bora nchini na Tume kushirikiana

(d) b) Tume ya Kurekebisha sheria kufanya mapitio ya sheria na kuainisha sheria zinazokinzana na sheria zinazotoa haki za binadamu na kuzifanyia marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki ambapo kumekua na ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili nchini, kamati inashauri Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora kufanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha inakuwa kimbilio la kwanza kwa wananchi waliothirika na vitendo vya ukatili hususani wananchi wanyonge.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla jumla ya **Sh. 105,002,000.** Kiasi hiki kitatokana na makusanyo ya **Sh. 45,000,000** kutoka **Fungu 41-** Wizara ya Katiba na Sheria**, Sh. 60,000,000** kutoka **Fungu 35-** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na **Sh. 2000** kutoka **Fungu 55**-Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kiasi hiki ni sawa kabisa na kiasi kilichopangwa mwaka 2022/2023 kama unavyobainishwa katika Jedwali Na. 5.

**JEDWALI Na.5** – Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024

| FUNGU | KIASI KILICHOIDHINISHWA 2022/2023 | KIASI KILICHOIDHINISHWA 2023/2024 | ASILIMIA YA ULINGANISHO KATI YA 2022/23 NA 2023/24 |
|---|---|---|---|
| **Fungu 35**-Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 60,00,000 | 100 |
| **Fungu 41**-Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 45,000,000 | 100 |
| **Fungu 55** -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 | 2000 | 100 |
| **JUMLA** | **105,002,000** | **105,002,000** | **100** |

***Chanzo****: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

***Mheshimiwa Spika***, Kamati ilielezwa kuwa Wizara na taasisi zake kwa kawaida msingi wa kazi zake ni kutoa huduma kwa taasisi za Serikali na usaidizi kwa jamii, jambo ambalo halitegemewi kukawa na maduhuli makubwa yanayoweza kukusanywa na baadhi ya taasisi kutokuwa na maduhuli yoyote. Hata hivyo, kamati ina maoni kuwa kukosekana kwa maduhuli kwa baadhi ya ofisi huenda kunatokana na ofisi hizo kushindwa kubuni vyanzo vya mapato ambavyo vingeendana na kazi za ofisi husika.

3.2 Matumizi ya Kawaida

***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla **Sh. 140,764,214,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 34,236,366,000** ni mishahara, na

**Sh. 106,527,848,000** ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 6

**JEDWALI NA. 6**– Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2023/2024

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41 –** Wizara ya Katiba na Sheria | 7,234,664,000 | 19,208,535,000 | 26,443,199,000 |
| **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 734,606,000 | 4,861,300,000 | 5,595,906,000 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,072,737,000 | 12,290,130,000 | 16,362,867,000 |
| **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 3,629,161,000 | 13,446,669,000 | 17,075,830,000 |
| **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 14,766,538,000 | 47,172,391,000 | 61,938,929,000 |
| **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,847,924,000 | 5,303,614,000 | 8,151,538,000 |
| **Fungu 59** – Tume ya | 950,736,000 | 4,245,209,000 | 5,195,945,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kurekebisha Sheria | | | |
| **JUMLA KUU** | **34,236,366,000** | **106,527,848,000** | **140,764,214,000** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **Sh. 53,943,330,000** sawa na **asilimia 62.13** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 86,820,884,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze watumishi kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria, hususani Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Sababu nyingine ni Wizara kuweka bajeti ya kuanza mchakato wa Katiba mpya ikiwa ndio ni kipaombele chake cha kwanza kwa mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilitaarifiwa kuwa, watumishi wapya **47** wameajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, **354** katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na 44 katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ongezeko hilo pamoja na uwepo wa kazi nyingine mpya ikiwemo kazi ya kuratibu mchakato wa Katiba mpya linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi na kuongezeka kwa mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza sana **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na Serikali yake kwa ujumla kwa kuajiri watumishi wapya wengi katika taasisi chini ya Wizara hii. Mathalani, Kamati ilielezwa kuwa, waajiriwa wapya **354** katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni ongezeko kubwa zaidi lililofanyika kwa muda wa miezi tisa tu na halijawahi kutokea katika kipindi chochote cha Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa watumishi wapya kumepunguza kwa kiasi upungufu uliokuwa umekithiri wa watumishi kwenye baadhi ya taasisi. Aidha, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kutawezesha kuanzishwa kwa Ofisi mpya katika **wilaya 50** ambazo hazikuwa na Ofisi hii, na hivyo kufanya Ofisi hiyo kuwa na Ofisi katika wilaya 94 nchini na kubakia **Wilaya 45** pekee**.**

Aidha, kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo limepelekea mahitaji makubwa ya vyumba vya Ofisi kwenye baadhi ya wilaya jambo linaloweza kupelekea Ofisi kuwekwa katika vyumba vya kupanga. Pia kumepelekea mahitaji makubwa ya vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa watumishi, vielelezo na nyaraka nyingine muhimu. Kwa sababu hii, kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi na haraka za kuandaa Ofisi katika wilaya zote ambako Ofisi mpya zimeanzishwa pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi muhimu.

3.3 **Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 24,876,800,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 13,110,800,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 11,766,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepungua kwa **Sh. 1,094,770,000** sawa na **asilimia 4.2** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Sababu ya kupungua huku kunatokana na miradi mingi iliyopangwa Kwenda kutekelezwa kwa mwaka 2023/2023 tayari ipo katika hatua za utekelezaji kutoka mwaka 2022/2023 kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7** – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | **NA 6389** – Ujenzi wa vituo jumuishi wa taasisi za kisheria za Serikali Mwanza na Arusha | 2,000,000,000 | 0 |
| | **NA 6210** - Programu ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) | 0 | 455,000,000 |
| **Fungu 41 –** Wizara ya Katiba na Sheria | **NA. 5501** Awamu ya Pili ya Uimarishaji wa Upatikanaji Haki za Kisheria na Haki za Binadamu Tanzania | 0 | 234,510,000 |
| | **NA.5502** Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana | 0 | 650,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | na Rushwa Tanzania (BSAAT) | | |
| | **NA. 5507** Upatikanaji Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike | 442,668,000 | 3,912,627,880 |
| | **NA. 5508** Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu | 2,057,002,500 | 0 |
| | **NA. 6201** Haki Mtandao (e-Justice) | 2,611,129,500 | 0 |
| | **NA. 6207** Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji Haki (IMPACT) | 0 | 2,041,132,658 |
| | **NA. 6517** Kuimarisha Haki za Mtoto (UNICEF Multisectoral) | 0 | 3,378,219,462 |
| | **NA. 4632** Program ya | 0 | 234,510,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Usimamizi wa Utajiriasili na Maliasilia za Kijamii na Kiuchumi Tanzania (Natural Wealth and Resources Socioeconomic Governance) | | |
| **Fungu 35-** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | **NA 6389:** Ujenzi wa Ofisi katika mikoa mbalimbali | 6,000,000,000 | |
| **Fungu 6** | **NA 6210 -** Programu ujenzi wa Mfumo wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) | | 600,000,000 |
| | **NA. 6517** Kuimarisha Haki za Mtoto (UNICEF Multisectoral) | 0 | 260,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **13,110,800,000** | **11,766,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **24,876,800,000** | |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria, 2023 Taarifa ya Waziri kwa Kamati pamoja na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani na inaendelea kuishauri Serikali kuzidi kupunguza matumizi ya fedha za nje kadri inavyowezekana. Aidha, kamati inashauri Wizara kuendelea kuongeza bajeti ya maendeleo ili kuziwezesha taasisi zilizo chini yake kujenga majengo ya ofisi na kupunguza uhaba wa vyumba vya ofisi.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ibuni njia za kuongeza maduhuli kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuongeza kiwango cha makusanyo katika Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake.

(ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha Ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

(iii) Serikali iongeze vipindi vya elimu ya sheria kwa umma ili kuwawezesha wananchi kutambua wajibu na haki zao.

4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu

4.2.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

i) Serikali ihakikishe inawasilisha Bungeni taarifa ya hali ya utetekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu nchini ili kutekeleza matakwa ya Ibara ya 131(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

ii) Uwezeshaji wa upatikanaji wa miundombinu ya TEHAMA katika ngazi ya mahakama uendane sambamba na uboreshaji wa miundombinu hiyo katika taasisi ambazo ni wadau wa mahakama ikiwemo Magereza, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

iii) Wizara ihakikishe inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha mafunzo kwa watalaam wake kutokana na kupatikana kwa kiwanja Na 2 Kitalu “L” Hati Na. 70633 kilichopo Usagara Misungwi, Mkoani Mwanza kwa ajili ya kazi hiyo.

**4.2.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

(i) Serikali ihakikishe inatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Wanasheria wa Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo utungaji wa sheria ndogo;

(ii) Serikali ihakikishe inamaliza kazi ya kutafsiri Sheria Kuu (Principal Legislation) Pamoja na kuanza kazi ya kutafsiri kanuni zote zilizokatika lugha ya Kingereza Kwenda katika lugha ya Kiswahili ili ziweze kusomeka na kueleweka kwa urahisi na Wananchi;

**4.2.3 Fungu 35-Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

(i) Serikali ihakikishe inaanzisha Ofisi za Taifa za Mashtaka kwenye Wilaya ambazo hazina Ofisi hizo.

(ii) Kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya kikatili nchini ikiwemo mauaji ya binadamu jambo ambalo linaweza pia kuwatisha mashahidi wa Jamhuri na kupelekea mashahidi kutotoa ushirikiano wa kutoa ushahidi kwa upande wa Serikali, kamati inashauri Serikali kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya ulinzi wa mashahidi ili waweze kutoa ushirikiano kwa matukio wanayoweza kuyatolea ushahidi.

(iii) Serikali iendelee kuboresha mazingira ya kazi kwa waendesha mashtaka ikiwemo kuongeza vitendea kazi kama vile magari na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya usalama wa nyaraka na watumishi.

(iv) Serikali inashauriwa kuanza mpango wa kuwa na ulinzi kwa waendesha mashtaka hususani kwa waendesha mashtaka wanaosimamia mashtaka makubwa na yenye maslahi makubwa kwa nchi na jamii.

### 4.2.4 Fungu 19-Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

(i) Serikali ihakikishe inaendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watalaam wake ili kuweza kuwa na watalaam wa kutosha katika maeneo ya kimkakati kama vile gesi, mafuta, uwekezaji, anga, madini, uchumi wa bluu na TEHAMA.

(ii) Serikali inashauriwa kutangaza mafanikio inayoyapata pamoja na kazi zake ili iweze kufahamika kwa wananchi.

### 4.2.5 Fungu 12-Tume ya Utumishi wa Mahakama

(i) Tume ihakikishe inatumia majengo ya Serikali katika kuendeshea za vikao vya Tume ili kupunguza gharama.

(ii) Tume iendelee kuboresha matumizi ya TEHAMA ikiwemo kuongeza vifaa vya kurekodia Ushahidi.

### 4.2.6 Fungu 55-Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

(i) Tume ihakikishe inatangaza kazi zake ili ziweze kufahamika kwa wananchi.

(ii) Tume ihakikishe inafanya kazi za uchunguzi wa uvunjifu wa haki za binadamu na kutoa taarifa Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

### 4.2.7 Fungu 59-Tume ya Kurekebisha Sheria

(i) Tume ihakikishe inafanya tafiti za sheria hususani sheria za haki jinai, sheria za usalama barabarani, sheria za ardhi, hifadhi na wafugaji.

(ii) Tume ihakikishe inafanya utafiti wa sheria zilizopitwa na wakati na kupendekeza marekebisho yake bungeni.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasimi ya Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Damasi Daniel Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi Mkubwa pamoja na ushirikiano wa hali ya juu alioipatia Kamati hii wakati ikitekeleza majukumu yake. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb), Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kumsaidia vyema Waziri kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kwa ushirikiano alioipatia Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa

ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Mary Gaspar Makondo.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
25 Aprili, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha taarifa hiyo. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya bajeti ili aweze kuwasilisha. Mheshimiwa Omary Kigua kwa niaba ya Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. OMARI MOHAMED KIGUA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu

utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama Fungu Na. 40 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Sura ya 11, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadili na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 160.3 Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 61 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Mahakama, shilingi bilioni 2.4 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(IJA)*, shilingi bilioni 57.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)*, na shilingi bilioni 39.1 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, shilingi bilioni 36 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3.1 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 108.2 ambazo ni sawa na asilimia 67.5 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na asilimia 63 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni 39.5 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC),* shilingi bilioni 40.1ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(IJA)* na shilingi bilioni 27.1 ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 25.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.3 ni fedha za nje. Mwenendo huu ni wa kuridhisha na Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati na kama ilivyotarajiwa kwa Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulipanga kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni12.6 ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni shilingi bilioni 5.9 ikiwa sawa na asilimia 47.4 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/23, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa katika kutekeleza masuala yafuatayo:

(a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu ambapo katika kipindi cha Julai – Disemba, 2022 Mfuko wa Mahakama imeweza kufanya utatuzi wa mashauri 134,989 kati ya mashauri 185,291 sawa na asilimia 72 ya mashauri yaliyofunguliwa katika kipindi hicho.

(b) Uanzishwaji wa Mahakama zinazotembea *(Mobile Courts)* katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza pamoja na mipango ya kuendeleza katika Mkoa wa Arusha.

(c) Kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma ambapo Mfuko wa Mahakama imeweza kukamilisha maandalizi ya mfumo wa kurekodi na kutafsiri mwenendo wa mashauri (*transcription and translation software),* kukamilisha ujenzi wa Mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri pamoja na kufanya maboresho ya mifumo ya e-Wakili, *e-library, e- project management*, *e-court broker , process server* na *Judicial portal*.

(d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini ambapo Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Desemba, 2022 imeweza kukamilisha Ujenzi wa Mahakama 20 za Wilaya za Gairo, Mvomero, Kilombero, Songwe, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'wale, Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Sikonge na Mahakama ya Mwanzo Kimbe (Kilindi) pamoja na kuendelea kutekeleza ujenzi na ukarabati wa Mahakama mbalimbali pamoja na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu, nyumba za Majaji na wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2022/2023, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali.

(ii) Mahitaji ya bajeti yasiyoendana na maboresho.

(iii) Uhaba na uchakavu wa magari na hivyo kusababisha gharama kubwa za matengenezo.

(iv) Uchakavu wa Majengo ya Mahakama hasa za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali, kuona haja ya kuiongezea Mfuko wa Mahakama fedha kila mwaka ili hatimaye kukidhi mahitaji ya uendashaji wa Mahakama ambayo ndio chombo cha kutolea haki Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya Kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo:-

(a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu *(Backlog)*.

(b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma.

(c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama.

(d) Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, na nidhamu ya watumishi na

(e) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya bajeti kwa mwaka 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mfuko wa Mahakama ulipewa ukomo wa jumla ya Shilingi bilioni 217.9 Kati

ya fedha hizo, shilingi bilioni 61.2 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, shilingi bilioni 2.3 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(IJA)*, shilingi bilioni 69.6 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 84.8 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 31 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 53.8 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Fungu hili imeongezeka kwa shilingi bilioni 57.7 sawa na asilimia 36 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa fedha za maendeleo kutoka nje ambazo ni mkopo. Aidha, Kamati ilihakikishiwa juu ya uhakika wa upatikanaji wa mkopo huu na hivyo kutokuathiri utekelezaji wa miradi iliyo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli. Kwa upande wa mapato katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi bilioni 12.6. Maoni na mapendekezo ya Kamati, utekelezaji wa mpango (2021/2022 – 2025/2026) wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto inayoendelea kukabili Mfuko wa Mahakama ni pamoja na uhaba na uchakavu wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali. Aidha, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na ukosefu wa nyumba za Majaji, licha ya Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 kutoa shilingi bilioni 16 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, Mfuko wa Mahakama bado unakumbwa na changamoto hii. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za maendeleo za kutosha kila mwaka ili Mfuko wa Mahakama uweze kujenga Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya,

Mahakama Kuu pamoja na Nyumba za Majaji na Mahakimu ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi na vitendeakazi kwa Mfuko wa Mahakama. Ili kuongeza tija na ufanisi kwa Mfuko wa Mahakama ni dhahiri kwamba suala la watumishi wa kutosha na vitendeakazi kama vile magari ni muhimu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Mfuko wa Mahakama una upungufu wa watumishi 4,528, pamoja na uhaba na uchakavu wa magari. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza watumishi na vitendeakazi katika Mahakama zote nchini ili Mahakama itoe haki na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo za ndani. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba utolewaji wa fedha za maendeleo ya ndani umekuwa wa kusuasua. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 fedha za maendeleo ya ndani zimepungua kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Tano. Aidha, bado Mfuko wa Mahakama unatumia kiasi kikubwa cha fedha katika kukodi nyumba za Majaji pamoja na kumbi za mikutano. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha za maendeleo za ndani kwa Fungu 40 ili kuongeza ufanisi na tija ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuliko kutegemea fedha za nje ambazo upatikanaji wake siyo wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuziwezesha taasisi zinazofanya kazi pamoja na Mahakama. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya Ofisi ya Mahakama. Aidha, Mahakama katika kutekeleza majukumu yake hushirikiana na taasisi kama vile Jeshi la Polisi Tanzania, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Jeshi la Magereza. Kwa msingi huo, ni vyema taasisi hizi pia zikawezeshwa ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya TEHAMA. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha inafanya maboresho makubwa ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Mfuko wa Mahakama. Mifumo hii imepunguza gharama na kuokoa fedha za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mfuko wa Mahakama inamilikiwa na kuendeshwa na Serikali kwa asilimia 100. Mfano, mfumo wa kutafasiri unatumiwa na Mahakama lakini programu yake ni mali ya mtu binafsi. Hali hii inaweza kuhatarisha usalama wa mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vyema Bunge letu. Kamati inawashukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro - Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba - Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Pauline Gekul - Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha mashauriano na Kamati wakati wa kujadili Bajeti ya Fungu 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inamshukuru pia Dkt. Natu E Maamry Mwamba - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Prof. Elisante Ole Gabriel - Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na Wataalam wote wa Mfuko wa Mahakama na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umakini na weledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko

wa Mahakama. Naomba kuwatambua kama ilivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Emmanuel Rhobi na Makatibu wa Kamati kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya Shilingi 217,978,755,000 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**25 APRILI, 2023**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama sura ya 11, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadili na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 160,275,825,000.00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 61,017,018,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,391,425,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Shilingi**

**57,774,382,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 39,093,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Shilingi 36,002,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,091,000,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya **Shilingi 108,214,279,269.83** ambazo ni sawa na **asilimia 67.5** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/23 ikilinganishwa na **asilimia 63** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi 39,468,829,566.64 ni** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), **Shilingi 40,083,483,314.12** kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **Shilingi 1,568,646,130.70** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **Shilingi 27,093,320,258.37** ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 25,820,538,972.37** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,272,781,286** ni fedha za nje. Mwenendo huu ni wa kuridhisha na Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati na kama ilivyotarajiwa kwa mfuko huu

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2022/23 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Shilingi 12,571,199,000** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni **Shilingi 5,953,664,792.47** ikiwa sawa na **asilimia 47.4** ya lengo la mwaka mzima.

**Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Bajeti wa Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/23**

| Matumizi | Bajeti | Fedha zilizotolewa Hadi Februari | Asilimia ya Bajeti |
|---|---|---|---|
| Mishahara Mahakama | 61,017,018,000.00 | 40,083,483,314.12 | 65.7 |
| Mishahara | 2,391,425,000.00 | 1,568,646,130.70 | 65.6 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (IJA) | | | |
| Matumizi Mengineyo | 57,774,382,000.00 | 39,468,829,566.64 | 68.3 |
| Maendeleo Fedha za Ndani | 36,002,000,000.00 | 25,820,538,972.37 | 71.7 |
| Maendeleo Fedha za Nje | 3,091,000,000.00. | 1,272,781,286 | 41.2 |
| **Jumla Kuu** | **160,275,825,000.00** | **96,599,464,820.52** | **67.5** |

***Chanzo:*** *Mfuko wa Mahakama*

## 3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa katika kutekeleza masuala yafuatayo:

### 3.1. Mafanikio

a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu ambapo katika kipindi cha Julai – Disemba, 2022 Mfuko wa Mahakama imeweza kufanya utatuzi wa mashauri 134,989 kati ya mashauri 185,291 sawa na **asilimia 72** ya mashauri yaliyofunguliwa katika kipindi hicho;

b) Uanzishwaji wa Mahakama zinazotembea (Mobile Courts) katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza pamoja na mipango ya kuendeleza katika Mkoa wa Arusha;

c) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma ambapo Mfuko wa Mahakama imeweza kukamilisha

maandalizi ya mfumo wa kurekodi na kutafsiri mwenendo wa mashauri (transcription and translation software), kukamilisha ujenzi wa Mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri pamoja na kufanya maboresho ya mifumo ya e-Wakili, e-library, e- project management, e-court broker , process server na Judicial portal; na

d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini ambapo Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Desemba, 2022 imeweza kukamilisha Ujenzi wa Mahakama 20 za Wilaya za Gairo, Mvomero, Kilombero, Songwe, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'wale, Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Sikonge na Mahakama ya Mwanzo Kimbe (Kilindi) pamoja na kuendelea kutekeleza ujenzi na ukarabati wa Mahakama mbalimbali pamoja na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu, nyumba za Majaji na wafanyakazi.

### 3.2. Changamoto

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2022/23, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali;
ii. Mahitaji ya bajeti yasiyoendana na maboresho;
iii. Uhaba na uchakavu wa magari na hivyo kusababisha gharama kubwa za matengenezo; na
iv. Uchakavu wa Majengo ya Mahakama hasa za Mwanzo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuona haja ya kuiongezea Mfuko wa Mahakama fedha kila mwaka ili hatimaye kukidhi mahitaji ya uendashaji wa Mahakama ambayo ndio chombo cha kutolea haki Kikatiba.

## 4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2023/24, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo:-

a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);
b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;
c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;
d) Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, na nidhamu ya watumishi; na
e) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

### 4.1. *Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24*

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Mahakama ulipewa ukomo wa jumla ya **Shilingi 217,978,755,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 61,234,024,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,345,228,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Shilingi 69,620,476,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na **Shilingi 84,779,027,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 31,002,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 53,777,000,000.00** ni fedha za nje. Bajeti ya fungu hili imeongezeka kwa **shilingi 57,702,930,000** sawa na **asilimia 36.0** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/23. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa fedha za

maendeleo kutoka nje ambazo ni mkopo. Aidha, Kamati ilihakikishiwa juu ya uhakika wa upatikanaji wa mkopo huu na hivyo kutokuathiri utekelezaji wa miradi iliyo chini yake.

### 4.2. *Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato katika mwaka wa fedha 2023/24 Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 12,571,199,000.00**.

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 5.1. *Utekelezaji wa Mpango (2021/22 – 2025/26) wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali*

**Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto inayoendelea kukabili Mfuko wa Mahakama ni pamoja na uhaba na uchakavu wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali. Aidha, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na ukosefu wa nyumba za Majaji, licha ya Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kutoa **Shilingi bilioni 16** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, Mfuko wa Mahakama bado unakumbwa na changamoto hii. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za maendeleo za kutosha kila mwaka ili Mfuko wa Mahakama uweze kujenga Mahakama za mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu pamoja na Nyumba za Majaji na Mahakimu ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi.

### 5.2. *Watumishi na Vitendea kazi kwa Mfuko wa Mahakama*

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza tija na ufanisi kwa Mfuko wa Mahakama ni dhahiri kwamba suala la watumishi wa kutosha na vitendea kazi kama vile magari ni muhimu. Uchambuzi wa

Kamati ulibaini kwamba Mfuko wa Mahakama ina upungufu wa watumishi 4,528, pamoja na uhaba na uchakavu wa magari. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza watumishi na vitendea kazi katika mahakama zote nchini ili Mahakama itoe haki na kwa wakati.

### 5.3. *Fedha za Maendeleo za Ndani*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba utolewaji wa fedha za Maendeleo ya ndani umekuwa wa kusuasua. Katika mwaka wa fedha 2023/24 fedha za maendeleo ya ndani zimepungua kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 5**. Aidha, bado Mfuko wa Mahakama inatumia kiasi kikubwa cha fedha katika kukodi nyumba za Majaji pamoja na kumbi za mikutano. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha za maendeleo za ndani kwa Fungu 40 ili kuongeza ufanisi na tija ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuliko kutegemea fedha za nje ambazo upatikanaji wake sio wa uhakika.

### 5.4. *Kuziwezesha Taasisi zinazofanya kazi pamoja na Mahakama*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya Ofisi ya Mahakama. Aidha, Mahakama katika kutekeleza majukumu yake hushirikiana na Taasisi kama vile Jeshi la Polisi Tanzania, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Jeshi la Magereza. Kwa msingi huo ni vyema Taasisi hizi pia zikawezeshwa ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuwa na tija.

### 5.5. *Mifumo ya TEHAMA*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha inafanya maboresho makubwa ya matumizi ya mifumo ya

TEHAMA katika Mfuko wa Mahakama, mifumo hii imepunguza gharama na kuokoa fedha za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mfuko wa Mahakama inamilikiwa na kuendeshwa na Serikali kwa asilimia 100. Mfano mfumo wa kutafasiri unatumiwa na Mahakama lakini Programu yake ni mali ya mtu binafsi. Hali hii inaweza kuhatarisha usalama wa mfumo.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vyema Bunge letu. Kamati inawashukuru Mheshimiwa Dkt Damasi Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Pauline Gekul Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha mashauriano na Kamati wakati wa kujadili Bajeti ya Fungu 40. Aidha, Kamati inamshukuru pia Dkt. Natu E Maamry Mwamba Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Prof. Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na wataalam wote wa Mfuko wa Mahakama na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb) kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umakini na weledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb — Mwenyekiti

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Joseph Zacharious Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Zainab Athumani Katimba, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Dkt. Charles Kimei, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Omari Ali Omari, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi na Makatibu wa Kamati kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 jumla ya **Sh. 217,978,755,000** kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Daniel Baran Sillo (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
25 Aprili, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omari Kigua kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na mjadala wa jumla tuna tangazo dogo hapa kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria, kuna wageni wake ambao ni Naibu Mwanasheria Mkuu Dkt. Evaristo Longopa yupo hapa pia kuna wawakilishi kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa Tume Ndugu Alesia Mbuya na mwisho tuna Ndugu Grephen Mwakapeje Katibu Mtendaji Tume ya Kurekebisha Sheria, karibuni sana wageni wetu.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo dogo ambalo wote mnataarifiwa na kukumbushwa kwamba kliniki ya ardhi bado inaendelea katika viwanja vya Bunge na hivyo nyote mnatakiwa mfike kwa ajili ya huduma na watakuwepo hadi Tarehe 28 Aprili mwaka huu.

Waheshimiwa Wabunge tunaanza mjadala wetu wa jumla naanza na Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Luhaga Mpina wajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika bajeti ya

Wizara ya Katiba na Sheria na naomba nianze kwa kutambua na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa ya kuimarisha eneo zima la haki za binadamu, demokrasia pamoja na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hayo napenda kufanya rejea kwenye mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara Katiba na Sheria ambayo nilitoa mwaka jana Tarehe 28 Aprili, 2022 ambapo nilipendekeza ya kwamba Serikali ilete Bungeni Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria ya Uchaguzi ili zifanyiwe maboresho kwa lengo zima la kuimarisha ushiriki wa wanawake kwa maana ya usawa wa kijinsia katika siasa lakini pia kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake ndani ya vyama vya siasa na vivyo hivyo kutambua suala zima la ukatili wa kimtandao kwa wanawake wanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Damasi Ndumbaro ambaye aliridhia mapendekezo hayo na akaielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria ibebe jukumu hilo na ianze kufanya mapitio ya sheria hizo mbili, nami nilipata fursa ya kukutana na Tume hiyo na kuwasilisha maoni yangu siku ya Tarehe 11 Mei, na naipongeza sana Tume ya Kurekebisha Sheria kwa sababu natambua ya kwamba, mwezi wa Tatu mwaka huu wamewasilisha ripoti ya mapendekezo yao kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hivyo naipongeza sana Kikosi Kazi cha Mheshimiwa Rais waliopewa jukumu la kutoa maoni na mapendekezo kuhusu hali nzima ya masuala ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa hapa nchini, ambao na wao wameshawasilisha ripoti yao kwa Mheshimiwa Rais waliwasilisha mwishoni mwa mwaka jana, nami pia nawashukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni yangu mbele ya kikosi kazi hicho siku ya Tarehe 14J ulai, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu naomba nitumie fursa hii kuishauri na kuiomba Serikali kwamba itakapoleta maboresho ya sheria hapa Bungeni ya Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria ya Uchaguzi yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Uchaguzi itakapoletwa iainishe bayana namna ambavyo uteuzi wa wagombea ndani ya Vyama vya Siasa utafanywa na itapendeza sana iwapo sheria hii itakamilika na kuletwa Bungeni kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka kesho 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, kwa takwimu za sasa ni asilimia 2.1 tu ya Wenyeviti wa Vijiji ambao ni wanawake asilimia 12.8 tu ya Wenyetivi wa Serikali za Mitaa ambao ni wanawake asilimia 6.7 tu ya Wenyeviti wa Vitongoji ni wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba bado ipo haja ya kuongeza idadi ya viongozi wanawake katika hizi nafasi za kisiasa. Kwa muktadha huo, lazima Sheria ya Vyama za Siasa pamoja na Sheria ya Uchaguzi zije Bungeni kabla ya mchakato mzima wa kuteua wagombea kwa ajili ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili; katika mchakato wa Katiba mpya, naiomba sana Serikali ihakikishe kwamba asasi za kiraia kwa maana ya *CSOs* na *NGOs* zishirikishwe ipasavyo. Moja, zishirikishwe katika kutoa elimu kwa umma kuhusu Katiba; pili, zishirikishwe katika kutoa mchango na maoni katika namna bora ya kuboresha Katiba mpya. Hapa nitilie mkazo, ni muhimu sana kuhakikisha asasi za kiraia kwa maana ya *CSOs* na *NGOs* za mikoa ya pembezoni nazo zinashiriki ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu ni kuhusiana na *Samia Legal Aid Campaign*. Naipongeza sana Serikali kwa kuja na *Samia Legal Aid Campaing,* lakini nitumie fursa hii kusisitiza kwamba *Samia Legal Aid Campaign* ijielekeze zaidi katika changamoto ambazo zinawakumba wanawake na watoto. Mathalani, matunzo kwa watoto, ukatili wa kijinsia, mirathi, ardhi na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo huo, asasi za kiraia kwa maana *NGOs* na *CSOs* zipate fursa ya kushiriki katika maeneo yao. Hapa kipekee na kwa upendeleo kabisa naiomba sana Serikali kupitia Wizara hii, kwamba kwa kuwa Kagera ni kati ya mikoa ambayo ina changamoto kubwa katika maeneo haya, basi katika ile mikoa mitano ya mwanzo ambapo *Samia Legal Aid Campaign* itakwenda kufanyika, na Mkoa wa Kagera uwe mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kusemea viongozi wa Serikali za Mitaa. Nimefanya utafiti mdogo katika majimbo yetu na Wabunge wa majimbo wapo hapa ndani ya Bunge; iko changamoto kubwa ambayo inaendelea kwamba Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa, au Mwenyekiti wa Kitongoji anaweza akaondolewa katika nafasi yake bila kufuata utaratibu unaostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, itakapoleta hapa Bungeni Sheria ya Uchaguzi, ihakikishe Sheria hii inawalinda Viongozi wa Serikali za Mitaa waweze kumaliza muhula wao kama ambavyo sheria hii inalinda Madiwani na Wabunge. Pale ambapo kutakuwa na hitaji la kumwondoa kiongozi yule, basi kuwe na utaratibu ulio wazi, unaoeleweka ili kuondoa mianya ya hivi sasa ambayo inaweza kupelekea mtu kufanyiwa hila, mtu kutotendewa haki na kuondolewa pasipo utaratibu sahihi. Siyo hivyo tu, kuna suala zima la haki ya

kuchaguliwa na haki ya kuchagua. Hivi sasa yako maeneo mengi ambayo yanaongozwa na aidha Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kwa maana ya Wenyeviti wa Mtaa au Wenyeviti wa Vitongoji ambao wanakaimu. Hili jambo siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali ihakikishe kwamba inaweka utaratibu wa kulinda viongozi wetu wa Serikali za Mitaa kama ambavyo Madiwani na Wabunge wanavyolindwa, na pale ambapo kutakuwa na haja ya kumwondoa, basi uwekwe utaratibu rasmi kwa maana ya kufuata vigezo ili *impeachment* iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Lugangira. Nilimtaja Mheshimiwa Yahaya Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Agnes Lambert ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Nami nichukue nafasi hii kupongeza walioaminiwa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Wizara hii ya Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro, Naibu wake na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa utendaji mzuri ambao kwa hakika sisi kama Wabunge ambao tumepewa dhamana na Mheshimiwa Spika katika Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo tunaisimamia Wizara hii, tunaona namna ambavyo wanaitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia utendaji wa wateuliwa wengine ambao wameaminiwa katika Wizara hii

wakiwemo Mtendaji Mkuu wa Mahakama, *DPP*, *Solicitor General* kwa kazi zao nzuri ambazo wanazozifanya. Mmeona wenyewe aliposimama Ole-Gabriel hapa, makofi yalikuwa mengi sana; ni kwa sababu ni mtu ambaye ana ushirikiano na wenzake na ni mtu ambaye anafikika kirahisi sana. Kwa hiyo, utendaji wake unaonesha ni namna gani ambavyo anastahili kuwepo katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite katika kushauri, baada ya kutembelea na kuona majengo mazuri ambayo yamejengwa na Serikali kupitia Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Wizara hii ya Katiba na Sheria majengo ya Mahakama Jumuishi, na Mahakama za Mwanzo nyingi ambazo Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti hapa amezitaja. Ni kwamba anaendelea kuonesha kwamba dhamira ya Nchi hii ya utoaji haki kuwa katika sehemu ambazo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na changamoto kubwa hapo nyuma ambapo ukipita vijijini kwetu, wilaya na miji yetu, jengo lililokuwa baya sana ni la Mahakama, lakini sasa imekuwa kinyume chake, kwa sababu Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia ambao amewaamini kufanya kazi kwa niaba yake, wanafanya kazi vizuri na kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite kwenye jambo dogo tu na nichukue nafasi hii kulizungumzia, ni Tume ya Kurekebisha Sheria. Kuna sheria ambazo zinakizana na zipo lakini nyingine za miaka mingi sana. Kuna sheria za miaka ya 1970, na nyingine tumerithi kwa mkoloni, lakini zipo na *still* zinafanya kazi. Matokeo yake utendaji haki unakuwa haufanyiki vizuri. Sababu ni nini? Tunaendelea kuiomba na kuishauri Tume ya Mahakama iende ichakate sheria nyingi ambazo zinakizana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tu leo katika Bunge lako kipindi cha asubuhi, kulikuwa na hoja zilikuwa zinazungumzwa hapa kwamba kuna sheria zinakizana; Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto na Sheria ya Elimu. Hizi sheria zikitengenezwa vizuri, mgogoro ni mdogo sana kuliko tunavyodhani na tunavyoubeba. Ni nani anayehusika? Ni Tume hii ya Kurekebisha Sheria, inatakiwa ije na mchakato mahususi maalum ambao utafanya sasa tutoke katika kusuguana humu, sheria ipi ni bora na sheria ipi siyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kukubali mchakato wa Katiba. Mchakato wa Katiba utaondoa manung'uniko machache ambayo yapo. Sisi ambao tunaamini Katiba hii ni nzuri, ni marekebisho kidogo tu ambayo inaweza ikayafanya. Nampongeza Mheshimiwa Rais katika hii *Legal Aid Campaign* ambayo anaifanya. Kwa kweli itawasaidia sana watu wetu ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili ili kupata msaada wa kisheria. Kampeni hii pia itatoa elimu pana kwa mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Tume hii ya kurekebisha sheria, kuna mambo ambayo yanazungumzwa sana hapa sasa hivi kwenye mitandao na watu wetu, na katika Bunge lako Tukufu hili. Hapo nyuma kulikuwa na jambo ambalo linazungumzwa kuhusu ushoga la usagaji. Sheria za Ushoga zipo wazi sana, lakini Sheria za Usagaji bado zimejifumba, hazipo wazi. Atahukumiwaje msagaji na yule anayesagwa? Kwa hiyo, tunaiomba sana Tume ya kurekebisha sheria ije na hili, ilichakate ili kuja na sheria ambayo itatoa adhabu kali kwa hawa watu. Kwa sababu kwa sura iliyopo sasa hivi, ulawiti kwa watoto na kwa watu wa namna yeyote sheria zake zipo, lakini usagaji sheria imekaa kimya. Kwa hiyo, naomba sasa Tume hiyo ya Kurekebisha Sheria ije na mchakato huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nitapenda kulizungumzia kwa muhtasari tu kidogo, naona dakika zetu siyo nyingi; mwaka 2022 kwenye taarifa zilizopo ambazo siyo rasmi lakini ni za kweli, ni kwamba watoto waliolawitiwa mwaka 2022 ni 1,555. Kati ya hao, watoto 1,358 ni watoto wa kiume. Watoto wa kike waliolawitiwa ni 197. Ni jinsi gani tuone janga hili kwamba sasa limekuwa janga la Kitaifa. Kwa sababu gani? Tumekuwa tuna mchakato wa muda mrefu. Katika Bunge hili, miaka hii miwili tumekua tunaona hosteli zinajengwa nyingi hasa za sekondari kwa ajili ya wasichana, tumesahau vijana hawa, ambao ni watoto wadogo ambao sasa janga hili limehamia kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Tume hii ya Kurekebisha Sheria nayo ione. Pia Serikali iione kwamba sasa tutoke tulipokuwa tumejikita, tuone sasa wamehamia badala ya kukimbia kwa wa miaka 30, wanakimbilia kwa vijana wetu. Jambo hili ni hatari kwa jamii na tunaenda kutengeneza jamii ambayo baadaye sio mwanaume; atakuwa na sura ya kiume, lakini sio mwanaume. Sasa hawa wadada ambao wanakua, watapataje wanaume? Hilo nalo ni changamoto nyingine. Naomba tulisimamie hili kwa dhamira nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuishauri Serikali kupitia *DPP, Solicitor General* na *AG*. Uhalifu wa mitandaoni sasa unashika kasi sana. Ni vyema sasa na wao wakaenda na huu upepo wa kidunia, kwa sababu itabidi Mawakili wa Serikali kwenda kutetea kesi za mitandaoni, Waendesha mashtaka wataenda kuendesha kesi zinazotokana na wizi wa mitandaoni, na Mwanasheria Mkuu hivyo hivyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie na itoe elimu pana kwa Mawakili wetu wa upande wa *DPP* na upande wa Wakili Mkuu wa Serikali ili wapate elimu hii pana ya wizi wa mitandaoni ili waweze kunusuru watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare, nilimtaja Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Agnes Lambert na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ili nami niweze kuchangia hii hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa kwa namna ambavyo wanavyoendelea kuchapa kazi kule, nami nipo hapa Bungeni kuhakikisha kwamba nawawakilisha kikamilifu kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi wa Jimbo la Kisesa kama tulivyokubaliana kwamba masaa ni namba, na hakuna kupumzika mpaka kazi ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, suala la mambo ya kiujumla. Moja, Serikali imeshindwa kurudisha mifugo ya wafugaji 6,000 ambao wameshashinda kesi Mahakamani. Mheshimiwa Waziri suala hili ni la muda mrefu sana. Kwa sababu ni la muda mrefu, sasa Serikali itekeleze. Wapiga kura wangu mimi wa Jimbo la Kisesa ambao wanadai mifugo hii zaidi ya ng'ombe 400, sasa hivi wapo njiani kuja kuchukua mifugo yao. Akina Sai Maduhu, Masunga Muhamari, Ndaturu Muhororo, Zengo Kusekelwa, Dandika Kamasaga, Sambai Deke, hata akina Mzee Rerina kule kwa ndugu yangu hapa Mbunge, nao wote wako njiani kuja kuchukua mifugo yao. Sasa ni muhimu Serikali ikabidhi hao mifugo kwa hao wananchi ambao wameshinda kesi kihalali Mahakamani, warudishiwe mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa haraka haraka…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Rais ya Haki za Binadamu…

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa tu mzungumzaji, mimi pia Ushetu nina wananchi wangu walishinda kesi mwaka 2019, wako watatu, ng'ombe 500 na *documents* zote nimeshawapelekea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake na kwamba hawa wafugaji wote wa ng'ombe 6,000 wapo njiani kuja kuchukua mifugo yao hapa Dodoma kwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Tume ya Rais ya Haki za Jinai, mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake haya makubwa ya kuamua kuangalia kasoro na dosari zilizopo katika suala la ukamataji, upelelezi, uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka na kuinda hii Tume. Pia naipongeza Tume sasa hivi inavyoendelea. Changamoto moja tu ni kwamba wanapopata maoni hadharani ya watu wanaowapa maoni: Moja, wanasababisha watu wengine ule uhuru wa kutoa mawazo unapungua, lakini pia inaweza ikafanyika kampeni ya upotoshaji ili mwisho wa siku wakatoka na *results*

ambazo hazikutarajiwa, ambazo Mheshimiwa Rais hakuzitarajia wala wananchi hawakuzitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni Maazimio ya Bunge kuhusu kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali. Imesema, taarifa ya Mheshimiwa ya Waziri Kiambitisho B, ukurasa wa 146 anasema, Bunge liliazimia kuridhia kufuta hasara ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo hapa, taarifa hii ililetwa hapa Bungeni kwa *Order Paper* tarehe 19 Septemba, 2022 lakini haikujadiliwa hapa Bungeni na madai yaliyokuwa ya Waziri wa Fedha yalikuwa ni shilingi bilioni 19.75 zisamehewe, zifutwe kwenye vitabu vya Serikali, lakini Bunge hili halikujadili taarifa hiyo. Bunge liliahirishwa siku hiyo saa 4.39, hatukujadili wala hatukuridhia. Sasa haya mambo ya kuridhia, Waziri wa Katiba na Sheria ameyatoa wapi? Nani amemletea taarifa za kuridhia? Kwa nini anataka kulidanganya Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili, eneo hilo hilo la Azimio la Bunge, ni kufutwa kwa madai ya malimbikizo ya kodi. Nilisema kipindi kile; nililalamika sana huko nyuma kuhusu kufutwa kwa madai ya Shilingi trilioni 5.59, na kama maelezo ya Waziri ya Fedha alivyokuwa akiyatoa hapa, lakini Taarifa za Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2021/2022 zinasema kwamba haya mahesabu hayajaoneshwa kwenye vitabu hivyo, na hivyo inamaanisha kwamba yamefutwa. Kama yamefutwa, basi itakuwa amekiuka sheria Waziri wa Fedha anayehusika, na *TRA* watakuwa wamekiuka sheria kwa sababu hawana mamlaka hiyo kwa mujibu wa sheria, kifungu cha 34(1) ambacho kinataka lazima yapite hapa Bungeni na tuamue kwa njia ya azimio. Kwa hiyo, ukifuta tu kienyeji, maana yake unaingia kwenye makosa ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uendeshaji wa mashtaka. Hapa, *DPP* ameshindwa kukusanya Shilingi bilioni 170.61 ambazo tayari Mahakama imehukumu kwamba Washitakiwa wanatakiwa kutoa, hizi ni fedha za *plea bargaining*. Sasa ameshindwa kukusanya hizo fedha bila sababu zozote za msingi, na alikuwa na uwezo wa kukata rufaa upya, alikuwa na uwezo wa kutaifisha mali za washitakiwa wanaodaiwa, lakini mpaka sasa hivi *DPP* wetu ameshindwa kukusanya fedha hizo, na sababu za kutokukusanya hazieleweki. Namwelewa vizuri sana uwezo wake Sylvester Mwakitalu, huyu *DPP* wetu, ni Mwanasheria mzuri, nini kilichomkwazwa ashindwe kukusanya mapato halali ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa zinaletwa mbwembwe nyingi, mara unajua walionewa, mara unajua hawa... Kama ulinionewa, maamuzi haya hayakufanywa kwa *DPP* wakati huo. Maamuzi haya yalifanywa na Mahakama. Kama ulionewa, ulikata rufaa? Kwa nini hizi fedha hazijakusanywa? Suala la kutokukusanya fedha hizi limefanyika, Waziri wa Katiba na Sheria yupo, Waziri wa Fedha yupo, lakini naye *DPP* yupo. Kama *DPP* anashindwa kukusanya mpaka fedha ambazo zipo kwa mujibu wa sheria: Je, anapopokea mashtaka mengine kutoka kwa *DCI,* anapopokea mashauri mengine kutoka kwa TAKUKURU, anayafanyaje? Kama hawezi kukusanya, hata yale haya ambayo yako kwa mujibu wa sheria, Shilingi bilioni 170 Watanzania wanateseka fedha zao zipo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili suala la usimamizi wa mikataba. Tumeelezwa kwenye hotuba ya Waziri kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameweza kufanya upekuzi mikataba 1,304 na katika mikataba hiyo, mikataba 567 ina thamani ya Shilingi trilioni 91. Maana yake kuna mikataba 737 nayo haijafanyiwa uthamini katika mwaka mmoja wa fedha. Sasa kama Serikali imeenda kuingia mikataba ya trilioni moja,

Bajeti ya maendeleo tulinayoipitisha iko *around* Shilingi trilioni 15. Sasa hii mikataba ni ipi? Kwa nini haijawekwa kwenye majedwali? Ukienda kwenye viambatisho vyake kule, ameweka vitu vingine tu. Kilichoshindikana nini kuweka jedwali linaloonesha mikataba hii ya trilioni 91 ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tusipofanya hivyo, Serikali inaweza ikaingia mikataba ambayo haimo kwenye bajeti, haipo kwenye mpango wa maendeleo na sisi kama wasimamizi wa rasilimali za Taifa tukawa hatujalitendea haki Taifa hili kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini Waziri ameshindwa kuweka kiambatisho hapa kama Wabunge tujue mikataba hiyo ni ya nini? Miradi hiyo ni ya jambo gani? Sasa hivi tumeona mikataba 737 haijafanyiwa uthaminishwaji; na kwa nini haijafanyiwa uthaminishwaji? Mingine imefanyiwa uthamanishwaji, kwa nini hii haijafanyiwa? Hii ambayo imefanyiwa uthamanishwaji ni 567 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tutende haki. Waziri huyu, hakuna kupitisha bajeti yake, nanyi Wabunge nawaomba mpaka alete hili jedwali ili tujiridhishe na hicho ambacho kilichomo kwenye Hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la karibia mwisho, ni mashauri na madai ya usuluhishi; mashauri na madai ya usuluhishi hapa, jambo zuri hapa limetajwa kwamba tumeokoa hasa kwenye usuluhishi kwenye madai tumeokoa kama shilingi bilioni 165. Kwenye usuluhishi ni shilingi trilioni 13.33 na nasema; dakika moja tu namalizia.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi trilioni 13.33 wanasheria wetu wameshinda kesi mahakamani na

tukaokoa shilingi trilioni 13.33 ni jambo zuri. Mwezi wa 12 niliomba hapa jedwali lile liletwe tumeshinda kwenye mambo gani? Ni kesi zilihusu nini? Kwanini unatuletea tu idadi ya kesi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kama tusipofanya hivyo, tutaendelea kuingia kwenye matatizo. Hapa Waziri amesema tu kesi tulizoshinda lakini tulizoshindwa ameshindwa kusema na ndiyo maana hapa tuna ile kesi….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina muda wako umeisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:…** ya *Standard Chartered Bank* ya Hong Kong shilingi bilioni 342 ambayo nayo tulishindwa. Sasa haya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina muda wako umekwisha. Nilimtaja Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Eric Shigongo wajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita katika Tume ya Haki za Binadamu, Fungu 55. Katika Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katiba imeweka wazi kabisa majukumu inayopaswa kutekelezwa na Tume hii ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma majukumu haya kwa umakini na kwa umakini utaona namna ambavyo tume hii

imepewa majukumu mazito sana, majukumu nyeti, majukumu ambayo yasipotekelezwa kwa ufanisi wake Taifa hili litajikuta liko katika hatari kubwa sana ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki kwa maana ya Tume ya Haki za Binadamu pamoja na majukumu mengine tume hii ina wajibu wa kumulika taasisi zote za Kiserikali kuangalia kama misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora vinasimamiwa, vinatekelezwa kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hili ni kubwa sana na ukiangalia ukubwa wa majukumu ya tume hii utakubaliana na mimi kwamba Bajeti ya Tume hii inapaswa kwenda sambamba na uzito wa majukumu yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijaendelea mbele naomba nilipitishe Bunge lako Tukufu katikati ya Bajeti za miaka mitatu mfululizo ya Tume hii ya Tume ya Haki za Binadamu ili kwa pamoja tuangalie kama kweli bajeti hii inaendana sambamba na majukumu mazito ambayo tume hii imekabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022 tume hii iliomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 373.6. Nafahamu wewe ulikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, unafahamu vizuri majukumu haya. Katikati ya majukumu haya tume inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 373.6 pekeyake. Hiyo kama haitoshi, fedha hizi kwa 100% ni fedha za kutegemea wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika hatua Taifa lianweka rehani haki za Watanzania kwamba sasa wahisani ndiyo waje

sasa kulinda haki zetu nchini, tunapotea na tunazidi kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa Fedha wa 2022/2023, tume hii iliomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 115 tu. Kumbuka mwaka uliopita ilikuwa ni shilingi milioni 373 nayo ilikuwa ni ndogo tulipiga kelele. Sasa ikaenda mwaka unaofuata ikasema sasa hatuhitaji hata hiyo mia tatu sabini na kitu. Ikasema tunahitaji shilingi milioni 115 tu ambazo fedha hizi kwenye Wizara zingine hata kwenye baadhi ya mafungu ya Katiba na Sheria ni fedha za viburudisho tu, chai yaani chai na korosho, lakini tume inatuambia inahitaji milioni 115 kutekeleza wajibu wake wa kikatiba wa kulinda haki za Watanzania, *this is a joke. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, milioni hii 115 iliyoombwa mpaka Februari mwaka huu haijatoka hata shilingi moja. Ina maana gani hii? Ina maana ndani ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 Tume hii ya Haki za Binadamu ilikuwa ofisini kabisa inakula bata. Kwa sababu fedha hizi ni fedha za maendeleo na tume hii ili uweze kutoka na kwenda kutekeleza wajibu wake lazima fedha ya maendeleo iwepo kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituko kingine sasa mwaka huu wa fedha ambao sasa tuko hapa tunajadili bajeti ya Tume hii ya Haki za Binadamu, tume hii imesema yenyewe haina kazi kabisa ya kufanya. Yaani haiihitaji hata shilingi mia kutimiza wajibu wake na kwa lugha nyingine tume hii inataka kulieleza taifa au inataka kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba uvunjwaji wa Haki za Binadamu nchini umeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haujaisha na ndiyo maana Mama yetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele kila anapokutana na watu kila anapokwenda

anakemea juu ya uvunjifu wa Haki za Binadamu. Wabunge wengine wamesema lakini hata vyombo vingine vinavyosimamia ambavyo siyo vya Kiserikali ambavyo vinasimamia vinafuatilia mwenendo mzima wa Haki za Binadamu nchini wanasema ukiukwaji wa Haki za Binadamu nchini kwa sasa ni mkubwa kuliko wakati mwingine ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba fedha hizi kwa 100% ni fedha za wahisani. Utakumbuka kwa sasa taifa au niseme dunia kila nchi sasa hivi inapambana na hali yake kupambana na mapenzi ya jinsia moja kwa maana ya ushoga. Asilimia kubwa ya wahisani ambao wanasaidia nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania ni wale ambao wanaamini kwamba mapenzi ya jinsia moja ni Haki namba moja ya Binadamu; *which is not true*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kutegemea fedha za wahisani matokeo yake ndiyo haya tume inakaa ofisini haina kazi ya kufanya, ni watumishi ambao wana ajira za kudumu, wanalipwa mishahara inayotokana na kodi za Watanzania ambao ndiyo wanyonge hao hao ambao haki zao zimebinywa, zimepokwa na wanalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halikubaliki na niseme kabisa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapa atueleze hivi anadhani tume hii inapaswa kuendelea kuwepo? Tume ya kukaa ofisini, tume inayokuja leo inasema tunahitaji mtupitishie bajeti tu ya mshahara na viburudisho, sisi hatuna kazi ya kufanya. Waziri asiponipa majibu yanayojitosheleza, siku ya leo nitakwenda kukamata shilingi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niendelee kusema katikati ya changamoto za Tume ya Haki za Binadamu, tume ambayo haifanyi kazi kabisa kwa sababu kwanza haina fedha inahitaji uwe na kiongozi mwenye moyo wa kujali na kulinda

Haki za Binadamu kama Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan ambaye aliona kwa jicho la pembeni kwamba tume hii siyo tu imelala, yaani imeshajivua wajibu wake kabisa wa kikatiba ndipo alipoamua baada ya kusikia kelele za Watanzania kutokana na haki zao kupokwa akaamua kuunda Tume Maalum, Tume Maalum ambayo kazi yake ni kuchunguza mwenendo wa Haki za Binadamu nchini. Jukumu ambalo kikatiba wamekabidhiwa tume ya haki za binadamu na kwa lugha nyingine kuwa na tume nyingine hii ambayo Mama yetu Samia Suluhu Hassan ameiona na huenda asingeiweka tungekuwa katika hali ya hatari sana ya ukiukwaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyingine ni kwamba kwa sasa hivi Tume hii ya Haki za Binadamu imeisababishia Serikali kuingia gharama nyingine ya kuunda tume nyingine ya kufanya majukumu yake yale yale wakati tume yenyewe iko ofisini na mshahara unaotokana na kodi za Watanzania wanachukua kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Nimekuwa nikijiuliza na niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwenye kamati, nikasema; Tume ya Haki za Binadamu ina jukumu la kumulika taasisi za Kiserikali ili kuona kama Haki za Kibinadamu zinatendeka na nikasema kama ndiyo hivyo, tumekuwa tukimwona *CAG* akileta taarifa zake hapa Bungeni za kila mwaka na tumekuwa tukiona vituo vingine visivyo vya kiserikali viantaoa taarifa zake mfano kama hii hapa nikipata muda wa kuielezea nitaielezea ni kwa nini basi tume hii yenye wajibu wa kikatiba isiwe inaleta ripoti yake ya uchunguzi wa mwenendo wa haki za binadamu hapa Bungeni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnesta.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta muda wako umekwisha.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Eric Shigongo baadaye mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii nyeti, nianze kwa kusema kabisa kwamba naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nipongeze na kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imefanya kazi kubwa, imefanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya utoaji haki. Kwetu sisi ambao tulikaa kaa kidogo kwenye hii sekta kwa muda mrefu tunaona kabisa kama ni mapinduzi makubwa kwa sababu ni sekta ambayo ilikuwa kama imesahauliwa, majengo yalikuwa yamechakaa hata karatasi za kuandikia zilikuwa wakati mwingine ni shida unapoingia mahakamani asubuhi lakini kwa hali ilivyo sasa hivi kwa kweli tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Rais amegundua kabisa kwamba hapo ndiyo mahali ambapo akifanya uwekezaji hata nchi yetu itaheshimika duniani kote kwa sababu ya utoaji haki ulio katika viwango bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia viongozi wa Wizara hii, ndugu yangu na rafiki yangu Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri na Dada yangu Dada Pauline Gekul pamoja na wengine wote ambao ni wadau katika kuongoza sekta hii muhimu ya utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesisitiza juu ya suala la utoaji elimu. Nadhani hakuna jambo muhimu kama hili kwa sasa na elimu hii iende katika sehemu mbili; kwanza iende kwa wananchi lakini pia iende kwa watumishi katika sekta hii ya utoaji haki. Nikianza na mahakama kwa mfano ni vizuri watu wakaelewa sheria, wananchi wakaelewa sheria wakaelewa na jinsi ya kupata haki zao kwa kutumia sheria lakini pia watumishi wa mahakama wakapata mafunzo ili wananchi wanapokwenda mahakamani waone mahakama kama mahali rafiki, wasione mahakama kama ni mahali ambapo ni pa kuogopwa au ni mahali ambapo ni pa mabavu na kadhalika. Kwa hiyo, elimu ni muhimu katika sekta hizo zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri elimu ingetolewa sawa sawa hata malalamiko kama baadhi ya yaliyoletwa hapa juu ng'ombe waliokamatwa ambao ni suala la kukaza hukumu ya mahakama siyo suala la kuja kwa Waziri Ndumbaro tena. Nafikiri hata hayo tusingepata tabu kwa sababu hukumu ikishapatikana uko utaratibu wa kui-*execute* wa kuikaza kwa Kiswahili wanasema kwa hiyo hayo yote yanaashiria kwamba tuna changamoto juu ya watu ya kuelewa mfumo jinsi ya kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata suala la katiba mpya *for that matter* lisipotanguliwa au kwenda sambamba na elimu ya kutosha halitaleta tija yoyote. Tutakuwa na katiba imekaa hapo nzuri, hata kama iliyopo na kama hii ambayo iko hapa sasa hivi ambayo ina haki karibu zote lakini iko kabatini watu hawana

uwezo wa kuitumia wala kuweza kupata zile haki zao ambazo ziko ndani ya katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri mambo machache sana. Nimeona katika ukurasa wa 36 wa ripoti ya kamati imetoa ushauri kwa Tume ya Kurekebisha Sheria juu ya kufanya mambo mbalimbali. Ningependa kuongeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametaja pale kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria ishauriwe juu ya masuala ya Sheria za Ardhi. Tumejenga mahakama nzuri sana maeneo mengi ikiwa ni pamoja na Jimboni kwangu Mwanga lakini bado ukiwa na suala la ardhi utatakiwa kwenda Baraza la Kata ambalo kazi yake ni kutoa ushauri tu kusuluhisha kama vile masuala ya kusuluhisha ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapo lazima uende Mahakama ya Ardhi ambayo pale Mwanga haipo. Mahakama za Ardhi ziko chache tena haziko chini ya *Judiciary,* chini ya mahakama ziko chini ya Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo hiyo inaleta changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama iliwezekana kwa Mahakama Kuu kuwa na mamlaka ya kushughulikia mashauri ya ardhi na mashauri mengine ya kawaida sioni kwanini sijapata maelezo ya kutosha kutoka kwa Wizara kwamba ni kwa nini sheria isirekebishwe, mahakama za wilaya na mahakama za mahakimu wakazi zikaweza pia kushughulikia mashauri ya ardhi kama iliwezekana *High Court* naamini hata huko inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo linahitaji marekebisho ni juu ya hizi Sheria za Mienendo, *procedure* ambazo nilipata kusema hapa kwamba zinanyima haki sana watu kutokana na *procedure* zenyewe kuwa mzigo.

Kasuala kadogo kanatokea mtu amekamatiwa mizigo yake alikuwa anapeleka sokoni labda ni vitu vya kuharibika nyanya sijui na mihogo lakini kama imekamatwa na mamlaka ya Serikali akitaka kwenda mahakamani lazima atoe notisi ya siku 90. Nyanya zinaharibika ndani ya siku 90 na mihogo inaharibika. Kwa hiyo, analazimika tu kufuata kile anachoambiwa afanye hata kama anaona hakuna haki yake lakini afanye nini hawezi kufuata hiyo *procedure* ambayo ni mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hata kwenye mizani pale, mtu amekamatwa kwenye jambo ambalo ana hakika kabisa haki yake ipo lakini saa ngapi aende mahakamani aanze kutoa notisi ya siku 90 wakati mzigo ule ameubeba na fedha ya mkopo benki ambayo mwisho wa mwezi kuna marejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusipohangaika na hizi Sheria zetu za Mienendo zikarahisisha mienendo kwa baadhi ya mambo hata kwenye zile haki za msingi ambazo ziko ndani ya katiba. Nitoe tu mfano kwa mfano juzi hapa kule Mkoa wa Kilimanjaro wameandamana watu kupinga haya mambo ya ushoga. Nawapongeza wamefanya kitu kizuri sana lakini nafikiria tu kwamba angetokea mtu asiyejua haki za watu akawanyima kibali cha maandamano, wangefanyaje. Wangetakiwa kwenda ku-*challenge* ile. Sasa ku-*challenge* unatoa notisi ya siku 90 wakati watu wanaangamia na ushoga uko wapi na wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufike mahali turekebishe Sheria zetu za Mienendo zirahisishe jinsi ya kupata haki mbalimbali katika maeneo ambayo ni ya muhimu. Asilimia 90 mimi nasema ya haki katika katiba yetu na katika sheria zetu, zipo zinaweza zikapatikana, tatizo ni namna ya kuzipata ule mlolongo wa kuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mfupi tu kwa kumalizia tu imetamkwa hapa Bungeni kwamba Serikali imeshindwa kukusanya fedha zile za *Plea Bargaining.* Naheshimu sana huo mchango lakini nalazimika kutoa na maoni yangu. Wote tunafahamu kwamba mambo yale ya *Plea Bargaining* yalifanyika ilikuwa inafanyika na watu ambao wako ndani wako, jela. Mtu ameshakaa miaka miwili na kule hata mawakili, mimi nilikuwa wakili wakati ule, mawakili tulikuwa tunakatazwa kushiriki kwenye ule mchakato. Kwa hiyo, yalikuwa ni mambo ya kulazimisha, yalikuwa ni mambo ya kuumiza watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kipindi hiki ambacho tunataka kurekebisha mambo yaliyotokea nyuma ambayo yalitesa watu sidhani kama kuna haja ya kuanza kufikiria kuanza kuwakamata tena watu katika mambo haya ambayo katika *spirit* ya maridhiano tulishaona kwamba hayafai. *Plea Bargaining* maana yake ni *bargaining,* mnakaa mnapatana kwa hiari kama unaona haifai mnakubalina. Ku-*bargain* ni kama mnavyo-*bargain* bei na machinga kule ilimradi maslahi ya pande zote mbili yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile iliyokuwa inafanyika kama kuwekewa *pistol* hapa mtu yuko ndani miaka miwili analazimika kuchangiwa kuuza vitu kufanya nini halafu leo hii tumeshapata *reliefs* sasa tunaanza kuweka mambo sawasawa ili twende mbele, tunaanza kusema kwamba tuanze kukamata tena watu. Nafikiri hii siyo sahihi, ipo haja ndiyo ya kupitia baadhi ya zile kesi lakini nyingi kati ya zile kesi ile *Plea Bargaining* haikufanyika katika utaratibu ambao unakubalika kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sishauri hilo ambalo mwenzangu ameshauri, mimi naomba kutofautiana naye na kushauri Serikali

kwamba utaratibu huo hautafaa. Yale yaliyolipwa bila utaratibu *fine* yamelipwa, tuangalie utaratibu mwingine lakini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Eric Shigongo lakini naongeza nusu saa ili tuweze kukamilisha kazi yetu.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niamini kwamba tunachangia kwa dakika 10 na ninataka nizitumie dakika 10 hizi kwa kutoa mchango wangu kwa kifupi tu na ninaomba Wabunge mnisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 144 imetamka juu ya *Security of Tenure*. *Security of tenure* ya kwamba ziko nyadhifa katika taifa hili lazima watu walindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma kidogo Ibara ya 144(1); Bila kuathiri masharti mengine yaliyomo katika ibara hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Jamhuri ya Muungano atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini au umri mwingine wowote utakaotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yeyote).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ibara hii kuonyesha ya kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

imetamka wazi kwamba *CAG* awe *protected* na hiyo *security of tenure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko katika vita dhidi ya rushwa kwenye Taifa letu. Mara ya mwisho niliposimama hapa nilisema kwamba watu wanaiba, wanaiba, wanaib. *CAG* ameleta ripoti tena hapa bado wizi unaendelea na unazidi kuongezeka. Sasa, kwa nini nimesimama kuzungumza, nimesimama hapa kwa sababu ya mtu mmoja ambaye ninamwona ni wa muhimu sana kwenye vita dhidi ya rushwa kwenye Taifa langu; mtu huyu ni Mkurugenzi wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa TAKUKURU ambaye *CAG* akikamilisha kazi yake anamkabidhi mafaili yote anapata kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaenda kufungua kesi mahakamani kuwashitaki watu lakini hawi *protected* na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi yake ni kubwa anashughulika na watu wakubwa, watu wenye uwezo lakini hana *protection* yoyote kama mwenzake *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, kwamba jambo hili lilifanyika kwa bahati mbaya au lilifanyika kwa lengo gani? Kwamba yule anayechukua kazi kwa *CAG* na kupeleka mahakamani na kupata kibali cha mwendesha mashtaka na kushitaki watu hawi *protected*. Ukienda upande wa pili wa Tanzania Zanzibar iko *protected,* Kenya yuko *protected,* Sierra Leone yuko *protected,* analindwa. Naongea hapa kwa sababu ya *confidence,* mtu huyu anahitaji *confidence,* awe na uhakika wa kazi yake alindwe na sheria ili iweze kutimiza majukumu yake sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukatae tukubali wako watu kwa simu moja tu mambo yanaweza yakabadilika, ushahidi unaweza ukabadilishwa na vitu vikabadilika kabisa na kesi isifike

hata mahakamani, kwa simu moja tu. Nitatoa mfano mmoja mfupi tu, Yesu alipokufa siku ya Ijumaa, Maria alipoenda kuomba mwili wake kwa Pilato, Pilato alikataa kutoa ule mwili. Mtu mmoja aitwaye Joseph Halimataya mtu mwenye nguvu na ushawishi, Maria alipoenda kwake kulia akamwambia twende, walipofika ofisini kwa Pilato akauliza mzee yupo akaambiwa yupo lakini ana mgeni, akasema ngoja nichungulie kidogo tu anione, alipofungua mlango hivi Pilato alivyomwona akasimama akamwambia karibu mzee, mgeni aliyekuwepo ndani akaambiwa subiri kwanza niongee na Joseph wewe usubiri. Kwa nini natoa huu mfano, wako watu wana nguvu, wako watu wana ushawishi, wanaweza kumpigia simu moja tu Mkurugenzi wa TAKUKURU na mambo yakabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tumpe uhakika Mkurugenzi wa TAKUKURU ili afanye kazi zake kwa *confidence,* afanye kazi yake vizuri bila hofu ya kwamba nitafukuzwa kazi kesho, ukishamteua iwe kazi kumwondoa. Maana yangu ni nini, mimi mwenyewe hapa namkumbuka kaka yangu mmoja, sitaki kumtaja jina hapa, aliwahi kusema msinitilie kitumbua changu mchanga. Hata yeye Mkurugenzi wa TAKUKURU ana watoto, ana familia kuna mambo mengine anaweza akaacha kuyashughulikia kwa sababu tu anaogopa kazi yake inaweza ikapotea. Nani hataki heshima, nani hataki kutembea kwenye hiyo shangingi kila mtu anataka hata mimi nataka. Niko tayari ku-*compromise* wakati mwingine ili nibaki ofisini. Wako watu wamedhurika kwa sababu walishindwa kutekeleza maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokiomba wakati umefika wa sisi kufikiria sasa jinsi ya kum-*protect* Mkurugenzi wa TAKUKURU. Jambo hili si geni, Zanzibar inafanyika nimesema, Sierra Leone wanafanya na Kenya wanafanya kwa nini Tanzania hatuwezi kum-*protect* mtu huyu? Umem-*protect* CAG,

anafanya vizuri, lakini Mkurugenzi wa TAKUKURU hana *protection*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo niunge mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Erick Shigongo.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha kuwa mhimili wa Mahakama ni chombo kikuu cha kusimamia utolewaji wa haki nchini. Chombo hiki ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha Ofisi ya Mahakama imefanikiwa kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ikiwemo mfumo wa usimamazi wa mashauri na kupelekea kuongeza tija katika utatuzi wa mashauri ikiwemo yaliyodumu kwa kipindi kirefu. Ofisi ya Mahakama imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini ikiwemo jengo la Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Mahakama inaendelea kukabiliwa na upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali na pia uchakavu wa majengo ya Mahakama za ngazi zote. Kama ilivyoshauriwa kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuna haja kwa Ofisi ya Mahakama kuongeza watumishi katika mahakama zote nchini ili kuongeza tija na ufanisi. Pia napendekeza Serikali kuhakikisha inatenga fedha za maendeleo za kutosha ili kuendeleza ujenzi na ukarabati Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama kuu pamoja na nyumba za Majaji ili kuboresha na kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbeya bado ina changamoto za uhaba wa Mahakama za Mwanzo na inapelekea wananchi kusafiri umbali mrefu kupata huduma ya Mahakama ya Mwanzo. Mji Mdogo wa Mbalizi wenye idadi ya watu zaidi ya 100,000, ina Mahakama ya Mwanzo ambayo ni ndogo sana na chakavu ambayo ni hatarishi kwa usalama na afya ya watumishi na hata wananchi kwa ujumla. Napendekeza Serikali ijenge Mahakama ya Mwanzo katika eneo la Utengule Usongwe ambalo limetolewa na wananchi. Pia naomba kuwepo na kipaumbele cha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo angalau mbili kwa kila Tarafa za Usongwe, Isangati na Tembela.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika Taifa letu nyakati zote kwa kutujalia amani, upendo, mshikamano na kutuepusha katika majanga mbalimbali makubwa nyakati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wetu wote kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2020 – 2025, kwani kuna mafanikio makubwa sana katika nyanja za kidiplomasia, kiuchumi, maridhiano ya kisiasa, ustawi wa jamii na utatuzi wa kero mbalimbali kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye sekta zote nchini. Aidha tunaendelea kuiombea nchi yetu baraka za Mwenyezi Mungu katika ulinzi, amani, mafanikio na mshikamano kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Rais wetu, viongozi na watendaji wetu wote awajaalie mafanikio mbalimbali katika kuliongoza Taifa letu wakati wote wanapotekeleza majukumu yao wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya Katiba na Sheria iliyowasilishwa katika Bunge letu hivi punde.

Pia Serikali iangalie mpango wa kufufua Mahakama za Mwanzo katika ngazi za tarafa ambazo zilianzishwa toka enzi za mkoloni ili kurahisisha wananchi kupata huduma za mahakama kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga mahakama zote kongwe zilizoanzishwa toka enzi za mkoloni ambayo majengo yake yote ni chakavu sana kwa sasa, mfano wake ni Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ambayo ilijengwa na mkoloni toka mwaka 1934 ambayo kwa sasa ni chakavu sana na iko ndani ya mita kumi ya hifadhi ya barabara kuu hali inayosababisha kelele nyingi sana za magari yanayopita wakati shughuli za mahakama zikiendelea na kuhatarisha usalama wa wananchi waliokuja kusikiliza mashauri ya ndugu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi nawasilisha maombi mahususi Wizarani kutupatia fedha za ujenzi wa jengo hilo la mahakama katika bajeti hiyo na tayari uwanja umeshapatikana, pia nitashukuru sana kama Wizara itatuma wataalamu wa Wizara kuja kuona hali halisi ya jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie utaratibu wa uteuzi wa wazee wa mahakama nchini kwa kuwekwa wazi kwa wananchi wa wanaopokea huduma katika eneo hilo na namna ya kuwahudumia kwani uwepo wao ni muhimu na kutaisaidia mahakama kutekeleza majukumu yake kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itoe kwa asilimia 100% fedha za ujenzi wa mahakama zinazoombwa katika kila mwaka wa bajeti nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100% na naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sasa namkaribisha Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baadaye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, atafatiwa na Mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru sana kwa nafasi hii, pia nishukuru na kuwapongeza wakuu wa mihimili yetu ya dola, Mheshimiwa Rais, Spika wa Bunge letu pia Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kusimamia misingi ya demokrasia, haki na utawala bora. Niwapongeze sana Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda huu pia nitumie kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, ambao wamepata fursa kuchangia hoja, kujibu au kuongelea maeneo ambayo yamefanyiwa wasilisho na Waziri wetu wa Katiba na Sheria ambaye amefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja kadhaa ambazo zimeibuliwa katika michango hiyo zikiwemo sheria zetu kupitwa na wakati. Katika hili ningeomba tu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wote na watumiaji wote wa sheria, kwa sasa sheria zote ambazo tungependa zitumike ni zile zilizokwishakufanyiwa rekebu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuingizwa kwenye tovuti ya Office *of the Attorney General Management of Information System,* ambako ukiingia tu unafikia *online law catalogue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi tumeendelea kuzitangaza kadri tunavyofanya urekebu, na itakapofika mwezi wa sita mwaka huu ningependa kutoa taarifa kwamba Serikali yetu tutatoa toleo la sheria zilizorekebiwa la mwaka 2023, ambako sheria zote kuu 446 zitakuwepo. Ni tendo la kuipongeza Serikali yetu kwa sababu toleo hili linakuja baada ya miaka 20 kupita. Toleo la mwisho la urekebu tulilonalo ni lile la 2002, na tena ambalo Serikali yetu ilipata ufadhili. Kwa hiyo ningependa kuipongeza sana Wizara ya Katiba na Sheria na

Serikali yetu kwa ujumla na Bunge hili kwa kuidhinisha fedha ambazo zimewezesha kazi hiyo kubwa sana kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kazi kubwa sasa ambayo tunaendelea nayo pamoja kwa kukamilisha urekebu ni ile ya kufanya tafasiri ya sheria kuu pamoja na sheria ndogo. Tayari tumekwishakuvuka asilimia 50, na katika zile sheria ndogo 29,700 tayari sheria ndogo 211 nazo tumesharekebu. Kwa hiyo fedha iliiyoombwa na Mheshimiwa Waziri wetu ni pamoja na mambo mengine itasukuma sana kufanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine vilevile tunashukuru sana maelekezo ya kiti kwa maana ya Mheshimiwa Spika, ambayo yameendana sanjari sana maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na nina kila sababu ya kumpongeza. Matumizi ya *Law Reform Commission,* Tume yetu ya Kurekebisha Sheria, kwa sasa Serikali imekwishakuamua kwamba, Tume hii itemize wajibu wake wa msingi wa kufanya utafiti kabla ya sheria hazijaletwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kila mmoja akisimama anasema Bunge liletewe sheria, kwa hiyo kuletewa kwa sheria nyingi tunazotamani ziletwe humu iendane na uwezeshaji mkubwa ambao tunatamani sana ufanyike kwenye Tume yetu ili iweze kutuhakikishia inafanya utafiti kwa kushirikiana na wadau wote na kutuwezesha katika hilo. Kwa hiyo Mheshimiwa Massare nikuhakikishie tu kwamba kwa sheria zile zilizokwishakufanyiwa urekebu makosa yale ya ukinzani yamekwishakufanyiwa kazi. Pia nikuhakikishie kwamba kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Serikali sheria zote zitakazofanyiwa utafiti zikaendelea kutokuwa na makosa mengi sana ya kiufundi au kiuchapishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia imewasilishwa kuhusu wananchi ambao wanashinda kesi lakini wanakuwa

hawajapata haki yao. Mheshimiwa Mpina ameongelea hili. Ningependa tu kueleza kwamba kwa sheria zetu zinazoongoza mienendo ya madai ni *Civil Procedure Act* ambako *Order XI* inaongelea habari ya *Executions*. Kwa Sheria ya Jinai (*Criminal Procedure Act)* Kifungu cha 353 kinaongelea namna ya kurejeshwa kwa mali iliyokamatwa kwa mtu aliyekwishakushinda kesi mpaka hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kumaliza nafuu zilizo kwenye sheria, kwa mfano kifungu cha 353, basi yule aliyeshinda na kama hajapata haki yake kuna namna ya kuwawajibisha watu wanaotatiza haki hiyo kufanyika kwa mujibu wa sheria na kama ilivyochangiwa vizuri sana na Mheshimiwa Tadayo wakati anatoa mchango wake hapa. Kwa hiyo labda, kwa sababu tuna dhamana ya kuwajibika kwa mujibu wa kazi tulizokwisha kupewa, nafikiri Mheshimiwa Mpina nitaomba kuendelea kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zetu kuona kikwazo ni kipi. Kama ni upungufu wa *legal aid* kwa wale wanaohusika basi ninaamini wajibu wetu ni kukwamua na kuhakikisha kwamba watu wanaohusika wanaendelea kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amekwishawasilisha kwenye hotuba yake, ofisi yangu kupitia idara zake hasa uandishi wa sheria, itaendelea kutimiza yale ambayo tayari yamewekwa humo. Pia tuendelee kuwaahidi kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba, kile ambacho tumekuwa tukikifanya hata kwa Mbunge mmoja mmoja anapotuletea hoja, tutaendelea kutoa majibu ya haraka na tutaendelea vilevile kufanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Katiba na Sheria; na kwa mambo yote yanayohusu mikataba. Nafikiri hili ni jambo ambalo tutaendelea kulitolea maelezo kadiri ya mikataba inavyojadiliwa, inavyohitimishwa ikiendana na mashauri ambayo yako kwenye mahakama za ndani na za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukichelea wakati mwingine kuongelea kesi iliyomalizika hatua moja lakini bado inaendelea kwenye hatua zingine au kwenye majadiliano mengine ambayo bado yanaendelea kwa mujibu wa sheria. Hoja ya mwisho ya Mheshimiwa Mpina nafikiri alikuwa anaongelea *standard charted;* jambo hili bado kuna majadiliano ya Serikali yanayoendelea na wale walio na tuzo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja na Waziri, nakupongeza sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Pauline Gekul

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru kwa nafasi, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa nafasi hii tena, kutupa afya njema kuendelea kutekeleza wajibu wetu katika wizara hii. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelekezo yake, Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kutupa imani sisi wasaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nita-*respond* kwenye mambo machache. Jambo la kwanza nimshukuru Mheshimiwa Neema Lugangira kwa mchango wake. Ametoa ushauri mzuri kwa Wizara yetu; na kubwa zaidi ametoa ushauri kwamba wakati tunarekebisha sheria hizi za vyama vya siasa basi Tume yetu ifanye kasi kuleta marekebisho hayo na tuweze kuyaleta. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ukiangalia bajeti zetu hapa miongoni mwa kasma ambazo zimetuongezea fedha katika Tume yetu hii ya kurekebisha sheria ni pamoja na

kazi hizi kumalizika na Tume yetu ilishamaliza utafiti katika sheria hizi za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema, Mbunge, mawazo yako hayo ni mazuri na yataendelea kuzingatiwa pale ambako tutaleta sasa marekebisho haya basi tutaendelea kuboresha; lakini kwa sasa kama wizara tumechukulia *serious* na ndio maana katika bajeti ya Tume kumekuwa na ongezeko la fedha ili kazi hizi ziendelee. Pia tunawapa kipaumbele kwa kuwa tunaelekea kwenye mwaka wa uchaguzi wa Serikali za mitaa na uchaguzi mkuu sheria hizi ziangaliwe kwa jicho la karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge pia ametushauri katika suala zima la katiba mpya kwamba ushirikishwaji wawe wazi, asasi mbalimbali zishirikishwe, *NGO's* na taasisi zingine na wananchi kwa ujumla washirikishwe. Hili ni la msingi, ndiyo maana tumekuja kwenye Bunge hili mkiona kwenye bajeti zetu kuna ongezeko kwa ajili ya kazi hii ya mchakato wa katiba na ni fedha kubwa. Tushukuru Bunge hili kwamba mmeliona hilo kuanzia kwenye kamati lakini Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan. Kazi hii itakapoanza tutashirikisha kote Bara pamoja na zenzetu wa Zanzibar, wananchi watatoa maoni yao mchakato utakuwa wa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la viongozi wetu wa Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia; kwamba wasiondolewe kienyeji. Kwa sasa taratibu ziko wazi kabisa chini ya Serikali zetu za Mitaa, chini ya Ofisi ya DC akisadiwa na makatibu tarafa jambo hili limekuwa likifanyika kwa kufuata taratibu, Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa haondolewi tu bila utaratibu. Lakini katika marekebisho na maboresho haya ambayo yanaletwa na Tume basi tutaliangalia kama kuna mapungufu, lakini kwa sasa utaratibu

uko vizuri na wananchi wanashirikishwa. Tunafahamu mkutano mkuu wa kijiji unakuwepo lakini taratibu hizo zinasimamiwa na ofisi zetu za wakuu wa wilaya na mambo haya yamekuwa yakifanyika kwa uwazi ili mtu pia ajitetee kama anatuhumiwa kwa jambo lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jesca amechangia kwenye Tume yetu ya Haki za Binadamu na umuhimu wa Tume hii. Tume hii ni muhimu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema. Tume hii imekuwa ikifanya kazi zake. Naomba nimrifae *(to refer)* Mheshimiwa Mbunge katika ukurasa wa randama yetu kazi ambazo tume imefanya ukurasa wa sita mpaka saba, pale utaona kazi ambazo Tume imefanya. Pale ambako kuna ukiukwaji wowote wa haki za binadamu Tume hii haijafungwa mikono na imekuwa ikifanya kazi zake siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *good enough* taarifa zake tumeshazikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu zitaletwa kwenye Bunge hili hakuna ambaye anazuia Tume hii isilete taarifa katika Bunge hili. kwa hiyo baada ya Tume kutukabidhi hizi taarifa kama Wizara taarifa hii tumekabidhi Ofisi ya Waziri Mkuu na taarifa hizi zitaletwa katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni suala la bajeti ya Tume hii. Mheshimiwa Mbunge Agnesta amelizungumzia kwa kina, kwamba tume hii haipati fedha ipasavyo. Ukiona kwenye *disbursement* ya fedha kwa mwaka huu unaondelea Tume imepata zaidi ya asilimia 60, yaani kwenye *disbursement* wamepata fedha na ndiyo maana wamefanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *increment* za bajeti kwa miaka mitatu mfululizo Tume hii imekuwa ikiongezewa fedha ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo. Na tumeona, miaka mitatu mfululizo bajeti yao ilikuwa *five billion,* lakini mwaka uliofuata *six billion,* mwaka huu Bunge lako Tukufu

litakaporidhia, na tunashukuru kamati zimeridhia bajeti hii ya ongezeko kwa Tume, Tume imepitishiwa zaidi ya *eight billion* ambayo kwa kweli sisi kama wizara tunafahamu umuhimu wake. Kimsingi ndiyo maana tunaona katika nyongeza za bajeti Tume hii haijaachwa. Kwa hiyo nimwakikishie Mheshimiwa Jesca kwamba Tume hii itaendelea kufanya kazi zake kwa umakini pia Serikali na Wizara tumekuwa tukiangalia kwamba inapata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba fedha za maendeleo ni kweli lakini Tume haisimami peke yake. Wizara hii tuna taasisi nyingi tumekuwa tukishirikiana katika miundombinu. Tume haijakwama kazi zake kwa kuwa haina miundombinu, ndiyo maana hata kwa upande wa Zanzibar Tume ina ofisi zake. Kwa hiyo kadri tunavyoendelea kupata fedha na kutenga fedha kwa ajili ya Tume hii na hata miundombinu tutaendelea kurekebisha vile ambavyo bajeti itaendelea kuruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namkaribisha Mtoa hoja, Mheshimiwa Daktari Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Daktari Jaji Feleshi kwa maelezo aliyoyatoa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Pauline Philipo Gekul kwa maelezo ambayo ametoa katika kujibu hoja mbalimbali za waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo hoja aliyoizungumzia Mheshimiwa Agnesta kuhusiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa mujibu wa Mkataba wa Paris umeweka viwango kwamba Tume za Haki za

Binadamu zianzishwe ama kwa Sheria ama kwa Katiba, sisi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Tume hii tumeanzisha kwa nyaraka zote mbili Sheria pamoja na Katiba. Tumeiweka kwenye Katiba ili isiweze kuguswa na kuchezewa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuweka Tume hii katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni dhamira wazi kabisa kwamba Serikali imeipa Tume hii heshima kubwa sana na kwamba haiwezi kuchezewa au kufutwa na mtu yeyote kirahisi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Agnesta akubaliane nami kwamba Tume hii ni Tume ambayo sisi kama Serikali tunaiheshimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiongeza Bajeti ya Tume kila mwaka. Mwaka 2021/2022, Bajeti ilikuwa ni bilioni 5.5, lakini leo nasimama hapa mapendekezo ya Bajeti endapo Bunge hili litaridhia na endapo Mheshimiwa Agnesta ataunga mkono ni Shilingi Bilioni 8.1 ongezeko takribani ya Shilingi Bilioni 2.6. Hiyo inaonyesha kwamba Serikali inaongeza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Agnesta ni Fedha ya Maendeleo. Fedha ya Maendeleo inatumika kujenga Miradi ya Miundombinu na Tume hii kwa sasa hivi haihitaji Miradi ya Miundombinu. Fedha za *Operations* ya Tume inatokana na *OC* na katika mwaka huu wa fedha mpaka kufika Machi, Tume imeishapata bilioni 2.2 na imetumia fedha hizo kufanya kazi za kutosha sana. Kwa hiyo kuna utofauti hapa Mheshimiwa Agnesta kati ya fedha za maendeleo na fedha za *operations,* fedha za *operations* ziko kwenye *OC* na tayari Tume hii imeishapokea asilimia 69.79, takribani asilimia 70 na hatujamaliza mwaka. Hii asilimia 30 iliyobaki itakamilika mpaka kufika Juni. Kwa hiyo Tume imepata fedha hizi za *operations*,

maendeleo ni miradi ambayo Tume hii haina miradi kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hoja alizozitoa Mheshimiwa Luhaga Mpina. Hoja ya kwanza ameshajibu *AG,* nisingependa kurejea lakini niseme tu pale ambapo mtu ameshinda kesi, amemshinda mtu yeyote yule achilia mbali Serikali, kuna utaratibu wa kisheria wa kukazia hukumu. Sasa hawa watu wana haki ya kufuata utaratibu huo wa kukazia hukumu, iwe dhidi ya Serikali iwe dhidi ya mtu mwingine yeyote sheria zetu zimeweka utaratibu mzuri. Tukiaanza kulitumia Bunge kukazia hukumu za Mahakama, tutakuwa tunaingilia Mhimili wa Mahakama, kwa hiyo tusimame kwenye misingi ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mpina, ameongelea suala la Tume ya Haki Jinai. Tume ya Haki Jinai hii ni maono na maelekezo na matakwa ya Mheshimiwa Rais, ili kuboresha mfumo wa haki jinai ambao tuliurithi toka wakati wa ukoloni. Kwenye hili tunapaswa kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuja na wazo hili na sisi tunaamini matokeo ya Tume ya Haki Jinai yatasaidia kuboresha mifumo ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina, ameongelea suala la Azimio la Kufuta Hasara ya Fedha kama ambavyo liko kwenye taarifa zangu. Alichokisema yeye ni ni kwamba hili jambo lililetwa lakini halijajadiliwa. Sasa hili ni jambo la Ushahidi, niombe kiti chako kitoe mwongozo kwa sababu tunahitaji sasa kwenda kwenye *Hansard* na kupitia kumbukumbu zote, tujue kama anachokisema ni kweli au siyo kweli na hatuwezi kukimaliza hapa bila kuomba Mwongozo wa Kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mpina ameongea suala la Ofisi ya Mwendesha Mashtaka kushindwa kukusanya shilingi bilioni 170. Najaribu kutafuta nitumie maneno gani kwa sababu tayari kiti kilishatoa mwongozo kwamba mambo yote yaliyokuwemo kwenye Taarifa ya *CAG* tutayajadili kwa mujibu wa utaratibu na Kanuni za Bunge tulizojiwekea. Sasa akinitaka mimi na Serikali tujibu leo, wakati utaratibu huo haujafika, tunakiuka hata miongozo ya Bunge ambayo tumejiwekea sisi wenyewe. Kwa hiyo tumwambie Mheshimiwa Mpina, tukifika wakati wa kujadili Taarifa za *CAG* jambo hili tutaliongea na Serikali itatoa maelezo yake wakati huo ukifika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina, vile vile ameongelea suala la upekuzi wa Mikataba na akasema kwamba kuna Mikataba kwa mujibu wake yeye anaona haijafanyiwa kazi na *AG*. Jambo hilo liko kwenye aya ya 53 ya Taarifa ya Bajeti ambayo tumeileta leo. Kwenye hili tunapaswa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sababu katika mwaka huu wa fedha amepekua mikataba mingi zaidi kwa asilimia 11 kuliko ilivyokuwa mwaka jana. Kwa hiyo amefanya ufanisi zaidi, mtu ambaye amefanya ufanisi tunapaswa kumpigia makofi mengi na kumpongeza na kwa taarifa tu ni kwamba mikataba yote iliyosainiwa ndani ya kipindi husika imepekuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa aya hii ya 53, hakuna Mkataba ambao haujapekuliwa. Ameongelea Mikataba ambayo imethaminishwa ambayo kwa mujibu wa taarifa hii ukurasa wa 28 ni mikataba 567. Mikataba yote iliyopekuliwa ni 1,304. Sasa siyo kila mkataba una thamani ya fedha, kuna mikataba mingine ni *memorandum of understanding* au ni makubaliano ambayo hayataji fedha mle ndani ambayo ina thamani ya fedha milioni 567. Kwa hiyo niseme kwamba hoja hizo ambazo amezisema Mheshimiwa

Mpina ni hoja ambazo sisi tumezifanyia kazi isipokuwa hili moja tu ambalo tutaomba Kiti kitupe mwongozo kwa kadri kitakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbalo ahsante sana na hoja imeungwa mkono. Katibu tuendelee na utaratibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajielekeza katika kitabu chetu cha pili, matumizi ya kawaida na katika kishikwambi tutatumia dirisha la vitabu vya mpango wa bajeti na tutatumia kitabu cha pili, *Estimate of Public Expenditure Consolidated Funds Services and Supply Vote Ministerial* na tutaanza Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, Ukurasa wa 380.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administrations and Human Resources Management Division*....................Sh. 7,635,961,980

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kifungu kilichotajwa ni cha Mshahara wa Waziri, hapo tuna wachangiaji watatu ambao wameomba kushika shilingi. Tutaanza na Mheshimiwa Simon Songe, Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda ili tumalize shughuli yetu.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ufafanuzi pamoja na kwamba hapa mwishoni Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake ameomba wewe utoe mwongozo. Tarehe 14 na 15 mwezi Septemba, mwaka jana kwa maana 2022 Kamati ya *PAC* ilijadili hoja ya Azimio la Kufuta Hasara kwa Serikali lenye thamani ya bilioni 19.7 ikiwa maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa bilioni 8.5, upotevu wa fedha milioni 453, matumizi batili bilioni 1.4 na upotevu wa vifaa bilioni 9.4, jumla kuwa na bilioni 19.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya tarehe 16 Septemba, 2022, *Order Paper* ilikuwa na hoja hii na Mheshimiwa Anatropia, kwa niaba ya Mwenyekiti aliwasilisha Hati hii Mezani na Naibu Waziri wa Fedha naye aliwasilisha Hati hii Mezani, lakini baada ya maswali na majibu Mheshimiwa Naibu Spika, kama sikosei ndiye aliyekuwa amekaa na walitoa hoja hii na haikujadiliwa na hayakuwa Maazimio ya Bunge lako tukufu. Sasa leo yamekuwa kwamba ndiyo maazimio ya Bunge.

Nataka tu ufafanuzi kwamba yalipitishwa lini na je, yalivyofutwa siku hiyo ilimaanisha kwamba ndiyo yalikuwa maazimio ya Bunge? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwamba jambo hili linataka ushahidi kwenda kwenye *Hansard* kuangalia kumbukumbu na kujiridhisha kama ilikuwa ni kosa au siyo. Hili tuliomba Mwongozo wa Kiti chako na endapo itabainika kwamba jambo hili halikupita, basi tutakuwa tayari kupokea maelekezo ya Kiti na kufanya masahihisho stahiki**.**

**MWENYEKITI:** Sawa. Tutarudi kwenye *Hansard* na kuangalia na baadaye kutoa maelezo, nafikiri tumemaliza.

Tunaendelea na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya Usimamizi wa Mikataba na kama ambavyo nilivyosema kwamba ni kweli kabisa kwanza suala la kufanya upekuzi kwa Mikataba yetu ni suala ambalo ni la muhimu sana ili kuweza kufahamu mikataba hiyo ina nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nilichokuwa nakiomba hapa kikubwa niliomba bango kitita linaloonyesha hiyo Mikataba iliyofanyiwa upekuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kujua Mikataba hiyo inahusu nini? Ni ya Mradi gani? Katika kufanya hivyo nimesema hapa kwamba mikataba iko 1,304 iliyofanyiwa upekuzi, iliyopewa thamani au iliyothamanishwa ni Mikataba 567 tu ambayo hiyo 567 ina trilioni 91 na nikasema bila Bunge hili kujiridhisha na hilo jambo inaweza kujikuta Serikali imeenda kuingia Mikataba ambayo

wala si yale tuliyokubaliana hapa Bungeni, yawezekana hayamo hata kwenye Mpango wa Maendeleo, yawezekana hayamo hata kwenye bajeti, yawezekana hata uwezo wa nchi kumiliki kuiweza kuihudumia hiyo mikataba haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshafanya upekuzi, sasa ni nini kilichoshindikana kuweka *annex* ya Mikataba hiyo ili Bunge lako lijue. Hata hivyo, aliposema Waziri kwamba zingine ni *memorandum (MOU)* siyo kweli kwa sababu Mwanasheria alisema ukaguzi wa mikataba na alifanya upekuzi wa *MOU*. Kwa hiyo, naomba Waziri ajibu hapa kwamba hilo Bango Kitita analileta na kama halileti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Luhaga Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu linasimamia shughuli za utekelezaji wa Serikali kupitia Kamati, lakini kupitia Bunge lenyewe. Katika Taarifa hii ya Bajeti tumesema kuhusiana na mikataba kwenye aya ya 53, ukurasa wa 27, tumetoa *summary* ya hiyo Mikataba na thamani yake, lakini hatujaambatanisha huo mchakato wa hiyo Mikataba yote 1,304. Tukisema tuiweke hapa inawezekana, lakini nyaraka hii itakuwa kubwa sana. Endapo Bunge lako na Kiti kitaelekeza, basi kupitia Kamati stahiki tutapeleka taarifa hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Luhaga Mpina, umeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu na Mheshimiwa Waziri na sababu za kutoridhika nayo mwezi Februari hapa, Kamati ya Katiba na Sheria ilipoleta taarifa yake nilihoji juu ya jambo lile, nikasema bango kitita hili ni muhimu sana ili kuliwezesha hili Bunge lielewe Mikataba hiyo ni ya nini? Sasa kama leo tena analeta rufaa tena ya kupeleka kwenye Kamati wakati toka mwezi Februari tulimwomba, naomba kwamba Bunge lako likubali na Wabunge waunge mkono hoja, tuijadili hii mada na kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa anaweza akavuta tu akatuletea kwenye vishikwambia sisi tukaiona hiyo *annex,* hili Bunge lako hili liweze kutenda haki kwa niaba ya Watanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Waziri amesema tayari itapelekwa kwenye Kamati, sasa tunajadili nini tena?

Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Katimba na baadaye Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri amesikika akitoa kauli ndani ya Bunge hili Tukufu na amesikika akisema na akitoa *commitment* kwamba Bungeni pataletwa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ili Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 13 na 17 ambacho kinaruhusu mtoto wa kike kuolewa chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mahakama ilitoa hukumu na ikatoa muda ambao inabidi Serikali ilete Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo ndani ya Bunge hili na huo muda kimsingi umeshapita. Nataka Waziri atoe kauli yake ni lini wataleta Muswada huo ndani ya Bunge hili tuweze kufanya

marekebisho na nisiporidhishwa na majibu ya Serikali nakusudia kuondoka na shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Zainab Katimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Rufani ni kweli ilitoa maelekezo hayo kwamba Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho kwenye Kifungu cha 13 na Kifungu cha 17 ili kutoruhusu mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18 kuoa au kuolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjulisha Mheshimiwa Zainab kwamba, Serikali ilileta mapendekezo haya Bungeni na yakaenda kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ambayo ni sehemu ya Bunge lako Tukufu, kwa utashi wa Bunge lako Tukufu kupitia Kamati hiyo, Bunge lilituagiza tukapate maoni zaidi kutoka kwa wadau mbalimbali. Naomba kumjulisha Mheshimiwa Zainab kwamba tumekamilisha zoezi hilo na endapo Mungu atatujalia afya kesho Tarehe 26 Aprili, tuna kongamano pale Morena kujadili hayo maoni ambayo yamekusanywa na baada ya hapo ndipo tutaweza kuleta Muswada huo hapa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri na ningependa nitoe hoja Wabunge wenzangu waweze kuniunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya hoja imeungwa mkono. Nitaanza na Judith Kapinga upande wa huku halafu Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani, Mheshimiwa Waziri kasimama.

**MBUNGE FULANI:** Ni mchangiaji.

**MWENYEKITI:** Ni mchangiaji, haya nitakupa nafasi hamna neno. Mheshimiwa Judith Kapinga tuanze. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ni sheria ambayo haijaanza kulalamikiwa leo wala jana. Hii ni sheria ambayo kwa muda mrefu tumekuwa tukisema, tukiongea. Wote tunafahamu Katiba yetu inavyosema. Mahakama ni *very independent,* ni taasisi ambayo ikitoa maamuzi yake ni lazima yaheshimiwe kwa maana ya Ukuu wa Muhimili huu. Tukifanya masihara ya kwamba maamuzi ya Muhimili kama wa Mahakama yakafanyiwa siasa, sasa kama Taifa tutakuwa hatuendi katika njia ambayo ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama imesema tubadilishe Sheria, lazima tubadilishe sheria. Kwa hiyo, Waziri alitakiwa kutuambia mabadiliko ya sheria yanaletwa lini hapa Bungeni? Na kwa ninavyofahamu mimi, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria atasema, haya mambo ambayo yanasemwa kwamba Muswada ulipelekwa kwenye Kamati, haukupelekwa kwenye Kamati! Kamati itasema hapa itatuambia ukweli, kwa hiyo Mahakama imekuja na haya maamuzi siku nyingi, imetoa

muda, fanyeni marekebisho kama Muhimili ambao unatenda haki kwa Taifa letu hausikilizwi, *then* kama Taifa hatuendi katika njia ambayo ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi tumeweka misingi ya kwamba kila mtoto wa Taifa hili atapata elimu na elimu msingi sisi wenyewe tumebadilisha mpaka kufikia Kidato cha Nne, lakini sasa mazingira ambayo tunaweka kwenye sheria zetu lazima ya-*support* sera ya elimu ambayo tunayo, sasa kama tunaruhusu mtoto wa miaka 14 aolewe...

**MWENYEKITI:** Muda umeisha Mheshimiwa Judith, tunaendelea na mwingine. Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linapokuja suala la watoto hata kama ingekuwa ni nini lazima wote hapa tusimame, lakini zaidi hapa kesi hii ilifunguliwa 2016, Mahakama Kuu ikatoa maamuzi na ikasema kifungu (13),(17) ni *uncostitutional.* Sasa swali, tusipoheshimu kinachosemwa na Mahakama yetu, tena kinatuambia hii ni *unconstitutional* na wote tume – *swear* hapa*,* tumeapishwa hapa wote tumeshika Katiba tukasema, Katiba lazima tuheshimu. Hakuna kitu kibaya sana kama utakutana na maamuzi ya Mahakama yanasema kifungu hii ni *uncostitutional* halafu bado tunavuta miguu kuleta marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani na kwa kuwa Serikali ilienda *Court of Appeal* na wakashindwa vilevile bado Mahakama ilisema nendeni mkabadilishe sheria. Mheshimiwa

Waziri *I think the most reasonable thing* ni useme unaleta marekebisho haya, Bunge la Septemba. Ukisema utaleta Bunge la Septemba utaeleweka. Ulipokuwa unasema kwamba umeleta kwenye Kamati ya Katiba na Sheria mimi nadhani labda ni Bunge lililopita, lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria, *I don't remember* haya yakiletwa kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tu Mheshimiwa Waziri, Wakili Msomi tunakupenda sana, *just say* unaleta Semptemba, kwani kuna shida gani? Ili upitishiwe bajeti hapa, haya mambo ya kuchukua maoni, maoni ya kitu gani kwenye *section* (13) na (17) na tayari kuna *directives* za Mahakama?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene nimekutaja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani, nadhani, nadhani tumeamua tu kulisema kwa sauti kubwa jambo hili, lakini kama ni kuelewana ni tayari Serikali na Bunge wamekwishaelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mosi, Muswada huu ulikuja hapa Bungeni na Muswada ulipofika hapa Bungeni ukaonekana kwa mazingira ya wakati ule nguvu ya wadau huko nje na yenyewe kelele imekuwa kubwa, ikaonekana kwamba pengine kuna haja ya kukusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau. Maoni ambayo Serikali inasema tayari inamalizia kesho, sasa mnatakaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yanasemekana Serikali tunamaliza maoni kesho, kuna mkutano mkubwa Morena na Waheshimiwa Wabunge ambao mnataka karibuni, mje mtoe maoni yenu tumalizie, tuingize Sheria hii humu Bungeni tubadilishe Sheria. Sasa kama mnataka kuzungumza tu, kama tunataka tuzungumze tu hakuna kitu tutakachozungumza, wala Serikali haitakuwa na jibu jingine zaidi ya kusema tulisikia maoni ya Bunge, kwamba twende tukapitie tupate maoni ya wadau zaidi, tayari Serikali imekwisha kufanya hilo. Sasa mnalotaka lifanyike linafanyika ipi? Maana linalofanyika ndiyo hilo la kukusanya maoni na tayari hatua za mwisho zimefikiwa na kwamba kesho kuna mkutano mkubwa Morena karibuni Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Salome Makamba karibu sana, kesho njoo utoe maoni ili tufikirie hasa lini tulete hii sheria hapa tuibadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba Serikali haiheshimu maamuzi ya Mahakama siyo kweli. Serikali inaheshimu maamuzi ya Mahakama na ndiyo maana ikaandaa Muswada na kuuleta hapa. Ulipofika hapa ndiyo ukapata maoni mengine. Waheshimiwa Wabunge ninyi hapa mnafikiria kusema tu kwamba tukabadilishe sheria ni jambo rahisi, twendeni tuichukue hiyo sheria tuilete hapa kama mtaona huko *reaction* itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo baadhi ya imani ambazo haziamini katika hicho mnachotaka kukifanya, yako makabila ambayo hayaamini katika hicho mnachotaka kukifanya, ziko *positions* nyingi siyo jambo rahisi kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nasema twendeni na *version* hiyo kwa sababu ndiyo msimamo tulionao mpaka sasa kwamba lazima tubadilishe sheria na sisi Serikali tunasema sawa, tumeleta Muswada, haukutengenezwa na mtu mwingine Serikali ndiyo imetengeneza. Tumefika hatua nzuri hii hatuna

sababu ya kubishana, tupe nafasi Serikali kesho Wabunge waje, watoe maoni yao, tulete hapa sheria wakati wowote ambao Bunge litakuwa lina nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Simbachawene. Mheshimiwa Taska nimekuona hapo, halafu Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Wakili Msomi *Advocate* Zainab Katimba kwa kuleta hoja hii hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba suala hili limejadiliwa kwa muda mrefu, tumekuwa tukiomba sheria hii ibadilishwe kwa sababu ya madhara yaliyopo kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zinakinzana kuna Sheria ya Mtoto inasema kwamba umri wa mtoto ni miaka 18, ukija kwenye Sheria ya *Education Act,* mtu akimpa mimba mtoto ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 ambaye ni mwanafunzi anafungwa jela miaka 30. Sasa kama unamfunga mtu akimpa mimba mwanafunzi ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18, kwa nini unaruhusu mtu amuoe mwanafunzi mwenye miaka 15? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina *logic*, sheria zinakinzana, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto na Sheria ya *Education Act* na Sheria ya Jinai.*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska endelea.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huo bado haujaingia hapa Bungeni.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muache amalizie mchango wake.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huo haujaingia hapa Bungeni, labda kama ulienda kwenye Kamati lakini kwa kumbukumbu zangu sikumbuki kuuona Muswada kuingia hapa. Kingine maamuzi ya Mahakama ni maamuzi ya mwisho hamna sababu ya kujadili tena huu Muswada. Sheria iletwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunamalizia na Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waheshimiwa Wabunge, watu huko watoto wanajua ni zamu yetu sisi, yaani kama ni kubutua mpira tumebakishwa sisi tu! Sijui kama tunajua tunayemzungumzia ni mtoto? Sasa mimi ni mama na ni mama wa mabinti. Mimi ningeolewa nikiwa na miaka 14 leo msingekuwa na Nusrat ambaye nazungumza hapa leo. Siko tayari kuingia kwenye *list* ya Watunga Sheria ambao tutashindwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa, haiwezekani. Kwa hiyo ni wakati wetu sisi wa kuamua na siyo kwamba tuna mashaka na Serikali lakini ukiumwa na nyoka unakuwa na wasiwasi, ni muda mrefu sana tumejadili kuhusiana na Sheria ya Ndoa na namna ambavyo inakandamiza haki ya watoto na Mtoto wa Kike kupata elimu na ku-*access resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Serikali tumeshamaliza kukusanya maoni, maoni tumeshasema na tunajua kuna changamoto huko ndiyo maana tulitaka pia Sheria za Kimila na sheria nyingine za hivyo vingine ambavyo

mnapata navyo kigugumizi, waingie waangalie kwa namna gani ambavyo Serikali inaweza. Tunahitaji hiyo sheria kwa sababu ni wakati muafaka umefika, leteni sheria tufanye marekebisho kwa sababu ukweli ni kwamba hata Bunge bado halijaanza kuzungumza kwenye *documentation* hakuna hatujawahi ku-*table* Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Ndoa kwa hiyo tunazungumza kama *process*, sasa *process* zimeisha *it is time now* tulete sheria tufanye marekebisho tumpe hakim toto.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri baada ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwamba kwenye Bunge hili Tukufu sisi wenyewe tumetunga sheria mbalimbali ambazo zinatambua umri wa mtoto ni zaidi ya miaka 18, kuna sheria mbalimbali, Sheria za Jinai, *SOSPA*, inatamka kabisa umri wa mtoto wa kike, ukijihusisha katika mapenzi na mtoto wa kike wa chini ya miaka 18, awe ameridhia awe hajaridhia, amekubali hajakubali huo ni ubakaji. Kwa hiyo, sheria zetu nyingi hata kwenye Sheria ya Elimu imejibainisha kabisa kwamba mtoto inabidi aende shule.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab malizia.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Kuna Sheria ya Elimu lakini hata ukienda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba umri wa wa mtoto inabidi uwe kuanzia miaka 18 na kuendelea. Kwa hiyo sasa Mahakama yenyewe imetupa tafsiri na kusema kwamba kifungu cha 13 na Kifungu cha 17 cha Sheria ya Ndoa kinakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unachangia, sema wewe umekubali haya maelezo ya Waziri au haujakubali?

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali namrudishia Waziri Shilingi yake kwa sharti ya kwamba, walete Muswada wa Marekebisho ya Sheria ndani ya Bunge hili kwa Hati ya Dharura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab tumekusikia lakini naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwa ufupi sana.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili siyo suala la Wabunge peke yetu ni la wananchi wote Tanzania nzima. Kwa hiyo, ushauri wa Serikali hata kama Mahakama imeshatoa muda mrefu hukumu, lakini mchakato wa Muswada wa Sheria ninyi mnajua Wanasheria wote mko hapa, lazima tupitie kila kipengele hata hiyo Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ilipitia *White Paper* Tanzania nzima walishirikishwa, kwa hiyo vitu vingine tusilazimishe kufanya kwa haraka. Serikali tumewapa muda wamekubali na wataleta. Ugomvi umekwisha, tunaheshimu na tunathamini maoni yetu wenyewe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima subiri kuna hoja ya Salome Makamba, Mheshimiwa Salome Makamba. Hoja ya Mheshimiwa Zainab imekwisha mwenyewe amekubali amerudisha Shilingi kwa Waziri. Mheshimiwa Salome malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu kabla ya kuendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma Kanuni ya 122(5) na (6) sawa, ambayo inasema kwamba hoja ikishatolewa, Wabunge wanachangia hoja ya kuondoa Shilingi ambayo imechangiwa kwa muda usiozidi dakika Tatu. (6) Kinasema Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo, sasa Wabunge hoja ametoa Mheshimiwa Katimba, Wabunge wamechangia hoja, *expectation* ilikuwa Waziri ajibu atoe *commitment,* huu Muswada unakuja lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tena ukianza kumjibia Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba ukae nilishakuelewa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haya naomba Kanuni basi ifuatwe.

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Halima Kanuni ya 122 hiyohiyo Kanuni Ndogo ya Saba, mhitimishaji wa hoja ni mwenyewe mtoa hoja na ameshahitimisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kwenda Kanuni ya 122 (7) kabla ya Kanuni ya 122 (6).

**MWENYEKITI:** Tumeshamaliza. Mheshimiwa Salome endelea. Mheshimiwa Salome umeghairi au? Haya endelea.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeniita?

**MWENYEKITI:** Nimekuita uendelee, umalizie.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza nimuombe tu Mheshimiwa Waziri kwa busara imuongoze, akasome kifungu cha 13(2) cha *Basic Rights and Duties Act* atapata majibu kwamba anachokifanya kwenda kwenye maoni anapuyanga hoja hii tayari ilikuwa ishajifunga yenyewe.

Mheshimiwa mwenyekiti, hoja yangu hasa hapa nataka kushika Shilingi ya Waziri na kama sitaridhishwa nitashika Shilingi ya Waziri. Hoja yangu ni kuhusiana na Sheria za Habari zote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alieleza kwamba Aprili alivyoingia tu madarakani, alieleza kwamba Sheria za Habari zikapitiwe na vifungu vyote vinavyobana Vyombo vya Habari na wanahabari vibadilishwe, Julai 28, Mheshimiwa Rais pia alikutana na Wahariri wa Vyombo vya Habari Ikulu, akasisitiza hilo. Desemba 17, 2022, Mheshimiwa Nape Nauye alikutana na wadau kuhusiana na mambo ya Sheria za Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *to my surprise* kinachonishangaza Februari 10 mwaka huu, Serikali imeleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, kwenye

Muswada ule wameleta Mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari na wameleta vifungu wanavyotaka kuvibadilisha ni Nane tu kati ya vifungu 35 ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Habari alikaa na Wanahabari kongamano kubwa la kitaifa, wakakubaliana watakuja kuvibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameleta Vifungu Nane tu kati ya vifungu 16, 16 ambavyo Mahakama ya Afrika Mashariki ilisema vifungu hivyo ni batili, viko kinyume na Mkataba wa Afrika Mashariki, vinakiuka haki na uhuru wa habari na wanahabari.

**MWENYEKITI:** Toa hoja Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa Waziri hivi ni kwanini wanawahadaa Watanzania hasa wanahabari? Juu ya suala la mabadiliko ya vyombo vya habari na wanahabari, wametuletea nusu mkate ambao upo kwenye ngazi ya Kamati na utaingia ndani ya Bunge hili hivi karibuni jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya Serikali na wananchi. Nisiporidhika nitashika Shilingi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *instruments* ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais, masuala yote yanayohusu vyombo vya habari na sheria zinazohusu masuala

ya taasisi zote za habari, zimewekwa kwenye Wizara nyingine husika na siyo Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, kwa utaratibu huo naomba tu kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwa mujibu wa kifungu cha 71 cha Kanuni zetu za Bunge, Mbunge anatakiwa kuzungumza mambo ambayo yako kwenye mjadala ulioko sasa, kifungu hicho cha 71(1),(c) kinasema: Mbunge hatazungumzia jambo ambalo.... *sorry* siyo cha 1(c) ni kifungu 1(d) Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko katika mjadala unaoendelea sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba kushauri tu kikao chako na wewe utupe mwongozo wako, kwa nini jambo hili lisisubiri kule ambako Mheshimiwa Rais ameweka *instruments* za sheria hizo na usimamizi wa vyombo na taasisi hizo za habari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya mwongozo huo nisikilizeni sasa. Kwa hiyo, baada ya mwongozo huo aliotoa na Kanuni aliyoisoma hoja yako haina mashiko kwa sasa hivi. Tuendelee Katibu tunaingia kwenye *guillotine*.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*....................Sh. 7,635,961,980
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 627,294,500
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*.........Sh. 1,219,687,000
